

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Saba – Tarehe 16 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

Hali Mbaya ya Hospitali ya Wilaya – Mbozi

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Majengo ya Hospitali ya Wilaya Mbozi – Vwawa yako kwenye hali mbaya na wodi za kulaza wagonjwa hazitoshelezi hali inayosababisha msongamano katika wodi chache zilizopo:-

Je, Serikali itayakarabati lini majengo ya zamani na kujenga mengine kwa ajili ya kulaza wagonjwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ya Vwawa ilipandishwa hadhi kutoka kituo cha afya mwaka 2002 kwa kuongezewa majengo yafuatayo Wodi ya Mama wajawazito1, wodi 1 ya wanaume, *pediatric ward* 1, Chumba cha kusubiria mama wajawazito kimoja, chumba cha upasuaji, jengo la mapokezi, *isolation ward*, jengo la kliniki (*RCH*), jengo la utawala, chumba cha kuhifadhiha maiti, jengo la kufulia nguo, jengo la upasuaji mkubwa na chumba cha *X-ray*.

Aidha, ni kweli kuwa baadhi ya majengo ya hospitali hiyo yameharibika kiasi cha kuhitaji kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Halmashauri imepanga kutumia shilingi 40,000,000 kwa ajili ya kukarabati jengo la upasuaji, shilingi 28,292,648 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la utawala na shilingi 18,968,672 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wodi ya wazazi (*Maternity Ward*).

Lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma za afya zinatolewa katika kiwango cha kuridhisha na kwa ufanisi mkubwa uweze kupatikana na ili kuimarisha afya za wananchi kwa maendeleo ya taifa hili.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Mbozi ina majengo haya kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoyataja. Lakini majengo haya ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja yamechakaa kwa kiasi kikubwa sana. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati hazitoshii kufanya hata asilimia 20 ya kazi yote inayohitajiwa. Je, ni lini Serikali itakuja na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba yale majengo yanakarabatiwa yanakuwa kwenye sura ya hospitali ya Wilaya?

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, agenda kubwa na kwa majibu ya Serikali ambayo walitupa kwenye kitabu hiki ya hoja za Wabunge na majibu ya Serikali kuhusu hotuba ya Bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka 2011/2012 Serikali ilisema kwamba Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ni moja ya Hospitali 10 nchini ambazo ziko chini ya mpango wa MAM kabambe wa kukarabatiwa na kujengwa majengo mapya. Sasa ni lini majengo mapya yatajengwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ili kuondoa msongamano wa watoto na watoto na watu wazima katika wodi chache zilizopo sasa hivi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Godfrey Zambi ni kweli yaani kwamba haya majengo yako hali hiyo ni kweli. Mwaka 2006 Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilikuwa imetegemea kwamba itapata hela kutoka World Bank hela hizi hazikupatikana. Sasa hapa swali la kwanza linasema kwamba hela hizi ambazo zimetengwa hapa ni kidogo hazitoshii. Sisi wote tulipoondoka hapa ndani katika Bajeti hii iliyopita tulijus kwamba Bajeti hii ilikuwa ni kidogo. Kwa hiyo, tukajua kwamba tunakwenda lakini tunakwenda na Bajeti ambayo haiwezi kubeba majukumu yote ambayo yamekusudiwa. Mimi nataka nimwombe Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba sisi na ye ye tutashirikiana katika jambo hili.

Vwawa anayoizungumza mimi nimekwendwa na ye ye ndiye nipeleka kule nafahamu kwa hiyo litakuwa ni jambo ambalo si la busara mimi kusimama hapa nikuambie anachosema Mheshimiwa Zambi siyo ni kweli anachosema. Lakini *ours is a cash budget* hela zilizopangwa kwa ajili ya jambo hilo ni hizi tulizipata hapa. Mimi namuomba atusaidie kitu kimoja wana *special request* ambazo ameomba hebu watuletee sisi tuione wote kwa pamoja kwamba tunafanya nini kusaidia katika hali hii ya uchakavu.

Kuhusu majengo mapya, litakuwa ni suala la kipaumbele kama Mheshimiwa Godfrey Zambi anafikiri kwamba kwa kweli majengo mapya sasa ni kipaumbele pale ninachowea kushauri hapa ni kwamba watuingizie katika bajeti hii inayokuja ili ikija sisi hii tuipitishe na tuilete hapa.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi linafana sana na Hospitali ya Longido. Kwa kuwa katika Hospitali ya Longido kuna majengo yaliyochakaa na majengo mapya yanahitajika na kulikuwa na ahadi ya Serikali kujenga hospitali mpya ya Wilaya.

Je, Serikali inatuambia nini sasa kuhusu hayo majengo kwa sababu nilitarajia majengo mapya yangejengwa katika Hospitali Mpya ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na jirani yangu sana kama ifuatavyo:-

Hospitali hii inayozungumzwa na Halmashauri hii inayozungumziwa ni katika zile Halmashauri Mpya kabisa hizi ambazo sasa hivi ndizo zahanati na hali anayozungumza Mheshimiwa Lekule Laizer ni kweli anachosema hapa. Tena Hospitali ya Wilaya ya Mheshimiwa

Michael Laizer ikijengwa pale na wananchi wangu wa kule Siha nao wananaufaika katika hiyo hospitali anayozungumza hapa.

Ninachosema hapa ni kwamba hela tulizokuwa nazo ni hizo tulizokuwa nazo. Hospitali hizi, hizi Wilaya Mpya zote tunakwenda nazo awamu kwa awamu. Kinachofanyika sasa hivi siyo kujenga hospitali mpya ni kutafuta kituo cha afya ambacho tunaona kinafanana tunaki-treat kinapewa hadhi kama Hospitali ya Wilaya.

Kwa hiyo, tunapeleka vitu vyote na mambo yote yanayohusika katika ile Hospitali ya Wilaya hapo ili tupatumie kwa kipindi cha mpito kuelekea kupata hospitali mpya. Kwa hiyo, mimi nataka nimuombe ndugu yangu Michael Lekule Laizer tutazungumza tutakaa tutaangalia vizuri kwamba tunasaidiae. Kama tunafikiri sasa kwamba tuondoke katika hilo wazo na twende kwenye majengo mapya na hospitali mpya na majengo mapya yote tutaangalia. Lakini kitakacho-determine itakuwa ni suala la Bajeti. (*Makofi*)

Na. 85

Hitaji la Gari la Wagonjwa – Hospitali ya Ipamba

MHE. DKT. WILLIAM AUGUSTAO MGIMWA aliuliza:-

Hospitali ya Ipamba Teule inayohudumia Wilaya ya Iringa Vijiji:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt William Augustao Mgimwa Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ina jumla ya Zahanati 48 na Vituo vya Afya 6 vinavyomilikiwa na Serikali zikiwemo zahanati 14 Vituo vya Afya Vitatu na Hospitali Teule ya Ipamba zinazomilikiwa na Taasisi za Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji huduma za afya, kituo cha afya kinapaswa kuwa na gari moja na hospitali ya Wilaya inapaswa kuwa na magari mawili kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa wagonjwa. Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ina magari matano ambapo gari moja liko katika Hospitali Teule ya Ipamba na magari mengine manne yako katika Vituo vya Afya vinavyomilikiwa na Serikali.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilihamishia gari aina ya HYUNDAI lenye namba Sm 4452 kwenda katika Hospitali Teule ya Ipamba baada ya Kituo cha Afya cha Ismani kupata gari aina ya *Landcruser Hardtop* mwaka 2011 yaani mwaka huu. Halmashauri inashauriwa kuzingatia katika vipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya kununua gari la wagonjwa katika Hospitali Teule ya Ipamba. (*Makofi*)

MHE. DKT. WILLIAM AUGUSTAO MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri kuhusu mahitaji ya gari katika hospitali hii lakini nina maswali mawili ya nyongeza au maombi kama ifuatavyo:-

(a)Ni kweli hiyo gari inayozungumzwa kwamba ilihamishwa kutoka kituo cha afya cha Ismani na kupelekwa pale Ipamba ni kweli. Lakini ile gari ni kwa maana ya jina. Mpaka leo hajatumika na imekuwa *condemned* na *is grounded*. Kwa hiyo, ni gari iliyoolekwa ambayo haiwezi kufanyakazi yoyote.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo taarifa iliyoopo. Kutokana na hilo naomba sasa kuomba kwa Mheshimiwa Waziri. Je, yuko tayari sasa kutazama namna yoyote, namna gani ile hospitali inaweza ikapata gari kwa haraka kwa sababu inawajibika kuhudumia vijiji 24 katika tarafa tatu. Dakika hii tunazungumza hawana gari yoyote kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa.

(b) Mheshimiwa Waziri anashauri kwamba Halmashauri izingatie kutenga Bajeti inayotosha kwa ajili ya mahitaji hayo.

Lakini bajeti inayozungumza sasa maana yake ni mwaka 2012/2013 ambako ni mbali na sasa tunakabiliana na matatizo ya kuhudumia wananchi katika afya. Naomba Mheshimiwa Waziri nipaye majibu ya maswali haya.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dkt. William A. Mgimwa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezungumza na Tina Sekambo, ambaye ndio Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Nikamwambia naomba uniombie na huko aliko atajua kwamba sasa namtaja kwamba ninam-quote yeye hii gari anayosema Mheshimiwa Mbunge aina ya Hyundai ni kweli imekuwa na matatizo mengi. Nikamwuliza hivi tunavyozungumza sasa hivi gari hiyo inatembea? Akaniambia gari hii inatembea. Sasa Mbunge yeye anatoka kule sasa mimi nikishindana naye hapa nikasema gari hitembe au inatembea yeye anajua kuliko mimi.

Lakini nataka nikuambie kitu kimoja ni ukweli kwamba gari hili limekuwa *on and off* na nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa William Lukvi ambaye lilipowashinda hili gari wallirudisha mpaka kwa Wakorea wakaenda wakaliangalia kwa sababu tatizo lake kubwa ni suala la *spare parts*.

Likarekebishwa likarudi na Mheshimiwa DED akaniambia kwamba linakwenda vizuri. Lakini ninachowea kusema hapa ni kwamba sisi tutakaa tutazungumza wana wenzao pale nimemwuliza wana shirika linaitwa KUAM amba wanasaidiana nao. Nikamwambia unadhani tukishirikiana na Halmashauri tukasogezza na gari pale tukaona jinsi ya kuwasaidia itasaidia? Akasema inawezekana.

Anachotaka Mbunge hapa na ndio maana ameuliza swali hapa, anataka hapa nimwambie kwamba tutapata gari lingine jipya. Lipi sasa magari yalikuwa ni 43 na yameshagawanywa na tumeelekezwa hapa kabla hatujaondoka tulete orodha. Ndio maana tumeshauri kwamba waingize kwenye bajeti inayokuja. Bajeti inayokuja ni kweli kama anavyosema mwaka 2012/2013 hii imeshapita, kwa hiyo, tutashirikiana naye tutasaidiana naye. (*Makofii*)

Kitu kimoja ambacho nataka nikiri mbele yako pamoja na kwamba umeniambia kwa kifupi ni kwamba ni kweli gari hili lina matatizo tutakaa na *Doctor* tutasaidiana. Kwamba nitamwambia hapa tuna hela mpya tutakupa gari nyininge mpya nitakuwa nasema uongo hapa nitabanwa nikirudi wewe bwana hii habari uliyoahidi ni ipi hiyo unayoizungumza. Kwa hiyo, naomba tushirikiane tusaidiane katika jambo hilo.

MHE. CHIKU A. AMBWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hospitali ya Ipamba ilikuwa ni tegemeo kubwa sana la wakazi wa Mkoa wa Iringa kwa ujumla. Na kwa kuwa kabla Serikali hajiaiteua na kushiriki kuanza kuendesha hospitali ilikuwa inafanya kazi nzuri na wananchi walikuwa wanapata matibabu na malalamiko yalikuwa ni kidogo sana.

Je, Serikali haioni kwamba ni bora hata wawarudishie wenywewe waliokuwa wanamiliki hiyo hospitali kwa sababu walikuwa ni bora zaidi kuliko sasa ilivyo katika Serikali ambayo imetamka wazi kwamba bajeti walijonayo haitoshi na hili tatizo kwa kila kitu kwamba bajeti haitoshi wakati wale walipokuwa wanamiliki hospitali ile ilikuwa ina manufaa makubwa sana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chiku Ambwao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi hospitali ile haiachi kuwa Hospitali ya Shirika la Dini kama ilivyo sasa hivi kwa sababu tunashirikiana nao. Hapa inaitwa Hospitali Teule yaani *Designated Hospital* unasema hivi, kwa sasa nikisema nijenge Hospitali ya Wilaya mpaka ijengwe watu wangu watakuwa wamekufa.

Kwa hiyo, kinachotembea sasa hivi ni kwamba umehamisha heshima zote zinazohusu hospitali ya Wilaya ukazipeleka katika Hospitali hii Ipamba ikapelekwa pale. Hawajanyang'anya umiliki, wenye miliki wa ile Hospitali ni hilo shirika la dini lilioko pale, kwa hiyo ukiondoa sasa yaani ndio unawafanya wale wananchi wateseke. Mambo ya *cost sharing policy* ni utaratibu wa namna ya kupeleka *drugs* na kila kitu kinabaki hivyo hivyo.

Kwa hiyo, mimi ningesema hivi kuna tatizo hapa linalozungumzwa hapa, Mheshimiwa Mbunge gari hili linalosemwa hapa Halmashauri hii ya Wilaya tumewapelekea gari mwaka huu mwezi Aprili tumepeleka gari pale tumepeleka katika Halmashauri hiyo haikwenda pale lakini imekwenda katika Halmashauri hiyo. Wote hawa kuwaruhusu wakisimama hapa kila mmoja atasema nataka gari na hospitali.

Mimi naomba tuwashukuru kwanza wale wenzetu ambao wamekubali kushirikiana na Serikali kwamba tuendeshe utaratibu ule, kwa sababu tukishasema tunawarudishia pale maana tutawarudishia mzigo wote unabaki kwao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Chiku Abwao pamoja na wenzako wote wanaotoka Iringa mimi nadhani utaratibu huu wa kuwa na hospitali Teule ni utaratibu mzuri. (*Makofii*)

Hata kule Mheshimiwa Michal Lekule Laizer, anakozungumza kama unaweza ukapata Hospitali ya Dini iko pale na inaweza ikatoa hizo *services*. Huduma za mama na mtoto zinapatikana pale Serikali inasema tatizo hakuna katika jambo hilo. (*Makofii*)

Kwa hilo, nilikuwa naomba tuliheshimu hilo, tulione hilo na kama kuna haya matatizo madogo madogo yanajitokeza pale sisi kama Serikali tutashirikiana wote kwa pamoja kuona kwamba tunaondoa haya matatizo kuliko sasa kuondoa huu utaratibu mzuri ambao ukimsikiliza Waziri wa Afya anazungumza kila siku hapa tutakuwa tunarudi nyuma. (*Makofii*)

MHE. LOLENSIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali iliahidi katika bajeti ya mwaka 2010/2011 kule gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Chikobe kule jimboni Busanda Wilayani Geita. Lakini mpaka sasa bado hawajatimiza ahadi hii ningependa kujua ni lini sasa wananchi hawa wataweza kupata gari hili kama ahadi ya Serikali ilivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naye anachosema Mheshimiwa Lolensia Bukwimba ni kweli tumekwenda naye amenipeleka mpaka kwenye hospitali zao ni kweli kuna ahadi kwamba tutawasaidia pale.

Tatizo ni hilo ninalolieleza hapa hapa kama lingekuwepo sisi tungepeleka, sisi tunataka afya za watu wetu zihudumiwa, mimi ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, sisi tutakwenda kukaa naye tuone vizuri kwenye orodha ambayo nimesema kwamba tutawaiteeni tuone jinsi ambavyo tunaweza tukafanya. Hakuna mtu ambaye anakataa kusaidia katika hospitali ile kwa sababu ndio wajibu wetu. (*Makofii*)

Na. 86

Kujenga Mahakama Kuu Singida

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Serikali imeahidi mara nyingi hapa Bungeni kuwa itajenga Mahakama Kuu Mkoani Singida:-

Je, utekelezaji wa ahadi hii umefikia wapi?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli mara kadhaa Serikali ilitoa ahadi ya kujenga Mahakama Kuu katika Mkoa wa Singida ikiwa pamoja na Mikoa mingine ambayo haina Mahakama Kuu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ikiruhusu tutajenga Mahakama hizo kwa awamu na katika kila Mkoa. Kwa hiyo, azma yetu ya kujenga Mahakama kila Mkoa ipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka Bunge lako Tukufu lilipitisha Mfuko wa Mahakama na katika Mfuko wa Mahakama kipaombele kimoja wapo ni ujenzi wa Mahakama Kuu. Kwa hiyo, hali ikiwa nzuri, Mfuko wa Mahakama ukienda vizuri nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya hivyo kwa kila Mkoa.

Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kukumbusha mara kwa mara Serikali juu ya ujenzi wa Mahakama Kuu Singida. Hili linadhihirisha jinsi gani Mheshimiwa Mbunge anavyopenda maendeleo katika sekta ya sheria.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba swali hili limekuwa la muda mrefu, nakumbuka Mawaziri watatu nimewahi kuwauliza swali hili na kwa kuwa mara zote wamekuwa na majibu mazuri sana yenye kuwatia moyo wananchi wa Mkoa wa Singida wenye moyo wa kujitolea pale wanapopewa mradi wowote wa maendeleo na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hajaonyesha kabisa kabisa ni lini ahadi hii itatekelezwa.

(a) Je, haoni kwamba anawakatisha tamaa wananchi wa Mkoa wa Singida na kuwafanya wakose imani na Serikali yao?

(b) Kwa kuwa Singida Mjini kuna Mahakama nzuri ya kisasa ya mwanzo ambayo toka imejengwa na kukamilika sasa ni zaidi ya miaka mitatu, lakini Mahakama hiyo hajafunguliwa, ipo tu, majengo mapya yamekuwa nyumba za popo. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuyaacha majengo haya mapya ya kisasa bila kufanya kazi ni kuendelea kuchezea hela za Serikali na kuwanyima haki wananchi wa Singida?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chilolo, kama ifuatavyo:-

Katika swali lake la kwanza, kama nilivyowaeleza Waheshimiwa Wabunge, mmetusaidia sana kupitisha ule Mfuko wa Mahakama na mwaka huu mmepitisha shilingi bilioni 20 katika Mfuko wa Mahakama, lakini tuliona kipaumbele namba moja kwanza kumaliza kesi mbalimbilia ambazo zimejilimbikiza kwa muda mrefu. Sasa kipaumbele namba mbili ni ujenzi wa Mahakama. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipao mbele chetu namba mbili ni ujenzi wa Mahakama na azma yetu ni kujenga Mahakama Kuu kila Mkoa ili kuwarahaishia wananchi kupata huduma zao.

Kwa hiyo, katika bajeti yetu ya mwaka 2012/2013 tutazingatia na kama nilivyosema kwamba tutaenda kwa awamu na vipindi vyote hivyo tulivyo ahidi angalau tumejenga Mahakama Kuu kule Mkoani Kagera na Mahakama Kuu kule Shinyanga ambayo inaendela. Kwa hiyo, tutaendelea kwa awamu ili wananchi wetu waweze kupata huduma za kisheria kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi kwenye bajeti tutalizingatia sana suala la ujenzi wa Mahakama kuanzia za mwanzo mpaka Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa Mahakama ile nafahamu kwamba pale Singida tumejenga Mahakama ya Mwanzo nzuri sana, tatizo tulikuwa hatujaweka *furniture* katika Mhakama ile na kwa mwaka huu kwenye Bajeti tumeweka fedha za kutosha za kununua *furniture* kwa hiyo Mhehsimiwa jengo lile halitaendelea tena kuwa malazi ya popo bali tutaweka *furniture* na Mahakama nyngine ya wenzetu kule Karatu, zote tutaweka *furniture* ili ziweze ku-operate.

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka tu kumwuliza Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Mahakama ya Shinyanga ipo kwenye *process* na lile jengo limekaa muda mrefu sana sasa hivi nimepita nilivyoenda juzi nilikuta wametengeneza uzio. Nilikuwa nataka tu *commitment* ya Serikali. je, hilo jengo watalimaliza lini?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mhehsimiwa Rachel Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Makao Makuu Shinyanga liliikuwa katika *phase* mbili, *phase* ya kwanza tumeshamaliza na katika bajeti ya mwaka huu fedha zimetengwa kwa ajili ya kumaliza jengo hili. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi kwamba mwaka huu tumejwekeea fedha kwa ajili ya kumaliza Mahakama Kuu Shinyanga na ili tuanze Mikoa mingine. (*Makofii*)

Na. 87

Utoaji wa Maoni ya Kuandika Katiba Mpya

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA aliuliza:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya Watanzania wenyewe mazoea ya kusoma na kuielewa Katiba?

(b) Kama ni asilimia chache. Je, idadi hiyo ya watu wachache wanaielewa Katiba ya sasa kwa kiasi gani hata wawe na uhalali wa kufanyia mabadiliko Katiba hiyo na kusema kuwa wanawakilisha matakwa ya Watanzania wote?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna utafiti wowote uliofanyika kuonyesha ni kiasi gani cha Watanzania wanaielewa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo tafiti ambazo zimefanyiwa kazi ni kuhusu watu wenyewe elimu inayowawezesha kusoma na kuandika. Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2002 na 2007 karibu robo tatu ya Watanzania (asilimia 71) walikuwa wanajua kusoma na kuandika.

Kwa maeneo ya Vijijini asilimia 70 wanaojua kusoma na kuandika na ukilinganisha katika Jiji la Dar es Salaam asilimia 92 wanajua kusoma na kuandika na asilimia 87 kwa Miji mingine yote Mikuu.

Pia katika maeneo ya vijijini ni asilimia kubwa ya watu wazima wamesoma elimu ya msingi. Naamini kwamba wananchi hao wote wana uwezo wa kuisoma Katiba na kuwa na uelewa katika upeo tofauti. Kiuhalsia ni asilimia ndogo ya Watanzania ambao wanaielewa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutojua kusoma na kuandika kwa Mtanzania hakumaanishi Mtanzania huyo kukosa haki yake ya kushiriki katika maamuzi au mjadala au uchambuzi wa masuala mbalimbali ya Kitaifa na kutoa maoni yake kuhusu mustakabali wa nchi yetu kwa kuwa hiyo ni haki ya msingi ya kila raia wa Tanzania.

Hivyo basi, kila Mtanzania, bila kujali uelewa wake wa Katiba ya sasa, ana haki ya kushiriki kikamilifu katika kutoa mawazo yake katika mchakato mzima wa kupata Katiba mpya utakaaoanza mara tu baada ya Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 utakaopitishwa na Bunge lako Tukufu. Baada ya hapo, Serikali imejipanga vilivyo kuwaelimisha wananchi kuhusu Katiba iliyopo.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri pamoja na majibu hayo nina swali moja la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Waziri amekiri wazi kwamba hakuna utafiti ambao umefanya kubaini ni idadi ipi ya Watanzania wanaifahamu Katiba. Sasa naomba kuiomba Serikali. Je ina mpango gani kuhakikisha kwamba wakati huu tunapojadili mabadiliko ya Katiba yetu mpya kusambaza *copies* ya Katiba yetu ya sasa iliyoandikwa kwa Kiswahili ili Watanzania hawa wanapotoa maoni yao kwenye Tume ambayo itaundwa na Mheshimiwa Rais baada ya kukamilika kwa mjadala hapa kwamba wanapotoa mawazo yao wafanye rejea ya Katiba ya sasa ili mawazo yao yaweze kuzingatia uhalisia wa Katiba ya sasa? Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Mbunge la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumejipanga vilivyo katika kutoa elimu ya Katiba katika nchi nzima. Sasa hivi tunachofanya ni kwamba tunachapisha Katiba nakala laki mbili (200,000) hizo nakala laki mbili tutazigawanya katika taasisi mbalimbali zilizo za Kiserikali na zisizo za Kiserikali. Kwa hiyo, tutaanza kugawa kutoka Mawizarani, vyuo Vikuu, shule za sekondari mpaka chini yaani kwenye taasisi zote za elimu pamoja na NGO zote bila kuangalia kwamba ni NGO ya aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kazi hii itafanya na Tume, Tume kwa upande wake itachapicha nakala kama milioni 5 hivi kwa ajili ya kuwasambazia wananchi pale watakapokuwa wanatoa elimu wanatanguliza kwanza elimu ya Katiba na Katiba zenyewe ili wananchi waelewe ni nini wanakijadili ambacho hakiko kwenye Katiba au waweke mlinganisho kati ya Katiba iliyopo na hayo mapendeleko ambayo wanataka kuyatoa sasa hivi.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa Watanzania wengi Vijiji hawajui sheria na wengine wanapelekwa Mahakamani kwa kutokujua sheria na kubandikizwa kesi na kufungwa. Je, Serikali itawasaidiaje Watanzania hawa wanaoishi Vijiji angalau nao wajue sheria na Katiba ya nchi?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Msabaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Serikali mpaka sasa hivi inatoa elimu katika vyombo mbalimbali kuhuzu mambo ya sheria. Tuna kitengo maalum katika Wizara yangu ambacho kinashughulikia suala la marekebisho ya sheria. Kwa hiyo, wanapofanya marekebisho wanatoa elimu kwa umma. Kw ahiyo, wananchi kwa njia hiyo wanapata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanganyika Law Society* pia huwa inatoa msaada wa kisheria na kutoa elimu. Lakini sasa hivi kwenye Wizara yangu tumeanzisha kurugenzi maalum ambayo itashughulikia na masuala ya kuwasaidia wananchi kuhusu mambo ya sheria. Kitengo hicho tutakiimarisha ili kiweze kutoa msaada wa kisheria kwa wale wananchi ambao hawawezi kuweka mawakili na wale wanaotaka maelekezo kuhusu njia gani wafanye ili kupata haki zao.

Na. 88

Hitaji la Soko- Mbikarazi

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Wananchi wa kijiji cha Mukarazi Kata ya Mabamba- Kibondo, walioko katika mpaka wa Tanzania na Burundi, wanapata usumbufu mkubwa wa mauzo ya bidhaa zao kutoka *TRA, Customs* na Idara ya Polisi mipakani.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwajengea soko mpakani wananchi hao ili nao wafaidike na fursa za ushirikiano wa Afrika Mashariki?

(b) Je, ni hatua zipi zinafanywa na Serikali za kuwaondolea usumbufu wananchi kutoka Idara hizo za Serikali kwani wananchi wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu bidhaa zinazotakiwa kulipiwa ushuru?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Jimbo la Muhamwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuendeleza masoko ya mipakani Wilayani Kibondo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imefanya majadiliano na Benki ya Rasilimali (*TIB*) ili kufadhili ujenzi wa masoko ya mipakani ambapo katika mpango huu masoko yaliyopewa kipaumbele ni yale ya Mukarazi na Muhanje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, ilipewa jukumu la kuandaa michoro ya ujenzi wa masoko hayo. Tayari michoro imeandalwa na kikao cha Halamshauri (*Council Management Team – CMT*) kimeshapitia michoro hiyo na kutoa mapendekezo ya kuboresha michoro, ambayo tayari imepelekwa kwa mtaalamu wa michoro.

Baada ya kufanya maboresho yaliyopendekezwa katika hatua za ujenzi zitaendelea chini ya ufadhilli wa *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokamilika kwa ujenzi wa masoko ya mipakani kutawakutanisha kwa pamoja wafanyabiashara kutoka Burundi na Tanzania na hivyo kuifanya biashara kati ya nchi hizi mbili jirani kuwa rasmi na kuongeza uwazi na ushindani katika biashara. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ebu tungempa nafasi Mheshimiwa Waziri ajibu swali. Kuna nini? Ebu naomba tumpe kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu swali, watu wanataka kusikiliza majibu ya maswali waliouliza. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu suala la elimu kwa wananchi, Serikali kwa kupitia Halmashauri imeandaa mpango wa mafunzo ili kuelimisha Jumuiya ya Wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuhusu biashara ya mipakani.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya ngu itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo pamoja na Taasisi nyingine kama Mamlaka ya Mapato na Uhamiaji katika kutoa elimu inayohitajika ili wafanyabiashara na wananchi wa maeneo ya mipakani wafaidike na fursa za masoko ya Kikanda hususani Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, yaani *SADC*.

Hii itasaidia kujua taratibu na Sheria zinazohusu ufanyaji biashara mipakani ili kuondoa bugudha zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho. Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi zake imekuwa ikitoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa mipakani kuhusu fursa za masoko urasimishaji wa biashara kwa kuwa na leseni za biashara, elimu ya ujasiriamali, elimu ya vipimo na umuhimu wa wafanyabiashara kuijunga katika vikundi na kusajili majina ya biashara.

Mafunzo hayo yametolewa katika masoko ya Sirari, Shirati, Mutukula, Tunduma na Kasulumu. Elimu hii imesaidia kwa kiwango kikubwa, kwani wananchi wa maeneo hayo wameweza kusajili vikundi vya biashara takribani 81. Jitihada hizi za kuelimisha wafanyabiashara mipakani zitaendelea katika mipaka mingine iliyosalia awamu kwa awamu..

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Benki ya Rasilimali *TIB* imekubali kutoa fedha hizi sasa ni lini Serikali itasimamia ili hizi harakati za michoro na nini iweze kukamilika kwa haraka ili soko hili liweze kuanza kujengwa mapema iwezekanavyo?

(b) Swali la pili ni kuhusu usumbufu ambao wamekuwa wanaupata wananchi wa Kijiji wa Mkarazi na Mabamba kwa sababu vituo hivi vya *Custom, TRA* na Polisi viko katikati ya Vijiji. Sasa tumekuwa tunaomba muda mrefu na nimekuwa nauliza hili kwenye Wizara mbali kwamba kwa nii kituo hiki kisihamishwe kikapelekwa mpakani ili wananchi waache kusumbuliwa ndani ya nchi yao.

Watu wanakaguliwa wameenda kununua chumvi anakaguliwa, ameenda kufanya nini anakaguliwa. Kwa nini kisihamishwe kikawekwa mwisho? Kwa sababu hata soko hili likijengwa bado usumbufu utakuwa upo kwa wananchi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mkosamali na nimjibu maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza ni kweli kama alivyosema benki ya rasilimali *TIB* imekubali ufadhili yani *finacing* ya miradi hii ambayo nimeelezea. Pili hatua ya mwisho iliyokuwa imebaki ni ile ya kawaida, mchakato mzima wa kuwa na michoro na wataalamu umekamilika kuititia Kamati ya Halmashauri ya *CMT* na sisi hivi michoro hii inapokamilishwa kitaalamu basi ujenzi kuititia benki ya *TIB* utaanza mara moja.

(b) *TRA* na *Customs* kwa kuwa na vituo katikati ya Vijiji. Serikali imeona hili suala na sio pale tu, tuna maeneo mengine ambako wananchi wanalazimka ku-searchiwa au kukaguliwa mizigo yao ndani ya vijiji vyao jambo ambalo tunadhani tatalitatuwa kwa kuwa na mpango kabambe wa Serikali wa *one boarder post*.

One stop boarder post ni mpango ambao tumeuanza tayari, tunajenga vituo katika mipaka ambayo imechaguliwa ambako wananchi watakaguliwa upande mmoja tu na kama unatoka nchi ya Tanzania kwenda Zimbabwe au kwenda mpaka mwingine utakaguliwa upande wa Tanzania na utakapokwenda mpaka wa pili, utapita moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nashukuru sana. (*Makofii*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu ya Waziri amejaribu kugusia mpaka wa Tunduma ambao ni mpaka ambao unaunganisha nchi zote za Kusini mwa Afrika na kumekuwa na mkakati wa Serikali wa kujenga kituo cha kibashara cha kimataifa ama soko kuu la kimataifa. Je, tungependa kufahamu kauli ya Serikali ni lini ujenzi huo utaanza?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mpango wa kujenga soko la kimaifa Tunduma na mpango huu umeanza katika hatua za awali kama tunavyotumia utaratibu wa Halmashauri, Utaratibu wa uwepo kwa mchakato ambao tayari umeshaanza na tunaeendelea na utaratibu wa kutafuta fedha na fedha zitakapopatikana tunapenda kumwaahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba soko hilo litajengwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nilisema wale waliosimama mwanzo niliowaona. Sasa waliohamasika baadaye tena ninaomba niendelee na swali na linalofuata. Tunaendelea na swali linalofuata. Litalizwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mbeya. Mheshimiwa Cynthia uliza swali lako.

Na. 89

Kutoa Leseni ya Kuuza Sukari Kutoka Malawi

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Mkoa wa Mbeya wamekuwa wakitumia Sukari kutoka Malawi inayoingizwa nchini kwa njia za magendo.

Je, Serikali itaruhusu wafanyabiashara kutoka Mbeya kupata leseni za kuuza Sukari kutoka Malawi kihalali?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Sukari nchini uliana kujitokeza tangu mwishoni mwa mwaka 2010. Aidha, kwa kawaida viwanda vya Sukari hufungwa kati ya mwezi Machi na mwezi Mei kila mwaka kwa ajili ya kufanya ukarabati wa viwanda hivyo. Hata hivyo, upungufu huo hujitokeza zaidi kutokana na Sukari kuuzwa nje ya nchi kwa njia zisizo rasmi au kwa maneno mengine kwa njia za magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba maeneo ya mipakani kama vile Mikoa ya Mbeya, Mtwara na Ruvuma hupata Sukari kutoka nchi jirani inayoingizwa na wafanyabiashara kuititia njia zisizo rasmi. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Bodi ya Sukari ilikwishatoa taarifa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ya mipakani, ukiwemo Mikoa wa Mbeya, kuwasilisha kwao majina ya makampuni yatakayoingizwa katika utaratibu wa kununua Sukari kutoka nchi jirani ili kukidhi mahitaji na kudhibiti uingizaji wa Sukari kwa njia zisizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa Sukari kutoka nje hufanyika tu inapobainika kuwepo upungufu wa Sukari nchini. Katika mwaka 2011/2012 Serikali imeruhusu wafanyabiashara kuingiza Sukari kiasi cha tani 120,000 kutokana na uhaba wa Sukari ambao umejitokeza.

Bodi ya Sukari kuititia Makatibu Tawala wa Mikoa ilitoa tangazo tarehe 12 Septemba, 2011 kuwataarifu wafanyabiashara wote nchini wenye uwezo wa kuagiza Sukari kutoka nje kuomba vibali vya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inampongeza Mheshimiwa Ngoye za kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanapata bidhaa ya sukari kwa bei nzuri na tunawashauri wafanya biashara wote wa Mikoa wa Mbeya na mikoa mingine wawasilishé majina yao kwenye Bodi ya Sukari kwa kuititia Sekretarieti ya Mikoa ili wapatiwe vibali vya kuagiza sukari kutoka nchi jirani.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru sana na ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na amefafanua vizuri. Hata hivyo nina maswali madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kurekebisha hali ya matatizo ya sukari hapa nchini.

Lakini bado suala la sukari mpaka hivi tunavyozungumza ni tete. Bei ya sukari ni kubwa kwa wananchi. Je, kwa hivi sasa mpaka tunavyozungumza Serikali inaendelea kufanya hatua gani ili kurekebisha hatua hiyo? (*Makof!*)

Swali la pili, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna wafanya biashara ambao wanaendelea kupeleka sukari nje kwa njia zisizo rasmi na ninajua kwamba kuna hatua ambazo zimeendelea kufanyika. Ni hatua gari ambazo zimechukuliwa dhidi ya hawa wafanya biashara ambao wanaendelea kupeleka sukari nje wakati Watanzania wakipata matatizo hapa nchini? (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, baada ya mwezi wa nne, mwezi wa tano na wa sita, ukarabati unapokuwa unafanyika katika viwanda vyetu vya sukari nchini katika hali ya kawaida

kunakuwa na upungufu wa sukari na mwaka huu tangu mwaka wa fedha ulipoanza 2011/2012 tayari Serikali imeliona hilo na kuagiza kuingizwa nchini tani laki moja na elfu ishirini ambazo tayari zinaendelea kuingizwa na ili kuondoa tatizo lillolokuiwepo la kampuni au kampuni mbili au tatu kuingiza sukari yote na wao kuwa na *monopoly* katika kuigawa na kusambaza nchini Serikali ililagiza kwamba kila kampuni ipewe mwisho tani 5,000. Hili zoezi linaendelea na tunao wasambazaji wengi sana nchini amba wanaendelea kuingiza sukari na sukari hiyo inaendelea kusambazwa.

Pili, kutokana na ukweli kwamba kuna watu nchi hii amba ni walangazi, wanalandua sukari ya Tanzania wanaipeleka nchi za jirani. Wanaipeleka kwa njia za punda, kwa njia za bajaji, njia za magari, njia za baharini na njia zote ambazo Serikali imezitafuta na kuzigundua, Serikali kwa kupitia tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu ilipiga marufuku kabisa kupeleka sukari nje ya nchi.

Kwa nini tunafanya hivi, kwa sababu sukari ambayo tunaiagiza ije nchini inakuwa hajjalipiwa ushuru. Kitendo cha kuilangua tena iende nchi za jirani ambako na wao wangeweza kuagiza ya kwao ni kitendo cha kuikosisha Serikali mapato na tunasema na tunasema na narudia.

"Mfanya biashara yoyote nchini atakayekamatwa na kujihusisha na kupeleka sukari nje ya nchi, jambo la kwanza tutamkamata na kumpeleka katika vyombo vya Sheria na Serikali imeandaa hatua za ziada za kufanya kuhakikisha kwamba hilo jambo linakomeshwa kabisa kabisa".

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swalii moja la nyongeza. Kufanya biashara ni haki ya Mtanzania yoyote yule iwe ni kampuni au hata wamachinga. Upande huo wa mpaka wetu wa Malawi na Tanzania wanaofanya biashara ya sukari na biashara zingine ni hawa wafanya biashara wadogo wadogo. Kwa nini iwe ni makampuni tu yaruhusiwe kufanya biashara na si hawa wafanya biashara wadogo wadogo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa *Captain* John Komba, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi. Tupate nafasi ya kuendelea na maswali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba wafanya biashara na wajasiriamali wadogo wadogo kama vile walivyo wafanya biashara wakubwa wana haki ya kufanya biashara zote ikiwa ni pamoja na biashara ya Serikali. Kwa sababu ya umuhimu wa kudhibiti biashara ya sukari Serikali imesitiza kwamba wafanya biashara wadogo wadogo wanaweza wakati wowote wakajunga katika vikundi ili wawe na ukubwa na nguvu inayostahili kuweza kupata leseni na vibali vya kuingiza sukari kama wenzao wakubwa.

Na. 90

Tatizo la Tembo Wanaovamia Mashamba na Makazi ya Watu Bukoba Vijiji

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Kumekuwepo na matukio ya tembo kuvamia mashamba na makazi ya watu katika Kata za Kyamulaila, Ruhunga, Mugajwaje na Kibirizi na kwamba kila wananchi wanapofuatilia utatuzi wa tatizo hilo wanaambiwa hatua za kuwatimua tembo hao zitachukuliwa:-

Je, Serikali inachukua hatua zipi kutatua tatizo hilo na kulikomesha kabisa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa maeneo mengi nchini yanakabiliwa na ongezeko la matukio ya wanyamapori waharibifu hususan tembo kuvamia

mashamba ya wananchi na kuharibu mazao na mali zingine. Wilaya ya Bukoba Vijijini hususan Kata za Kyamulaile, Ruhunga, Mugajwale na Kibirizi nayo imeathirika.

Miongoni mwa sababu zinazopelekea kuongezeka kwa matukio haya ni pamoja na kuzibwa kwa mapitio ya wanyama kufuata uanzishwaji wa mashamba ya mifugo (*ranch*) kama vile ranchi ya Mabale, Kitengule, Kikurura na Kagoma.

Aidha, kumetokea uharibifu mkubwa wa mazingira katika mashamba hayo kufuatia wawekezaji kuruhusu wananchi kukata miti kwa ajili ya mkaa na mbao. Vile vile viro vijiji ndani ya maeneo ya *ranch* hivyo kusababisha kupungua kwa maeneo yaliyokuwa yakinutumiwa na tembo na kuongeza migongano baina ya wanyama hao na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonesha wananchi 40 waliharibiwa mazao yao mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahindi, migomba, mihogo, magimbi na viazi vitamu katika mashamba yenye jumla ya ekari 38.25 sambamba na matukio ya wananchi wanne (4) kuuawa na ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili Wilaya ya Bukoba Vijijini, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Moja, kuwatumia askari wanyamapori wa vituo vya Ibanda/Rumanyika, *KDU* – Kanda ya Ziwa pamoja na mapori ya Burigi/Biharamulo na Kimisi kufukuza tembo wanaovamia mashamba. Kuanzia tarehe 7 Novemba, 2011 askari watatu kutoka pori la akiba Burigi wamekuwa wakishirikiana na askari wa Halmashauri kuwafukuza ndovu waliovamia mashmaba ya wananchi na kuendelea kuweka ulinzi kuzuia wanyama hawa wasirudi mashambani.

Pili, kuweka watumishi na gari katika kituo cha kudhibiti wanyama waharibifu cha Kabale – Karagwe ambacho kinatoa huduma katika Wilaya zinazopata madhara Mkoani Kagera na

Tatu, Serikali inaendelea kutambua na kuhifadhi shoroba/mapito ya wanyamapori hususan ndovu pamoja na kuendeleza tafiti za namna ya kudhibiti uharibifu unaotokana na wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na ushirikishwaji wa wananchi na viongozi katika Kata nilizozitaja hususan matumizi ya njia mbadala ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa katika kuzuia uharibifu. Njia hizo ni pamoja na matumizi ya uzio wa kamba ulipakiwa mchanganyiko wa pilipili na *oil* chafu, kuzunguka mashamba pamoja na matumizi ya vitovali vyenye mchanganyiko wa kinyesi cha tembo na pilipili ambavyo vikichomwa harufu yake huwafukuza tembo.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu ambayo kidogo yanatia moyo lakini niombe kumwuliza kwamba kwa vile tembo hawa wamekuwa wasumbu kwa muda mrefu sana na kila tukiuliza majibu ni hayo hayo ambayo yameonekana leo. Ni lini wataruhusu wananchi kuua tembo hawa na kuwala? (*Kicheko*)

Kama sheria hairuhusu ni lini Waziri ataupeleka Muswada wa kuomba sheria hii irekebishwe ili wananchi waruhusiwe kuwaua? Swali la pili, kwa hawa wananchi anaowasema 40 ambaao walioathiriwa na wanyama ni msaada gani ambaao wananchi walipewa wa kama chakula au fidia na kwa hao wanne waliouawa ni fidia ipi ambayo illipwa kwa ndugu wa marehemu? Asante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pole sana kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wengine wengi sana nchini ambaao wamekuwa wakiathirika kwa kuharibiwa mali zao na wakati mwingine maisha.

Tatizo kubwa tulilonalo ni kwamba si uwepo na kutokuwepo kwa tembo au ndovu kama wengine wanavyoita. Tatizo kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ni ongezeko la shughuli za binadamu ambalo limesababisha pia wakati mwingine mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa mfano kwa ukanda wa Kaskazini Magharibi mwa nchi yetu kuna ongezeko kubwa sana la mifugo. Kwa mfano, mifugo mingine inatoka nchi jirani ambayo inafanya maeneo ambayo yamekuwa ni makazi ya wanyama hawa yawe *distubed* na hivyo kuwafanya waweze kutoka nje ya eneo lao la asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu mimi ni kwamba tukiendeleza jitihada za kupunguza au kudhibiti uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa uharibifu au wanyama hawa hawatakuwa na gharama kubwa.

Miaka ya nyuma miaka ya 80 tulikuwa na tembo waliofikia laki moja na elfu arobaini na sita. Hivi sasa tulionao ni kama laki moja na elfu kumi tu. Ni wachache sana. Miaka hiyo ya 1986 tukiwa na tembo au ndovu 146,000 hatukuwa na matukio ya namna hii.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba hata tukiwaua, labda tuwaue tuwamalize kabisa jambo ambalo halitatu tatizo. Kwa hiyo, niombe tu kwamba tuendelee kushirikiana kufanya jitihada za kudhibiti uharibifu wa mazingira. Lakini vile pale inapotokea tatizo kama vile ambavyo tumekuwa tukifanya tuendelee kusaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu suala la pili la msaada unaotolewa, kupitia Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 ya Wanyamapori na Kanuni zake tumepitisha utaratibu wa kutoa kifuta machozi. Juzi nilikuwa Rombo na Siha nikawaambia wananchi ya kwamba Serikali imedhamiria kwamba kila kunapotokea tatizo kwa kadiri inavyowezekana tutakuwa tukilipa kifuta machozi kama ni binadamu kauawa na tutakuwa tunalipa kifuta jasho kama ni mazao yameharibiwa.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine pale ambapo mazao yao yameharibiwa watuletee taarifa na tumekwisha kuji-*commit* kwamba tukiipata taarifa *within one month* tutakuwa tumelipa labda kuwepo utata wa kwamba taarifa zilizoletwa ziwe na matatizo au ziwe na namna fulani la kugushi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba hawa wananchi waliouawa Serikali italipa kifuta machozi shilingi milioni moja kwa kila mwananchi na kwa mazao yaliyoharibiwa totalipa kifuta jasho.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Tatizo la tembo waharibifu wa mazao ambalo lipo Bukoba Vijiji vile pale lipi katika Jimbo langu la Singida Mashariki na tembo wameharibu sana mazao kwenye Kata za Kikio, Isuna na Mang'oli.

Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri ni kiasi gani cha fedha ambazo Serikali imezitenga kwa ajili ya kifuta machozi na kifuta jasho kama ambavyo Sheria ya Wanyamapori inataka. Aidha ni fedha kiasi gani zimepelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kama zipo? Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kwamba tatizo hili linapotokea tutakuwa tukilipa. Kwa mwaka huu wa fedha, fedha tulizotenga kwa ajili ya *ku-deal problem animals* ni kama milioni 300 hivi.

Lakini fedha hizi hazipelekwi kwenye Halmashauri kama mgao. Tunazitoa baada ya tukio kuwa limetokea, tumeletewa taarifa, uhakiki umefanyika, ndiyo tunalipa. Ndiyo maana kwa maeneo ambayo uhakiki umefanyika na umekamilika kama maeneo ya Rombo, Siha na hata Bunda tumekuwa tukipeleka moja kwa moja. Maana yake sasa hivi kwa maeneo tuliyoyataja ya Misuna na zile Kata zingine niombe tu kwamba uwasiliane na wale wananchi pamoja na Halmashauri husika, kwa maana ya Mkurugenzi ili watuletee taarifa hizo tuweze kuwalipa mara moja.

Ahadi ya Uvunaji wa Mamba Mto Ruvuma na Uchimbaji wa Visima katika Kata za Mnavira na Chikolopola

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Wizara ya Maliasili na Utalii iliahidi kuvuna mamba katika mto Ruvuma ikiwa ni pamoja na kuchangia katika uchimbaji wa visima vya maji na vituo vya afya katika Kata za Mnavira na Chikolopola:-

(a)Je, ni lini Serikali itapeleka wavunaji hao ili kupunguza mamba hao amba huleta madhara makubwa kwa wananchi?

(b)Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya kuchangia uchimbaji wa visima na ujenzi wa vituo vya afya itatekelezwa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali kupitia Wizara yangu, tena mimi mwenyewe, iliahidi kushughulikia tatizo la mamba hatari kwa kupeleka wavunaji ili kuondoa madhara makubwa yanayowapata Wananchi. Zoezi la kuhesabu mamba ili kubaini idadi ya mamba waliopo katika eneo hilo kupitia Taasisi ya Wanyamapori Tanzania, lilikamilika mwezi Mei na Juni mwaka huu. Matokeo ya sensa hiyo, yanaonesha kuwepo ongezeko la idadi ya mamba katika maeneo hayo. Kutokana na matokeo hayo, Wizara yangu imeteua makampuni matatu yenye mashamba ya ufugaji wa mamba, kufanya uvunaji wa mamba hao katika Kata za Mnavira na Chikolopola. Vibali kwa ajili ya kazi hiyo vimekwishatolewa na tunategemea kazi hiyo itaanza kufanyika mwezi huu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza tatizo la wanyama hatari na waharibifu wakiwemo mamba, nilipokuwa ziarani Mkoani Mtwara, Wizara yangu iliahidi kuchangia shilingi millioni 47 ili kusaidla shughuli za uchimbaji visima ili Wananchi wasiende mtoni kutafuta maji na ujenzi wa Vituo vya Afya ili wawe wanapata huduma mapema pale wanapopata matafito kama yaitokea katika Wilaya tatu za Nanyumbu, Lulindi na Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upatikanaji wa fedha unategemea makusanyo, Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha malipo ya fedha hizo na zitakuwa zikilipwa kwa awamu. Tutaanza mwezi huu wa 11 kupeleka shilingi millioni kumi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, kwa makusudio hayo kama niliyoeleza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Pili, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Wananchi wa Jimbo la Lulindi kwa sasa wanakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji na upungufu wa chakula na hivyo kusababisha Wananchi wengi sana kwenda kwenye mto huu kwa ajili ya kupata mahitaji ya maji. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatutajia Makampuni hayo matatu ambayo Wizara yake imekwishayateua kwenda kufanya kazi hiyo?

(ii) Mheshimiwa Waziri ameahidi kwamba ataanza kupeleka shilingi millioni kumi kwa ajili ya kutekeleza ahadi ambazo ameziweka. Je, anaweza akamweleza Mkurugenzi kwamba kwa sasa fedha hizi zimelenga kwenye ahadi ipi?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Bwanausi pamoja na Wananchi wa Lulindi, kwa mapokezi ya kipekee ambayo niliyapata nilipokwenda kule. Niseme tu kwamba, Wizara yangu kama nilivyosema, imekwishateua Makampuni matatu kwa ajili ya kufanya uvunaji huo. Makampuni hyayo ni pamoja na Kampuni ya *Muze Crocodile Ranch* ya Sumbawanga, *Kosam Crocodile Farm* ya Sumbawanga pamoja na *Kaole Crocodile Farm* ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa maelekezo fedha hizo ziweze kutumika kwa shughuli hiyo katika utaratibu wa kupeleka fedha hizo, tumeshafanya hivyo; tumemwelekeza Mkurugenzi kwamba, fedha hizi ni kwa ajili ya Wananchi wa Lulindi kwenye ahadi ambayo niliitoa nilipokuwa kule. Nimwombe tu Mbunge mwenzangu afuatilie ili kuhakikisha kwamba, fedha hizo zinatumika kama tulivyokuwa tumeahidi.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ziwa Rukwa lila mamba wengi sana na inasemekana kuwa ni Ziwa la kwanza kuwa na mamba duniani. Mamba hao wamekuwa wakiwadhuru wavuvi, wanawakamata akina mama wanaokwenda kuchota maji na watoto wanaokwenda kuoga na wakati mwingine wanasambaa kwenye mito mikubwa kama ya Momba na Nzovwe, wanawavizia akina mama wanapokwenda kuchota maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapunguza mamba hao ikiwa ni pamoja na kutoa fidia kwa wale waliojeruhiwa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuititia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapor (TAWIRI), inaendelea na sensa pana zaidi, baada ya kukamilisha sensa kwenye maeneo ambayo yalikuwa ni *spot areas* kama Mto Ruvuma kwa ajili ya kubaini idadi ya mamba kwa nchi nzima. Niseme tu kwamba, kwa *trend* ambayo imekuwepo kwa miaka mitatu toka 2008, imekuwa ikionesha tofauti na mazingira yalivyo. Mwaka 2008/2009, tulitoa vibali kwa makampuni 28 ili yaweze kuvuna mamba. Kati ya hayo, makampuni 28 yalirudisha vibali vile kwamba, yamekosa mamba na kuomba yabadilishiwe maeneo mengine; kumaanisha kwamba idadi ya mamba imepungua na hawapatikani. Matukio ya Wananchi kuuawa au kujeruhiwa yanaongezeka. Kwa hiyo, tumeamua kufanya utafiti wa kina zaidi kujaribu kuangalia tatizo hasa lipo kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyouliza kuhusu suala la kifuta machozi au kifuta jasho, lakini kwa kesi hii ni kifuta machozi zaidi; ni kwamba, Serikali itakuwa ikilipa na tutakuwa tukifanya hivyo. Cha muhimu, atuletee taarifa kama nilivyokwishakusema wakati ninajibu swalii la Mbunge wa Bukoba Vijijini.

Na. 92

Matokeo ya Uchunguzi wa Samaki Wenye Mionzi ya Nyuklia Kutoka Japani

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Katika Bunge la Kumi, Mkutano wa Nne, Serikali ilitoa taarifa kwa umma juu ya kuingizwa nchini kwa samaki waliohisiwa kuwa na mionzi ya nyuklia kutoka Japani na kuahidi kufanya uchunguzi juu ya suala hilo ili kutoa taarifa ya kina:-

Je, nini matokeo ya uchunguzi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa tarehe 27 Julai, 2011 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, ilitoa taarifa kwa umma kuhusu kuingizwa nchini kwa samaki aina ya vibua (*mackerel*), waliodhaniwa kuwa na mionzi ya nyuklia kutoka Japani. Samaki walioingizwa na Kampuni ya *Alphakrust Ltd* ya Jijini Dar-es-Salaam. Vile vile katika taarifa yake, Serikali iliahidi kufanya uchunguzi wa suala hilo ili kutoa taarifa ya kina kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi zinazohusika na Usalama na Ubora wa Chakula Nchini, ambazo ni Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Mamlaka ya Chakula na Dawa na Kamisheni ya Nguvu za Atomiki Tanzania, zimefanya uchunguzi kuhusu kuingizwa nchini samaki hao na matokeo ya uchunguzi ni kama ifuatavyo:-

- (a) Uhakiki wa uhalali wa nyaraka mbalimbali zilizohusika na samaki hawa kuingizwa nchini. Hii ilibainika kwamba, nyaraka zote ziliikuwa ni halali na taratibu zote za uingizwaji samaki nchini zilizingatiwa.
- (b) Uchunguzi uliofanywa ndani ya nchi katika Maabara ya Kamisheni ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*) na kuwasilishwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tarehe 29 Julai, 2011, kwa barua yenyewe Kumb. Na. *TAEC/CON/ENV/04/01/1*, ulionesha kwamba, samaki hao hawakuwa wamechafuliwa na mionzi ya nyuklia na hivyo walikuwa salama kwa matumizi ya binadamu.
- (c) Ili kujiridhisha zaidi, mnamo tarehe 22 Agosti, 2011, Serikali kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*), ilichukua sampuli nyingine na kuzipeleka katika Maabara ya *NECSA* iliyoko Afrika Kusini, ambayo ina ithibati namba *ISO 17025:2005* kwa ajili ya uchunguzi wa mionzi ya nyuklia. Matokeo ya uchunguzi huo pia yalionesha kuwa samaki hao hawakuwa wamechafuliwa na mionzi ya nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi huo wa kimaabara, ulizingatia Viwango vya Kimataifa vinavyotolewa na Taasisi ya Kimataifa inayohusika na kuandaa viwango vya vyakula (*Codex Alimentarius Commission*), iliyopo chini ya Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9 Septemba, 2011 Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilitoa tamko rasmi kuufahamisha umma kupitia vyombo vya habari kuwa, samaki hao ni salama kwa matumizi ya binadamu. Kampuni ya *Alphakrust Ltd*. ilipewa ruhusa na *TFDA* kwa barua Na. *BA.137/298/225/14* ya tarehe 9 Septemba, 2011 ili kuwauza samaki hao.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa taarifa hiyo ya tarehe 27 ilitolewa katika Bunge hili; kwa nini baadhi ya uchunguzi wa kina mliouahidi katika Bunge hili haukuletwa hapa Bungeni na badala yake umetolewa katika vyombo vya habari?

(ii) Inaonesha kwamba uchunguzi huu wa kina ambaa umeelezwa katika majibu ya Waziri umefanywa kwa samaki tu. Je, mmejiridhishaje kwamba Wananchi wetu wa Tanzania waliokula samaki hawa hawakupata madhara?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya unyeti wa suala zima na haraka iliyohitajika kuupa taarifa Umma wa Tanzania, ilibidi taarifa hiyo itolewe kwa sababu kulikuwa na zaidi ya kipindi cha mwezi mzima kabla Bunge lako Tukufu halijakutana tena. Kwa hiyo, kulikuwa na haja ya kutoa taarifa hiyo kwenye Vyombo vya Umma, lakini pia Kiwizara tulikuwa tayari tumejipanga ili Serikali iweze kuja kutoa taarifa hii pia Bungeni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka kwamba, katika taarifa iliyotolewa tarehe 27 Julai, 2011 samaki hao wengi walizuiwa. Kuna kilo kama 800 ambazo hazikuweza kurudishwa, lakini samaki wengine kilo 123,908 walibakizwa na kuhifadhiwa chini ya ulinzi wa vyombo vyetu vya usalama na hivyo hawakutumika. Maadam ilishagundulika kwamba, samaki hao hawakuwa na madhara, *logic* yake ni kwamba, wanadamu waliotumia zile kilo 800 basi na wao hawakuwa na sababu ya kuwa na hofu maana hawakuwa na madhara.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona. Je, kwa nini Serikali inaaagiza samaki kutoka nje ya nchi pamoja na kwamba tuna samaki wengi katika maziwa, katika bahari yetu na katika baadhi ya mito iliyoko katika Nchi ya Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna mito mingi, maziwa pamoja na mabwawa, lakini nyenzo zetu za kuvua bado hazitoshelezi kuweza kuvua samaki wanaotutosheleza nchini; kwa hiyo, bado kuna makampuni mengi kama hii ya *Alfakrust*, ambayo kwa kipindi kirefu sasa imekuwa ikiagiza samaki kutoka nje; Yemen, India na Japan, ili kuweza kujazia tofauti inayotokana na kutoweza kuvuna kiasi kinachotakiwa nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna minong'ono imejitokeza hapa inaonekana suala hilo inabidi kulifanyia kazi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tunaendelea na swali linalofuata, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa.

Na. 93

Fidia Kutokana na Ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Serikali imekwishaanza ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma kwa kiwango cha lami:-

Je, imezingatia kwa kiasi gani haki ya Wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara hiyo kulipwa fidia ya mali zao?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imekwishaanza ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa Barabara hii yenye jumla ya urefu wa kilometra 260, utagharimu jumla ya shilingi bilioni 230 na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Shirika la Misaada la Kimataifa la Japoni (*JAICA*) na Serikali ya Tanzania (*GOT*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu; sehemu ya kwanza ni ya Iringa – Migori, yenye jumla ya kilometra 95.2 ambao unatekelezwa na Kampuni ya *SIECO* kwa gharama ya shilingi bilioni 84.22 kwa muda wa miezi 35. Sehemu ya pili ni Migori – Fufwe Escapement yenye jumla ya kilometra 93.2 ambayo inatekelezwa na Kampuni ya *SIECO* kwa gharama ya shilingi bilioni 73.6 kwa miezi 35. Sehemu ya tatu ni Fufwe Escapement hadi

Dodoma, yenye jumla ya kilometra 70.9 ambayo inatekelezwa na Kampuni ya *China Communication Construction Company* kwa gharama ya shilingi bilioni 64.33 kwa kipindi cha miezi 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kazi hizi ni kwamba, katika *package* zote tatu, wakandarasi wamekamilisha *mobilization* pamoja na ujenzi wa kambi zao na sasa wanaendelea na kazi ya kusafisha barabara na ujenzi wa Kambi za Wahandisi Waelekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Sheria ya Barabara, *Cap. 167* ya Mwaka 1967 na Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007, watu wote wanaostahili kulipwa fidia ya mali zao zitakazoathirika na ujenzi huu, watalipwa fidia na ambao hawastahili kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria, hawatalipwa. Hadi sasa kwa upande wa Mkoa wa Iringa watu 181 wanaostahili kulipwa fidia wamekwishalipwa, ambapo jumla ya shilingi milioni 355.02 zimetumika. Kwa upande wa Mkoa wa Dodoma, jumla ya watu 306 wamekwishalipwa jumla ya shilingi milioni 414.13 na wiki moja iliyopita tumelipa milioni 933 kwa Wananchi watakaoguswa katika eneo la *diversion* hapa Dodoma.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, ninamshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri na ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa hiyo Barabara ya Dodoma – Iringa. Nina maswali mawili tu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Sheria hizi ni za hivi karibuni; na kwa kuwa kuna Wananchi wengine wameshaendeleza maeneo yao kabla ya Sheria hizo; kwa mfano, Msikiti wa Izazi; Serikali ina mpango gani wa kurudi na kuangalia upya kuona kama kuna wanaopata haki zao na kuna wengine ambao wamefidiwa hawakufidiwa kihalali?

(ii) Tumeshuhudia kuna baadhi ya maeneo yamejengwa kandokando ya barabara na majengo hayo ni kama *Petrol Stations* na wamiliki wamepata hati za kumiliki na vibali vya ujenzi wa hizo *petrol stations* na majengo yao yamebomolewa bila kupewa fidia. Serikali inasema nini kwa sababu kuna baadhi ya watendaji wamewapa hivyo vibali na hizo hati na hapohapo Wananchi hao hawapewi fidia; je, hao waliotoa hivyo vibali na hizo hati wanachukuliwa hatua gani na Serikali kwa sababu ni kama uonevu kwa Mwananchi? (*Makof*)

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, hii Sheria siyo ya hivi karibuni: Sheria hii ya Hifadhi ya Barabara imeanza mwaka 1932, ikafanyiwa *amendment* mwaka 1939, 1942, 1959, 1967 kuitia *Cap. 167*, 1969, 1992, 1993 na imefanyiwa *amendment* pia kuitia Sheria Namba 13 ya Mwaka 2007. Pia imetolewa kwenye *Government Notice Number 471* ya mwaka 1962; kwa hiyo, hii Sheria imekuwepo tangu mwaka 1932.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuitia Sheria Namba Nne na Namba Tano ambazo ni Sheria za Ardhi za Mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Namba Sita ya Mwaka 2007 na Sheria Namba Nane ya Mwaka 2007 ya Mipango Miji, inatambua hifadhi ya barabara.

Kuitia Ibara ya Katiba, kifungu namba 26(1) na (2) kinasema kila Mtanzania ana wajibu wa kuheshimu Katiba na kuheshimu Sheria. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba wale waliofuatwa na barabara na wale ambao wapo nje ya hifadhi ya barabara, wanalipwa fidia. Wale ambao wapo ndani ya hifadhi ya barabara, hakuna cha fidia na ndiyo maana nimeeleza katika jibu langu la msingi kwa wale waliofuatwa na barabara kwenye hii *deviation* ya kilomita kumi hapa Dodoma tumelipa shilingi milioni 633 na wametoa *notice* ya miezi mitatu ili watu waweze kupisha na wamelpwa fedha mpaka za kuhamisha pamoja na za kupangisha katika kipindi cha miezi mitatu. Wale waliogawa maeneo wawe ni Watumishi wa Serikali, kwa vile wamevunja Sheria,

wana haki ya kushtakiwa, lakini Wananchi waliojenga nao, *ignorance of law is not a defense.* (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, hatuna muda, ninaomba tuendelee na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini.

Na. 94

Barabara ya Nyololo - Mgololo

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Barabara ya Nyololo - Igowole - Kibao - Mtango - Mgololo ni muhimu sana katika kukuza Uchumi wa Tanzania kwa ujumla na imepita katika viwanda vikubwa vile *Uniliver Tea Company, Mufindi Tea Company* na Kiwanda cha Karatasi Mgololo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami badala ya kuendelea kutumia gharama kubwa za kuikarabati kila mwaka?

(b) Je, kwa nini Serikali inashindwa kufanya maamuzi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kujenga Barabara ya Nyololo - Igowole - Kibao - Mtango - Mgololo kwa kiwango cha lami na hivyo imepanga kuanza kufanyia upembusi yakinifu katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Katika sehemu ya (b), Serikali haiashindwa kufanya maamuzi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Uamuzi wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, utategemea matokeo yatakayotokana na upembusi yakinifu au *feasibility study, detail design, pamoja na upatikanaji wa fedha.*

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri.

(i) Bahati nzuri sana miaka iliyopita walishafanya upembusi lakini kufuatana na mabadiliko ya kiuchumi, ninaishukuru sana Serikali sasa hivi imeshachukua hatua kufanya upembusi upya. Mategemeo ni kupata majibu mazuri ya upembusi. Je, majibu yakiwa mazuri Serikali itaanza lini kujenga hiyo barabara?

(ii) Kwa kuwa Barabara ya Nyololo inakatisha pale Mji Mdogo wa Nyololo; na kwa kuwa sasa hivi pale Nyololo hakuna stendi ya mabasi na tukizingatia kwamba mabasi makubwa yanayokwenda Songea, Mbeya na Zambia yanapita pale na pia kuna magari makubwa. Je, Serikali inachukua hatua gani kujenga stendi pale Nyololo ili watu waweze kusalimisha maisha yao?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninapenda nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kushughulikia maendeleo na hasa hususan barabara katika Jimbo lake na Mkoa wa Iringa kwa ujumla. Katika jibu la msingi, nimeeleza kwamba, upembusi

yakinifu na *detail design* zinaweza kuanza kufanyika kwenye mwaka 2012/2013; yale yote aliyoyaomba Mheshimiwa Mbunge yatazingatiwa katika kazi hii ya upembuzi yakinifu na *detail design* katika eneo hili.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina swali dogo tu kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa kazi ya ujenzi wa barabara ni ya gharama kubwa; na kwa kuwa barabara zinapokosa *routine maintenance* zinaharibika na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali:-

Je, Waziri atatueleza nini kuhusu hali ya barabara inayotoka Tanga – Moshi - Arusha, hasa upande wa Mkoa wa Tanga kati ya *junction* inayokwenda Tanga na Segera, kuanzia Segera mpaka wa Kilimanjaro kwa sababu barabara hii ina hali mbaya; ina mashimo mengi; inaharibika kwa kasi; hatuoni mkakati wowote wa *maintainance*?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Mbewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hatua zote ambazo amezizungumza Mheshimiwa Freeman Mbewe na ndiyo maana kupitia *Amendment Act*, Namba Mbili ya Mwaka 1998, ilianzisha Mfuko wa Barabara, ambapo katika bajeti ya mwaka huu zaidi ya shilingi bilioni 300 zitakusanya kwa ajili ya kufanya *sport improvement* na *routine maintainance*.

Kuhusu barabara aliyozungumzia ya kutoka Segera mpaka Moshi, ile barabara ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu, zimetengwa fedha karibu shilingi bilioni 28 ambazo ni chini ya ufadhili wa *World Bank*, ambao wakishamaliza *detail design*, wataanza kufanya ukarabati upya ili barabara hii iweze kupitika katika majira yote ikiwa ni pamoja na kuipanua, kwa sababu tunatambua umuhimu wa barabara hii katika uchumi wa nchi yetu.

Na. 95

Takwimu za Mpango wa Watanzania Wanaofanya Kazi Nje

MHE. VICK P. KAMATA aliluliza:-

Maendeleo ya nchi yanatokana na juhudni na mchango wa Wananchi kwa ujumla wao ikiwa ni pamoja na wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi:-

Je, mpango wa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi unajitokeza wapi katika Mipango yetu ya Maendeleo?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Vick Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa, maendeleo kamili ya nchi yanatokana na mchango wa Wananchi wake, ikiwa ni pamoja na Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi, yaani *Diaspora*. Kwa kutambua hilo, llani ya CCM ya Mwaka 2005 na 2010 ilielekeza Serikali yetu kuwahuishwa Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje, katika michakato yetu ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011- 2016), suala la kuthamini rasilimali watu zilizopo ndani na nje ya nchi yetu limezingatiwa na limepewa kipaumbele. Jamii ya Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje huthaminiwa sana duniani na tukijipanga vizuri, jamii hiyo ina uwezo mkubwa wa kusaidia Taifa letu katika harakati zetu za maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni kama inavyotokea na kufanyika katika nchi nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, katika mwaka 2010 kiasi cha Dola za Marekani bilioni 40 ziliingia Barani Afrika kutoka kwenye Jamii ya *Diaspora* kama *remittances*, ambapo dola bilioni 21.5 pekee ziliingia katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Nchi zilizoongoza kupokea *remittances* hizo ni Nigeria dola bilioni kumi, Sudan dola bilioni tatu na nukta mbili, Kenya dola bilioni moja na nukta nane na Senegal dola bilioni moja nukta mbili.

Sisi Tanzania kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu, tunapokea wastani wa dola 250 milioni tu kwa mwaka. Mbali na maingizo haya ya fedha, Watanzania waishio nje, wana ujuzi wa kila aina ambao tunaweza kuutumia kwa faida yetu, badala ya kila mara kutegemea ujuzi wa Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Serikalini tumejipanga vizuri na tunajenga mazingira mazuri ya kuitambua na kuitumia jamii ya Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ili kuongeza kasi ya maendeleo.

MHE. VICK P. KAMATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali italeta rasmi Muswada wa Sheria ya Uraia wa Nchi Mbili ili tuweze kuujadili humu Bungeni?

MWENYEKITI: Ninakushukuru, Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Vick Kamata, swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, Serikali inao mpango wa kuondoa kero ya Watanzania wanaoishi nje na moja kati ya kero hizo ni suala la uraia pacha, yaani *dual citizenship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano ya Katiba yanayoendelea hivi sasa, tunakusudia kuliingiza suala hili kwenye majadiliano ya Katiba ili itakopofanyiwa marekebisho yake na majadiliano yake na kupitisha suala la uraia pacha litakuwemo katika suala hili na litakopofika katika kipindi hicho tutawasilisha Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwape heshima yenu sana, lakini kulingana na muda ninaomba niendelee. Ninaomba nimtendee haki Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, aweze kuuliza swali lake.

Na. 96

Kikosi cha Uokoaji Majini - Musoma

MHE. VINCENT J. NYERERE aliuliza:-

Kumekuwepo na ajali nyingi za majini kati ya Musoma na Rarya:-

Je, Serikali itaweka lini Kikosi cha Uokoaji Majini katika Manispaa ya Musoma Ufukwe wa Mwigobero ili kunusuru maisha ya watu wakati wa ajali hizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) - K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa naiba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na nchi nyingine za Jumuiya za Afrika Mashariki, imeanza maandalizi ya kujenga kituo cha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria. Mwanza imeteuliwa kuwa mwenyeji wa kituo hicho, ambacho kikikamilika kitakuwa

na nyezo za kutosha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji katika Ziwa hilo. Chini ya utaratibu huu, vituo vya ufuatiliaji na uokoaji vinatarajiwa kuanzishwa katika maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria. Kwa kuanzia, Serikali imetenga ofisi kwa ajili ya kituo hicho kuanza shughuli zake kabla ya kuwa na jengo lake Mwanza na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wamekubaliana kutenga fedha za uendeshaji wa kituo hicho kwenye bajeti ya 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kuwa, kuanza kwa kituo hiki hapo mwakani, kutanusuru sana maisha ya Wananchi wanaotumia ufukwe huo wa Mwigobero mara zinaopotokea ajali za majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumbua umuhimu wa kuwa na vyombo salama vya usafiri kati ya Musoma na Ronya, Serikali imeamua kujenga kivuko kipyka kwa ajili ya kuvusha watu kati ya Mwigobero Musoma Mjini na Kinesi Ronya. Ujenzi wa Kivuko hicho unatarajiwa kukamilika na kuanza kazi mapema mwakani (2012). Bila shaka chombo hicho kitaboresha huduma za usafiri kati ya Musoma na Ronya na kupunguza tishio la ajali za majini katika eneo hilo.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, ninasikitika swali langu la Musoma linajibowi Mwanza, mimi nilikuwa ninapenda swali langu la Musoma Ijibowi Musoma. (*Makofii*)

Swali la pili ni kwamba; tuna kikosi cha uokoaji na zimamoto katika Manispaa ya Musoma na Uwanja wa Ndege wa Musoma. Kwa nini Serikali isiwachukue watu hawa na kuwapa mafunzo pamoja na vifaa kwa ajili ya uokoaji majini? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri na ukizingatia majibu ya msingi ya swali la Musoma kujibowi kwa *reference* za Mwanza, ninadhani kutatakiwa kutoa majibu ya ziada kwenye swali hilo labda uingie swali la pili.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba radhi kwa kutokuwepo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Uokoaji kinachojengwa Jijini Mwanza kitakuwa na uwezo wa kuona matukio yote ya ajali katika Ziwa Victoria ikiwemo Musoma. Huu ni utaratibu unaotumia *radar* na *satellite*. Aidha, vifaa vya uokoaji kama maboti maalum na vifaa vingine vya uokoaji vitakuwa katika bandari zote za Ziwa pamoja na ile ya Musoma. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa maeneo hayo, waondoe shaka kwani Serikali yao makini imeliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa mafunzo kwa Wataalam wa Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji waliopo Manispaa ya Musoma, pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Musoma, Wizara kwa niaba ya Serikali imelipokea jambo hili na italifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea Maziwa yote Makuu, Victoria, Tanganyika na Nyasa, hizi changamoto Wizara ya Uchukuzi na Serikali ya Awamu Nne, imezitambua na inazifanya kazi kupata ufumbuzi endelevu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kulingana na muda, ninaomba niruhusu swali la mwisho kwa maana ya leo, kwa sababu Mheshimiwa Chibulunje ameondoa swali lake namba 98. Kwa hiyo, ninaomba nimwite Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

Na. 97

Utafiti wa Mafuta na Gesi - Rukwa

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Kati ya Mwaka 1984 na 1989 Serikali ilitoa kibali kwa Kampuni ya *Western Geophysical* ya Marekani kufanya utafiti wa Mafuta na Gesi katika Bonde la Ziwa Rukwa kwa nia ya kujua upatikanaji wa nishati hizo katika eneo hilo:-

- (a) Je, Serikali ilipatiwa taarifa gani kuhusu utafiti?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali kwa kampuni nyingine kufanya utafiti mwininge ili kujiridhisha na utafiti wa awali?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1985 Kampuni ya *Amoco Production Company* iliyosajiliwa Jimbo la Delaware Nchini Marekani, ilimtumia mkandarsi Kampuni ya *Western Geophysical* ya Uingereza ili kukusanya takwimu za mitetemo kwa maana ya *seismic data*. Kampuni hii ilikusanya takriban kilomita 1900 za mitetemo za *2D two dimension seismic data*. Takwimu hizo zilikusanya ndani na nje, *off and onshore* ya Ziwa Rukwa. Takwimu hizo za mitetemo za *2D zilitumika kutathmini* na kuhakiki aina na kina cha miamba iliyopo kwenye Bonde la Ziwa Rukwa. Hii ni hatua muhimu katika kuelewa endapo miamba hiyo ingelikuwa na uwezo wa kuzalisha na kuhifadhi mafuta na gesi. Kutokana na tathmini hizo, mwaka 1987, Kampuni ya Amoco ilichoronga visima viwili nje ya Ziwa katika maeneo ya Galula - 1 Kusini mwa Ziwa Rukwa na Ivuna - 1 Kusini Magharibi mwa Ziwa Rukwa. Uchorongaji wa visima hivi haukugundua mafuta wala gesi. Kampuni ya Amoco, ilijitoa kwenye utafutaji mafuta katika eneo hili mwaka 1992.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na *TPDC* illendelea kuwatafuta wawekezaji wengine wa utafutaji wa mafuta na gesi kwenye Bonde la Ziwa Rukwa. Mafanikio ya utafutaji wa mafuta katika Bonde la Ziwa Albert huko Uganda, yamesaidia kulifanya Bonde la Ziwa Rukwa kuwa kivutio.

Bonde hili lina tabia za kijiolojia zinazolingana na Bonde la Ziwa Albert. Juhudi za kutafuta mwekezaji zilizaa matunda mnamo tarehe 27 Oktoba, 2011 ambapo Serikali, *TPDC* na Kampuni ya Heritage Rukwa (T) Limited, iliyosajiliwa hapa Tanzania na kumilikiwa na Kampuni Tanzu ya Heritage Oil Plc ya Uingereza, waliingia Mkataba wa Utafutaji Mafuta kwa kugawana mapato. Mkataba huu ni wa miaka kumi na moja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uchambuzi wa jibu lake unaonesha nini kinaendelea. Nina swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa utafiti uliofanyika awali katika Ziwa Rukwa unaonesha haukuwa wa kina na wa kizalendo; na kwa kuwa Kituo hicho kuendelea kutafuta watafiti wengine imetokana na ugunduzi wa mafuta katika Ziwa Albert ambalo kijiolojia linafanana na Ziwa Rukwa:-

Je, Serikali imejipanga vipi kusimamia watafiti wa mara ya pili ikiwa ni pamoja na kushirikisha watafiti wazawa ndani ya nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Mallocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, *geological features* za Bonde la Ziwa Albert zinafanana na Bonde la Rukwa, lakini hiyo siyo tafsiri ya moja kwa moja kusema kwa sababu Albert wamepata mafuta na Rukwa tutapata mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni vizuri tuliweke bayana ni kwamba, teknolojia iliyokuwa inatumika miaka ya 80 imetofautiana sana na teknolojia inayotumika hivi sasa kwani kuna mambo kama nilivyosema; hawa watu walikwenda kwenye *two dimension* lakini sasa

wanakwenda kwenye *three dimension sites mid data analysis* na masuala mengine. Kwa hiyo, teknolojia ya kufanya utafiti imebadilika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, Wataalamu wa Wizara, wa *TPDC* na wa *Heritage Oil*, kwa pamoja tutakuwa tunafuatilia kwa karibu maendeleo yanayopatikana ili kwa pamoja tujuje kinachopatikana na kinachoendelea kwa manufaa ya Watanzania wote.

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri na sasa ninaomba niendelee na matangazo.

Kwanza kabisa, ninaomba niwatambue wageni waliopo katika Jukwaa la Spika, leo tumetembelewa na Mheshimiwa sana, Balozi wa Sweden Nchini Tanzania, Bwana Lennarth Hjelmaker, ameambatana na Bibi Margareta Brisman pamoja na Bwana Daniel Axxelson na Mr. Tumsifu Mmari. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wapo pia na Bwana Mark Polatjko, Mwambata wa Ubalozi, anayehusika na masuala ya Habari na Siasa na Bwana Victor Mlunde, ambaye ni Mchambuzi wa Masuala ya Siasa. Karibuni sana. (*Makofii*)

Yupo pia Dkt. Caroline MacQueen, Afisa wa Masuala ya Siasa, ameambatana na Ndugu Selemani Rehani. Pia wameambatana na Bibi Veslemoy Lothe Salvessen, ambaye ni Afisa wa Ubalozi wa Norway. Vilevile wameambatana na Bwana Logan Wheeler, Afisa kutoka Ubalozi wa Marekani, wakiwa na Bibi Tina Mdobilu. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Leticia Nyerere ana wageni wake kutoka Chama cha *The Green* cha Nchini Marekani. Wageni hao ni Bwana Rick Tingling, Bibi Michelle Clemons, Toussaint Tingling na Bahati Abel. (*Makofii*)

Pia kuna Watumishi kutoka Bunge la Kenya na Ghana katika ziara yao ya mafunzo kwenye Bunge letu; wa kwanza ni Ndugu Rebecca Musongo kutoka Kenya, Jecinta Nyeri kutoka Kenya, Winnie Morogo kutoka Kenya, John Kinuthia kutoka Kenya, Dinah Hammond kutoka Ghana na Charlotte Amakie Doke kutoka Ghana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hao kuna mgeni wa Mheshimiwa Waziri Mathias Chikawe na Waziri William Ngeleja, naye ni Balozi Ami Mpungwe. Karibu sana. (*Makofii*)

Vilevile wapo wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo nao ni wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Elimu, ninaomba wasimame kama wapo hapa ndani. (*Makofii*)

Vilevile tuna wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma. Wageni watatu kutoka CHAWATIATA, sasa hiyo CHAWATIATA sijui ni kitu gani lakini ni CHAWATIATA kutoka Mkoa wa Dodoma. Pia tuna wafanyakazi watatu kutoka *ORYX Gas* na *NEMC* wakiongozwa na Ndugu Moufidh Maulid; sijui wameketi wapi lakini karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia nina matangazo ya kazi; taarifa ya Kikao cha Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Tafadhalii, ninaomba uwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo tarehe 16 Novemba, 2011 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa *Basement*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti, Profesa David Mwakyusa, anawaalika kwenye kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo linalofuata ni la Kikao cha Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Ninaagizwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Ndugu Peter Serukamba kwamba, niwaombe tafadhalii Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 16 Novemba, 2011 saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala, Gholofa ya Pili. Mnaombwa Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu muweze kushiriki.

Waheshimiwa Wabunge, labda kabla sijaendelea na matangazo mengine, ninaomba niwataje wachangiaji watakaoanza kuchangia *agenda* ili waweze kujandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatia Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Agripina Buyogela.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa ninaomba nimwite Katibu kwa *agenda* inayofuata.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ninaomba ukae chini kwanza, kisha ninaomba usimame kwa utaratibu unaotakiwa ndani ya Bunge kutoa taarifa bila kufanya ulichokifanya.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Kanuni namba ngapi?

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Kanuni ya 47 ikisomwa sambamba na Kanuni ya 48.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa taarifa kuwa, kuna suala linaloendelea hivi sasa katika Wilaya ya Meatu Mkoo wa Shinyanga, ambalo ni la dharura sana.

Mkuu wa Mkoo wa Shinyanga, ameuagiza Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, kuanzia juzi kuanza kuchomaa nyumba kati ya 600 mpaka 1,000 zilizopo kwenye Hifadhi ya Jamii au WMA na Wananchi wameathirika sana, kwa sababu mpaka hivi sasa tunavyoongea, kuna watoto ambao wazazi wao wamekimbia wapo Polisi, Meatu, nyumba zimeungua pamoja na vyakula ndani yake na watu wengine hawajulikani walipo. Pia kuna mtu mmoja amevunjwa miguu amehamishiwa katika Hospitali ya Mkoo wa Shinyanga na baadaye kupata rufaa ya kwenda Hospitali ya Rufaa ya Bugando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tulijadili suala hili kama ni jambo la dharura ili angalau tuweze kuwapatia haki watu wanaohangaika na kuteseka Mkoani Shinyanga, Wilaya ya Meatu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, jambo hilo kwa kulitazama linaonekana ni la dharura, lakini kwa kuwa katika Kanuni zetu limechanganyika na mambo mengine mahususi, basi ninaomba nikushauri kwamba, uonane na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu ndiye mwenye Mamlaka ya Wakuu wa Mikoa ili tupate kulijua tatizo hilo kwa kina na Mheshimiwa Waziri Mkuu atashauri kadiri itakavyoonekana inafaa. Tunaendelea, Katibu kwa hatua inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011
(*The Constitutional Review Act, 2011*)

(Majadiliano yanaendelea)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwani tuna *agenda* nzito na mnazungumza bila kufuata utaratibu.

Ninaomba nimwite mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia ...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mnaotoka ninaomba mtoke kwa utaratibu ili tupate nafasi ya kuwasikiliza wanaochangia. Kuna umuhimu wa kuzingatia Kanuni, ninaomba muendelee kutoka taratibu.

Mheshimiwa Ndassa endelea.

MBUNGE FULANI: Wenye pesa ndiyo wa kwanza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasubiri hao ndugu zangu watoke kwa sababu ninaona wanapiga kelele lakini ...

MBUNGE FULANI: Wanafanya fujo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa, subiri wamalize kutoka kisha tutaendelea. Mheshimiwa Ndassa endelea.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana kwa nafasi hii na ninajadili suala zito ambalo lipo mbele yetu. Utangulizi wangu ni kwamba, nchi hii ni yetu sote, tungependa iendelee kuwa ya amani na utulivu na niwaombe sana hata hawa wenzetu amba kwa njia moja au nyngine wanasema wana nia nzuri, lakini nia yao siyo nzuri kwa sababu kama wangetaka kweli kuisaidia nchi hii, wangekaa ndani wakasikiliza na kutoa mawazo yao ili baadaye tuendelee, lakini ninaomba sisi tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala zito sana la nchi yetu, lakini mchakato huu umekuwa na mambo mengi sana na inawezekana kwa njia moja au nyngine, tuna wadau nje wanaosababisha mengine haya. Ninawaomba sana Mabalozi wanaoongoza nchi zao huko nje, amba kwa njia moja au nyngine inawezekana wapo hapa ...

MBUNGE FULANI: Wapo!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Watuache sisi Watanzania tufanye mambo yetu wenywewe kwani hii ni nchi huru na Mabalozi wana kazi zao maalum, lakini wanapokuja kwa njia moja au nyngine kusaidia kutaka kuhujumu shughuli nzito ya nchi yetu, kwa kweli siyo utaratibu mzuri na sijui kama Mabalozi wetu huko nje wanafanya hayo. Nina uhakika Mabalozi wote wana utaratibu wao katika nchi husika. Kwa hiyo, ninawasihi sana, kama mna utaratibu wa kukaa na vyama vingine, basi ikiwezekana mje mkae na Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndicho Chama Tawala. Bado ninasema nchi hii imejitawala miaka 50, tunafanya mambo yetu msituilingile tuachenii huru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo amba ninafikiri ulikuwa ni wa msingi sana, tunazungumzia Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Hii inaweza kuwa inachanganya sana, labda tungenesema kwamba, Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, hapo napo inge-sound vizuri, kwa sababu inawezekana watu wengine wanachanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya Katiba kama tutayasimamia vizuri, ninafikiri tutakwenda vizuri lakini inawezekana watu wengine wanasema Rais amepewa madaraka makubwa sana, siyo kweli! Jamani huyu ni Mkuu wa Nchi na katika mabadiliko haya kwenye Muswada huu kuna Ibara 34; Mheshimiwa Rais anasimamia majukumu manne tu, sasa haya majukumu manne watu wengine wanayabeza kwamba eti ni madaraka makubwa sana.

Hivi mnategemea nani aanzishe uundwaji wa Tume kama siyo Rais? Nani asimamie uteuzi wa Wajumbe kama siyo Rais? Nani awasilishiwe Ripoti kama siyo Rais? Nani atakayeitisha Bunge Maalum kama siyo Rais? Ninawaomba sana ndugu zangu msimwone Rais kama yeye, Rais siyo Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais ni Taasisi. Kwa hiyo, tusifike mahali tukasema kwamba eti

utaratibu wote huu Rais amepewa madaraka makubwa, hapana; madaraka haya ni ya kawaida kabisa wala siyo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotoka ni mbali sana ...

MBUNGE FULANI: Sana!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Kila mtu anajua tulipo sasa hivi na tunataka kwenda wapi, lakini ili tufike huko tunakotaka kwenda ni lazima utaratibu wa kuunda Katiba Mpya uanzishwe, kwa sababu utaratibu huu ndiyo tulionao sasa. Hivi tusipozungumza haya mnataka tukayazungumzie wapi maana uundwaji wa kila kitu ni lazima uanzie ndani ya Bunge?

Kwa hiyo, ninawasih sana ndugu zangu na ninawaomba sana Watanzania wenzangu kwamba tusipotoshwe na wenzetu amba wapo nje. Kwa mfano, wanasema eti Muswada huu umefanyiwa mabadiliko kwenye maudhui ya Muswada, lakini ninaomba niwasomee Sheria kwa ajili ya kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya Wananchi juu ya Katiba.

Pili, kuainisha na kuchambua maoni ya Wananchi. Tatu, kuainisha masharti kuhusu Mabaraza ya kuhalalisha masharti yaliyomo kwenye Rasimu ya Katiba; kuweka masharti juu ya utayarishaji na uwasilishaji wa Ripoti kuhusu maoni ya Wananchi; na mwisho ni kuweka utaratibu wa kuunda Bunge la Katiba.

Huu ndiyo Muswada na ndiyo maudhui yenyewe, sasa inapofika mahali huko nje watu wanasema Muswada huu umebadilishwa na kupotoshwa, huo ni upotoshaji wa dhati. Ninaomba tuwaambie Watanzania ukweli tuiswadanganye, hii ni sehemu ya kuanzia, tukishamaliza hapa ndugu zangu baada ya Tume tutapitia huu Muswada, Tume ikitoka hapo itakwenda ikakusanye maoni ya Wananchi kutoka makundi mbalimbali, baada ya hapo Rasimu ya Katiba kutokana na maoni hayo italetwa. Mbali na hayo, yapo mambo mengi ambayo yatazungumzwa; kwa hiyo, ninawasih sana Watanzania tujaribu kusikiliza, lakini tuone namna ambavyo Tanzania yetu itakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri au mapendekezo kwenye Ibara ya tano kuhusu kuundwa kwa Bunge la Katiba. Kwenye Ibara ya 20(2) kuna Wajumbe kwenye ile (c) kwamba, Mawaziri wenye dhamana ya mambo ya Katiba, lakini huku mwanzo kwenye (a) imezungumzia Wabunge lakini ninavyojua Mawaziri ni Wabunge.

Pili, kwenye ile (d) inayozungumzia Mwanasheria Mkoo wa Serikali; Mwanasheria Mkoo wa Serikali ni *Ex-Officio*, ambaye yuko kwenye Ibara ya 66. Kwa hiyo, ningeshauri nayo hiyo iondolewe kwa sababu tayari yeye anaingia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu ile ya (iv) imezungumzia Taasisi za Elimu ya Juu. Sasa Taasisi za Elimu ya Juu haikufanuliwa vizuri, ningeshauri ifafanuliwe. Unapozungumzia Taasisi za Elimu ya Juu; je, ni wanafunzi au wahadhiri wa vyuo? Kwa hiyo, ingefafanuliwa ingekuwa nzuri zaidi. Ile ya (v); makundi yenyе mahitaji maalum katika jamii ni yapi; je, ni ya walemavu au makundi ya vijana? Nayo pia ingefafanuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongezee lingine kama inawezekana; kuna baadhi ya makundi ambayo yamesahaulika, ambayo ingekuwa ni vizuri zaidi kama nayo yangeingizwa; kuna kundi kubwa la Wakulima ambalo halijatajwa; tuna kundi lingine kubwa la Wafanyakazi ambalo nalo halijatajwa; na pia kuna kundi moja la Wafanyakazi, ninafikiri ingekuwa vizuri zaidi kama nalo lingeingizwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeshauri ni kuomba tu kwamba, mabadiliko haya ya Katiba tunaiomba sana Serikali tusifanye mzaha hata kidogo. Tukisikiliza hawa wenzetu walioko nje, nina uhakika hawatatuifikisha pahala pazuri hata kidogo, kwa sababu wanasema maneno mengi sana. Ndugu zangu ninawaomba sana Watanzania, maeneo yote tusipotengeneza utaratibu huu leo na maneno yetu tunayoyatoa sisi hasa kama Viongozi wa

Kisiasa, hata kama ni Wanaharakati, tuzingatie utulivu tulionao ambao umeasisiwa na Baba wa Taifa na Vlongozi wengine Wakuu. Vingeneyvo, tukienda na utaratibu tulionao sasa wa kuchangamkia mambo ambayo hayana tija, hatuwezi kufika ambapo Tanzania yetu tunataka tufike. Tunataka tusherehekee miaka hamsini tarehe 9 Desemba, 2011 kwa amani na utulivu. Vurugu hazitatusaidia chochote kile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninaomba nikushukuru sana, lakini nisisitize Watanzania tunahitaji amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makof*)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kazi nzuri na kwa kuleta Muswada huu. Pia nichukue nafasi hii kipekee sana, kumshukuru na kumpongeza Rais wetu mpendwa, kwa kufikiria kuleta Muswada huu wakati huu; ingawa kweli wengi tunasema haukuwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, lakini Baba yako anapokuletea kitu kama hajakuahidi lazima ushukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusoma Muswada huu kwa umakini sana, ukurasa kwa ukurasa; wengi wameshasema mengi, lakini ninayo machache ya kuboresha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nilitaka nianze kugusia Ibara ya 5 ya Muswada ambayo inazungumzia Uundaji wa Tume. Kwenye Ibara hii tunaona mamlaka ya Mheshimiwa Rais ya kuunda Tume baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar. Pia Muswada huu unaelekeza kwamba, Mheshimiwa Rais pamoja na kushauriana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, atashauriana na Mwanasheria Mkuu wa Tanzania pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sababu ya msingi ya kuweka kipengele hiki cha Mheshimiwa Rais kushauriana na Wanasheria Wakuu wa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. Kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza Wanasheria Wakuu waondoke hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niangalie Ibara ya 20 ambayo Mheshimiwa Ndassa amemaliza kuizungumzia, inayohusiana na Muundo wa Wajumbe wa Tume hasa nilitaka nizungumzie Ibara ya 20(2)(a).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona Wajumbe wa Tume ya Bunge Maalum. Muswada huu unatoa nafasi ya kuongeza Wajumbe 116. Nimesoma kwenye Muswada huu nikajiliza hawa Wajumbe mia moja na kumi na sita wametoka wapi? Kwa nini wamekuwa hapa? Idadi hii ya mia moja na kumi na sita imefikiwaje? Kwa nini wasiwe kumi na tano? Kwa nini wasiwe mia moja na ishirini? Kigezo kipi kimetumika kuweka Wajumbe mia moja na kumi na sita? Pengine ningependa wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha anielimishe katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sijaona sifa au vigezo vyao vizuri vya kuwaweka hawa watu waliokaa hapa. Pia ukiangalia zimeelezwa Taasisi mbalimbali ambazo zitaunda Wajumbe hawa; Taasisi za Kidini, Asasi zisizo za Kiserikali na kadhalika. Ninajiliza pia hizi asasi hazijapewa idadi; hatujui ni Mashehe wangapi watakuwa ndani ya hao watu mia moja kumi na sita? Hatujui ni Maaskofu wangapi watakuwa ndani ya mia moja na kumi na sita? Hatujui ni watu wangapi watawakilisha asasi ambazo siyo za kidini? Kwa hiyo, nilidhani ni vizuri kwenye Muswada huu tukaweka idadi kamili kwamba, asasi za kidini zitatoa idadi kadhaa, asasi zisizo za Kiserikali zitatoa watu kadhaa na kadhalika ili sheria ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama alivyosema Mheshimiwa Ndassa, aliymaliza kuzungumza hapa, kuna makundi kusema kweli hayaonekani hapa; kuna makundi ya Wakulima nao wanahitaji kuwemo, kuna makundi ya Wafugaji sijawaona humu ndani na pia kuna makundi ya wenzetu Wafanyakazi sijawaona; ni vizuri nao wakawepo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa ninapenda nigosie Ibara ya 14 ya Muswada ambayo inahusiana na garama za shughuli za Tume. Muswada unaonesha kwamba, garama za Tume zitatoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Hilo sina tatizo nalo kabisa, tatizo langu linakuja kwenye Ibara ya 14(2). Ibara hii inazungumzia kwamba, Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watalipwa kwa kadiri Waziri atakavyoamua. Maneno haya kadiri Waziri atakavyoamua sikuyapenda.

Pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri anajua Kanuni za Fedha zipo, lakini anaweza akaamua kwenda kutoa malipo makubwa sana au pengine anaweza akatoa malipo ambayo hayakidhi ikilinganishwa na ile kazi ambayo itakuwa inafanyika. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Sheria ikae vizuri, haya maneno kadiri Waziri atakavyoamua tuyaondee ili sheria ikae vizuri. Tujue malipo ya Wajumbe wa Tume na Sekretarieti yatakuwa ni kiasi gani ili tuondoe huu utata ambao unaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye Muswada huu ukiangalia ni kwamba, mwisho wa siku litakuwepo Bunge Maalum. Bunge Maalum hili litakuwa ni tofauti sana na Bunge hili ambalo tunalizingumzia humu ndani. Malipo na mafao ya Bunge hili la kwetu la kawaida yanafahamika. Sasa kwa kuwa tutakuwa na Bunge Maalum ambalo litakuwa ni tofauti na hili, ninadhani ilikuwa ni vizuri kabisa malipo na mafao ya Bunge Maalum la Katiba yawekwe ndani ya sheria yajulikane, kwa sababu ukiangalia hapa Muswada haujasema chochote kuhusiana na malipo ya hilo Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni kuhusiana na Ibara ya 16 ya Muswada huu ambao tunaupendekeza. Ibara ya 16 ndio imetoa *terms of reference* (hadidu za rejea). Hadidu za rejea ndizo ambazo Tume itafanya kazi katika kuratibu maoni ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiangalia, zipo hadidu za rejea nyingi sana. Tunajua kipindi ambacho Tume imepewa ni kirefu na inaweze kana katika kufanya kazi hizo, kuna mambo yakawa yanabadilika kutokana na wakati. Hayo mambo yakitokea, Tume haitafanya jambo lolote mpaka ilete Muswada mwingine ndani ya Bunge hili, tuweze kubadilisha sheria hii ili tuwape *mandate* ya kufanya kazi fulani ambayo ilikuwa haimo katika hadidu za rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bunge letu litakutana Februari mwaka kesho, tutakapoondoka hapa tutakaa Desemba, Januari na Februari, ni kipindi kirefu sana na Tume itakuwa imeshaanza kazi na hivyo inaweza ikakutana na jambo ambalo ni muhimu sana kulifanya kazi na Bunge halitakuwepo kutunga sheria nyingine. Kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza hizi hadidu za rejea badala ya kukaa kwenye *body* (ndani ya Muswada), zikae kwenye Jedwali (*Schedule*).

Zikaa kwenye Jedwali maana yake ni kwamba, Waziri mwenye dhamana atakuwa na uwezo wakati wowote wa kuongeza hadidu za rejea ambazo anaona zina maslahi kwa Taifa hili. Kwa maana hiyo, ninaomba kipengele hiki kihamie kwenye Jedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa ninaliangalia ni Ibara ya 13(2), inayohusiana na Katibu wa Sekretarieti. Muswada unapendekeza kwamba, huyu atateuliwa na Rais, baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Sina wasiwasi na uteuzi wa Rais, ninafahamu Rais wetu yuko makini sana na timu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa ninaangalia tu hapa kwamba, kwa kuwa huyu Katibu wa Sekretarieti atakuwa anawajibika moja kwa moja kwenye Tume, nilidhani itakuwa bora zaidi Katibu huyu akawa mwajiriwa wa Tume. Ninapendekeza kazi hii ya Katibu wa Sekretarieti itangazwe, iwekewe vigezo watu washindane na mwisho wa siku tumpate Katibu ambaye ni bora, atakayewajibika moja kwa moja kwa Tume ya kuratibu maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie hapa kidogo ilikuwa ni kuhusiana na kazi za Tume. Kazi za Tume tumeziona ni nyingi sana, lakini mojawapo ya kazi hizi za Tume ni kuhusiana na kuratibu na kukusanya maoni ya Wananchi. Hapa ndio mahali ambapo ni

technical, pa ufundi sana. Kama Tume ita-*fai* kwenye eneo hili la kukusanya na kuratibu maoni ya Wananchi, basi kazi yote ambayo tunaifanya itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninapenda kushauri kwamba, Tume katika muda waliopewa wahakikishe wanajikita mijini, lakini pia waende vijiji ambako ndiko Wananchi wengi waliko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninapendekeza kuna maeneo ambayo yako pembezoni kama kule Tunduru, Sumbawanga - Rukwa kule, Karagwe, Ngara na sehemu nyingine, ninaomba Tume izame kabisa mpaka huko vijiji. Kwa mfano; kwenye Jimbo langu la Karagwe, nitafurahi sana kusikia Tume imejikita kule Bweranyange imechukua maoni, imekwenda Igurwa ikachukua maoni, imekwenda Kituntu, Ihembe, Nyaishozi, Nyakasimbi, Kandegesho na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kufanya hilo, Tume ihakikishe inatoa taarifa na muda wa kutosha ili Wananchi wajiandae, isiwe ni taarifa ya kushtukiza. Taarifa hii itolewe kwenye televisheni kwa muda wa kutosha, ratiba ijulikane mapema kwa Wananchi wote, itolewe kwenye redio. Kwangu kule Karagwe, tuna redio zetu; tuna Radio Karagwe ninapendekeza itumike vizuri sana kuwatangazia Wananchi. Tuna Radio FADECO Karagwe nayo itumike kuwatangazia Wananchi ili Wananchi wangu wajiandae vizuri kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu; wakati ninachaguliwa kule Karagwe waliniambia Blandes tunakutuma Bungeni ukatuwakilishe. Kazi yangu ni kuja kusema hapa kwa niaba ya Wananchi wa Karagwe.

Ninapenda kusema kwamba, Wananchi wa Jimbo la Karagwe wamepokea vizuri sana Muswada huu. Wapo waliochangia vizuri sana maoni yao na nimehakikisha kwamba, nimeyaleta hapa na ninashukuru kabisa kwenye *amendments*, Mheshimiwa Waziri amekubali mabadiliko. Kwa hiyo, Wananchi wa Jimbo la Karagwe nimewawakilisha vizuri sana humu ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakapotoka hapa nitakwenda kuhamasisha wajiandae kutoa maoni yao vizuri. Kwa heshima kubwa na taadhima, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Karagwe, ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mawazo yangu kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria imetuelekeza kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, Mbunge kazi yake ya kwanza ni kuishauri Serikali na kazi yake ya pili ni kuwakilisha mawazo ya Wananchi wake waliomchagua; hivyo basi, kwa kuwa ninawakilisha mawazo ya Wananchi wa Kasulu Vijiji, kwa niaba yao ninaomba nitangaze kwamba, ninaungana na mawazo ya Watanzania wanaosema Muswada huu usomwe kwa mara ya kwanza. Ndivyo nilivyotumwa na Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu ugomvi siyo Katiba tunayotaraja kuiandaa, mgogoro uliopo kwa Wananchi huko kuna wasiwasi mkubwa juu ya utaratibu huu kwamba, kwa kuwa kuna mabadiliko makubwa katika Muswada huu; ni vyema Wabunge tulipo hapa tunaowawakilisha Watanzania tupewe huu Muswada, tupate fursa ya kurudi Majimboni kwetu tuusome na tupate mawazo kutoka sehemu mbalimbali ili turudishe mawazo yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi uliopo hapa tunaweza tukavutana tu bila kujua tunachokifanya ni nini. Watanzania walio wengi wana hofu kulingana na Tume zilizotangulia hasa Tume ya Mwaka 1991, ambayo ilizunguka nchi nzima kutafuta maoni ya Watanzania wangapi wanaukubali Mfumo wa Vyama Vingi na wale wanaotaka Mfumo wa Chama Kimoja uendelee. Majibu yaliyotokea pale ni kwamba, asilimia themanini ilihitaji Mfumo wa Chama Kimoja uendelee. Ndiyo leo Watanzania walio wengi wanaendelea kujuliza; hivi isingekuwa hekima aliyokuwa nayo Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuamua kuungana na kundi la watu

wachache, leo mfumo wa Vyama Vingi usingekuwepo; na kama Mfumo wa Vyama Vingi usingekuwepo, umezia milango ya kusemea Watanzania walio wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sioni hofu na ninaishauri Serikali ikubaliane na matakwa ya watu walio wengi ili Muswada huu usomwe Mara ya Kwanza, mtakuwa mmerahisisha baadaye ukija kurudi hapa hakuna atakayepiga.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu, tuheshimu mawazo ya kila mmoja.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru hasa kwa kuheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba nishauri kwamba; ni vyema tukubaliane na Watanzania walio wengi, kwa sababu hatuna sababu yoyote ya kukimbiza taratibu za kuandaa Katiba. Ninavyoolewa, Watanzania walio wengi au binadamu tulioko Duniani, hakuna mtu asiyemhesimu Mwenyezi Mungu, kwa sababu anajua pumzi hii ninayopumua ni kwa ajili ya Mungu. Kitu cha pili kukihesimu Duniani ni Biblia, Msahafu na Katiba. Ninachokiona tunakiandaa hapa ni Mungu wa pili. Kwa sababu Katiba ndiyo inakueleza ni namna gani wewe uishi hapa Duniani na pia uishi hapa Tanzania kwa uhuru. Sasa kitu mnachokiandaa ni kikubwa sana kwa Watanzania.

Nilikuwa ninawaomba ndugu zangu tusiweke tofauti zetu za vyama, tusiweke ushabiki wa vyama, tuangalie Watanzania wanataka nini na tufike mahali tusije tukajiona na kujhesabu kwamba, sisi Wabunge tulipo hapa Bungeni ndiyo wenye akili sana kuliko wale tunaowawakilisha. Sisi ni kisemeo kwa niaba ya Wananchi waliotuleta hapa. Sasa ni vyema tufanye tathmini ya kina kujua Watanzania wanasemaje; kama wanasema Muswada huu usomwe kwa mara ya kwanza ni vyema tuwasikilize ili tuweze kutengeneza kitu ambacho hakitakuwa na malumbano baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa napenda kusema kwamba tunapokuwa tunafanya kazi kama hii, kuna neno moja linaitwa MMUA kirefu chake ni Maelewano, Maendeleo, Umoja na Amani, unajua muwa ni mtamu sana, na tusiposimamia haya maneno baadaye tutaleta matatizo. Mimi nilikuwa naomba ndugu zangu tusiwe na haraka katika kutengeneza hilo. Hii Katiba wote tunakubaliana kwamba tunataka Katiba ambayo inawekwa na wananchi, sasa kama wananchi ndio wanataka kuleta Katiba ni vyema tuwasikilize. Mkisikia watu walio wengi wanapiga kelele hata ikiwa ni robo tujifunze kwa Hayati Baba wa Taifa ambaye alikubaliana na asilimia 20 akaacha asilimia 80 kuna vitu alifikiria pale. Sasa leo mkionia watu wachache wanapiga kelele halafu watu mnaosema sisi ndio wenye mamlaka tutafanya tunavyotaka bado tutakuwa hatujafikia kwenye lengo letu la msingi la kuibadilisha hii Katiba iliyopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie hayo na hasa niliona ni vyema nionyeshe msimamo wa kile ninachokiamini kwamba Muswada huu umeletwa ukiwa na mabadiliko makubwa na mimi nipate nafasi kama nilivyoshauriwa na wapiga kura wangu na kupewa huu Muswada ili tuupitie vizuri, taratibu ambapo baadaye tukileta kwa mara ya pili utakuwa tayari hauna lawama.

Mheshimiwa mama yangu, dada yangu Waziri, hutakuwa na lawama kwa sababu tayari tunalilia turudi kwa wananchi, tukirudi tena maana yake ni kwamba hakuna atakayelalamika na mimi sioni kitakachoharibika kwa sababu kitu kimeandalisha tunakirudisha huko, tukileta ushauri unapokelewa kwa mara ya mwisho tunafanya marekebisho tunasonga mbele, hakuna sababu ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Katiba sio kitu cha dharura kama Muswada uliopitishwa juzi. Katiba ni kitu ambacho tunatakiwa tutulize akili zetu, tushirikishe bila ya kumdharaa mtu wa aina yejote, msomi, mjinga, msafi, mchafu wote waone kwamba wameshirikishwa. Mimi kwa kweli niliona ni vyema nisimame na nichangie na ninaishauri Serikali kwa nafasi niliyopewa ili tukubaliane na walio wengi Muswada huu usomwe kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, namshukuru Mheshimiwa Agripina kwa kutumia nafasi yake ya Kikatiba ya uwakilishi, ametekeleza jukumu lake vizuri kutoa maoni yake akiwa ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na mchangiaji anayefuata naomba sasa nimwite Mheshimiwa Mwigulu Nchemba halafu ningemba Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Igunga kwa kuchagua Mbunge anayetokana na CCM katika uchaguzi mdogo na hii wamekipa heshima kubwa sana chama changu na wamempa heshima kubwa sana Mwenyekiti wa chama changu na wamenipa heshima kubwa sana mimi niliyekuwa kiongozi wa kampeni katika huo uchaguzi mdogo kupitia Chama cha Mapinduzi, niwaahidi kwamba Serikali yetu pamoja na Mbunge walijemchagua hatutawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo sitazama sana kwenye mambo ya kitaalam, lakini nitajaribu kusema yale machache ambayo nimeyapata kupitia kusoma Muswada, lakini pia nitafafanua mengine kwa lugha iliyo rahisi zaidi ili Watanzania waweze kuelewa na nitawaomba sana Watanzania wasikilize kwa makini, watumie muda kutafakari haya tunayoyasema na baada ya hapo tunapopitisha Muswada huu waweze kuona kwamba nia tuliyonayo ni njema na sisi sote ni Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na hilo baada ya kuusoma Muswada huo na baada ya kuwasiliana na baadhi ya wapiga kura wangu maana yake ni wengi siwezi kusema nimewasiliana nao wote na baada ya kushauriana, kubadilishana mawazo niweke wazi kwamba naunga Muswada huu mkono asilimia mia moja kwa mia moja. Nikianzia na hilo hilo niweke wazi kwamba tunachokifanya hapa Watanzania waelewe tunatengeneza sheria, hatutengenezi Katiba hapa, hivi tunavyopitisha, hatupitishi Katiba, tunatengeneza sheria ambayo hiyo ni hatua tu ya kupanua wigo wa watu kutoa mawazo ni namna gani wapate Katiba ya aina gani. Kwenye hili tunalofanya tunatengeneza sheria ili wale watakaoenda kukusanya maoni wawe wanafanya shughuli ambayo inatambulika kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ningerudi Iramba mkanipa mawazo kuhusu Katiba kama hicho ninachokifanya si cha kisheria ni sawa na kuendesha mkuutano usio na muhtasari. Kwa hiyo, tunachofanya hapa tunatengeneza sheria ili kile chombo ambacho kitapita kukusanya maoni wawe wanafanya shughuli hiyo kisheria. Kwa hiyo, wananchi wa Tanzania ningewaomba tujenge utamaduni wa aina moja kwamba Watanzania milioni 42 hakuna siku tutakuwa na mawazo ya aina moja, hakuna hiyo siku. Hata watu wawili tu, ukiona kuna watu wawili wana mawazo ya aina moja ujue mmoja wao kati ya hao hafikirii. Kwa hiyo, Watanzania milioni 42 hakuna siku tutakubaliana kwamba mawazo yetu yaye moja kama moja ilivyo, lakini tunalotakiwa tujijengee utamaduni ni kuheshimu mawazo ya mwenzio. Usione yale unayoyatoa ndiyo hayo hayo tu na hapo ndipo tunapokosea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo tunayoyapata hata kwenye hili tunalotofautiana kusoma mara ya kwanza, kusoma mara ya pili, yote yale ni mawazo. Lakini ifike mahali kwamba mtu aseme nilikuwa na mawazo haya, lakini kwa sababu moja, mbili, tatu, nne nilizopewa hata hili nalo litatufikisha kwenye kitu kile tunachotaka kukipata. *A wise man changes his mind, but a fool will never*, hii naiona sana. Mtu anajiona lile analolisema ndilo hilo tu kama sio hilo basi utaratibu wote ni *fake*, huko tunakosea. Sasa hebu semeni tumefafanuliwa kisheria kwamba huu Muswada baada ya kuwa ulishaletwa tukapata marekebisho na ushauri wote wa kisheria ukarudishwa kwenye Kamati, Kamati imeshamaliza kazi yake, wewe unayesema urudishwe tena na usomwe mara ya kwanza baada ya hapa utapelekwa wapi? Hata mtoto akizaliwa kabla ya siku huwa anapelekwa mahali tu, lakini baada ya hapo harudishwi tumboni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lilitookena nikifanua kwa mfano rahisi zaidi ni kama vile tulikuwa na safari ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza tumefika Dodoma gari imeharibika, tumetengeneza mafundi tuliokuwa nao na mafundi wengine hata hawakuwemo kwenye ile safari, tumetengeneza imetengemaa, tumeshirikisha na wengine waliokuwa nje ya lile gari limetengemaa, sasa tunabishania kitu kimoja tu. Wengine tunasema baada ya kuwa imetengemaa sasa tuendelee na safari yetu, wengine wanasema maadam imetengemaa turudi Dar es Salaam kule kule tukaanze upya, *this is non sensible* maana tunafikiri tunarudi kinyume nyume Katiba hii hatutengenezi pambo, Katiba hii ambayo baada ya kupitisha huu Muswada watu wakatoa maoni, hatutengenezi pambo, tunategemea kitu hiki kikatoe ufumbuzi wa matatizo ambayo yameleteleza tuone kwamba kwa muda huu tunahitaji Katiba Mpya. Ni vyema Watanzania tukawa na malengo ya aina moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona hapa hatuna malengo ya aina moja. Inaruhusiwa kutofautiana mawazo, lakini kama nchi lazima tuwe na malengo ya aina moja. Kwa Watanzania walio wengi naiona kabisa malengo yao ni kuwa na Katiba Mpya. Lakini wengine wapo ambao dhahiri kabisa inaonekana malengo si ya aina moja. Tulio wengi tunaitumika Tanzania, lakini wapo nawaona wana mabwana wawili mtapasuka msamba. Hauwezi ukaridhisha Watanzania wanaotaka Katiba Mpya na ukaridhisha na wale wanaokwambia usipotoka nje ya Bunge basi uchaguzi ujao hatukupi fedha hauwezi ukaenda hivyo. Tena juzi juzi naishukuru sana Serikali yetu kwa kuwa na msimamo thabitii kuhusu ndoa za jinsia moja. Fedha za misaada zingine zina masharti magumu, wenzetu tayari walishaanza kupokea hiso fedha hatujui walipewa masharti gani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili niwaombe Watanzania tuwe na lengo la aina moja, tupitishe hili ambalo linahusu utaratibu tu, linahusu kuunda chombo kiwe na sheria ili kiweze kufanya hiyo shughuli kikiwa na mamlaka kamili. Kule kwenye utamu wa muwa kwenyewe ni kule ambako tutatoa maoni kwamba tunahitaji Katiba gani, tukichelewesha utaratibu huu nawaambieni hatutapata Katiba. Lakini kwa wale wenye malengo tofauti wanadhani tusipopata Katiba ni Rais ndiyo hajapata Katiba, tusipopata Katiba ni Tanzania hajapata Katiba Mpya. Wengine wanadhania tusipopata Katiba ni Chama cha Mapinduzi hakijapata Katiba ni Tanzania itakuwa hajapata Katiba Mpya. Kwenye Chama cha Mapinduzi watakuwa na Katiba yao. Ni vyema tukawa na lengo moja na huku tukijua kwamba tukipata Katiba Mpya tutapata ufumbuzi wa yale matatizo ambayo yalikuwa yanakwamishwa na Sheria Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wenzangu ni vyema tukaruhusu utaratibu huu ukapita ili tutoe maoni na baadaye tupate ufumbuzi kwa matatizo yanayolikabili hili rika la vijana. Wanavyuo tunapata matatizo makubwa sana kwenye ajira hata baada ya kuwa umemaliza shule tunapata taabu sana, unaenda kuanza kazi upya unaambiwa uwe na uzoefu wa miaka mitatu, tungetegemea tupitishe hili halafu sisi mjadala yetu tuwe tunalenga kwamba hivi hawa watu baada ya Muswada kupita watakopokuja hivi tuwape wazo gani kuhusu kutatua hili. Nilitegemea waseme kwenye Katiba Mpya itakayokuja waajiri wote wanapoajiri *graduates* waambiwe kigezo cha kwamba huyu hana uzoefu kisiwemo. Washauriane wao kule ambao wanatafuta mtu wa miaka 40 au miaka 15 kazini. Lakini pia nilitegemea kwa tatizo kubwa la ajira na hili la kuhusiana na kukosekana kwa uzoefu nilitegemea tuseme maadam wawekezaji huwa wanafutiwa kodi kwa kipindi huwa wanapata *grace period* nilitegemea Katiba Mpya labda vijana waseme sasa tutakapoenda kule Taasisi zote za Serikali, Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi Zisizo za Kiserikali zinapata *grace period* kutoka Serikalini ziwe zinachukua vijana wasiopungua kumi kwa mwaka mmoja ili wapate uzoefu wakati wanasubiri ajira ya kudumu. Liwekwe kule, tuweke kwenye mjadala wa kawaida. Wakulima, wafugaji kuna ugomvi wa ardhi na wawekezaji, kwenye utaratibu hatutatoa haya kwamba kuna hili, tutakuja kutoa wakati tunataka ile Katiba ambayo ndio itatatta hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi kuhusu upotevu wa mali kwenye Halmashauri. Madiwani wanasema sisi hatuna meno, wataalam wasio waadilifu wanajitengeneza makampuni, wanajipa zabuni wao kwa wao. Tulitegemea huu utaratibu wa kutengeneza utaratibu utengenezwe ili tukifika kule tuseme haya maoni yatakayoleta badiliko ni yale ya kule, lakini tukiendelea tu kusema Rais atateua Tume kwamba hili ni baya, Tume ile

itakayoteuliwa haipeleki mawazo yake, hata Rais akateua watu wake lakini hawapeleki mawazo yao, watapeleka mawazo ya wananchi, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kitu kingine kinachohusiana na hicho tunavyosema Rais amepewa mamlaka makubwa hivi Katiba ikija ya ajabu atakayelaumiwa ni nani, Jukwaa la Katiba? Amepewa mamlaka makubwa kulingana na ukubwa wa jukumu. Kama jukumu lingekuwa dogo angeweza kupewa hata Katibu Kata tu, lakini hili ni jukumu kubwa mno na la kulaumiwa aliyepewa dhamana ni yeye. Sasa hata Kocha tu wa timu huwa hapendi kupangiwa timu pamoja na kwamba wachezaji amewasajili yeye wote, leo hii mnataka kusema kwenye jukumu kubwa kama hili mnaongelea na hii Katiba tunayoongelea hata sisi ndio imetupa haya mamlaka ya kusema leo hapa. Kule ndiko tutakakosema haya si kwenye kupitisha utaratibu, kwenye utaratibu hatuwezi tukailaumu Katiba iliyopita. Tunatakiwa kuitumia itutengenezee muundo wote na baadaye tuweze kwenda kwenye hili tunalotaka kulifanikisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mawili ya kitaalam mengine yalishasemwa. Tumesema litakuwepo Bunge Maalum, ningeomba lile Bunge tuliacchie utaratibu wa namna watakavyoamua. Kwenye ile ngazi ya maamuzi tuliacchie Bunge Maalum lenyewe liweze kupanga ni namna gani wataamua kufikia makubaliano. Lakini tukirudi kwenye hili liliongoongelewa Ibara ya 20(2)(e) kwenye wale Wajumbe 116 hebu tuangalie je, tumeitumia 116 kuwapata 116, je, tumetumia kigezo cha Bajeti peke yake, kwa nini wasingekuwa wengi hata zaidi ya Wabunge ili kuonyesha kwamba lile ni Bunge Maalum, nitaomba Serikali wakati inajumuisha iweze kuyasema hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya mengine ya misingi mikuu ambayo tumeainishiwa kwenye Muswada mimi naunga mkono ibaki vilevile kwa sababu haina kinyume chake na hii tunapoongelea...

(Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili, Mheshimiwa.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Ahsante sana, narejea tena naunga mkono hoja asilimia mia moja kwa mia moja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ili aweze kuchangia lakini baada ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Steven Wasira. (*Makofii*)

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kutoa mawazo yangu juu ya Muswada ulioletwa mbele yetu. Nataka niseme wazi kwamba Wazanzibar wanajua kuwa Muswada ulioletwa hapa sio wa Katiba, bali ni mchakato wa kuunda Tume itakayosikiliza, kokusanya na kuratibu maoni ya wananchi juu ya suala zima la Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niseme Muswada huu umekuja chini ya Kanuni ya 86(2). Lakini aliyekuwa na mawazo mengine tofauti na hayo basi alikuwa atumie Kanuni ya 86(3)(a)(b), lakini hakuitumia.

Vilevile kama angelitumia Kanuni hiyo naamini kwamba Mheshimiwa Spika angetuuliza Wabunge, lakini kwa sababu mchangiaji wa Kambi ya Upinzani ametimiza masharti ya kuchangia Muswada huu bila ya kutumia vifungu hivyo basi hakuweza kuliuliza Bunge na nasema kwamba Muswada huu kuwepo ni halali. Vilevile nizishukuru Serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano na ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna walivyoshiriki kikamilifu katika kuupanga Muswada huu mpaka ukafika mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umezingatia kifungu cha 98(1)(b) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini vilevile ukazingatia kifungu cha 127(1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini pia ukazingatia kifungu cha 128(3) na (4) paragraph ya pili ukurasa wa 175 na

176 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwamba hapo tutakapofikia mahali tukakubaliana basi Muswada huu upitishwe na theluthi mbili kutoka Zanzibar na theluthi mbili kutoka Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumetolewa *schedule of amendment* na Mheshimiwa Zambi ambayo kifungu cha 6(c) kinataka kibadilishe maelezo yale kama yalivyo kifungu cha 6(c) cha Muswada kinasema; "Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha tatu, muundo wa Tume utazingatia msingi wa kuwepo kwa uwakilishi uliosawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano." Hivi ndivyo Muswada ulivyo, Mheshimiwa Zambi anataka kuturejesha nyuma kama kifungu hiki kifutwe na tufuate Jamhuri ya Muungano. Naomba tusije tukarudi nyuma, tukirudi nyuma basi Wazanzibar hatunao katika Bunge hili katika kupitisha suala hili. Naomba kifungu kibakie kama kilivyo kwenye Muswada. Marekebisho ya Mheshimiwa Zambi yataturejesha nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme kwamba hakuna muungano wa Arusha na Dar es Salaam. Kuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Sasa kama kuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Muswada ubaki, uheshimiwe kama ulivyo. Lakini vilevile niseme kwamba ikiwa kitafuatwa kifungu cha Mheshimiwa Zambi basi tutakubaliana au itakuwa mmekubaliana kufuata maelezo aliyojatoa Mheshimiwa Lissu ambayo ni kinyume na matakwa ya Muungano na ni kinyume na matakwa ya Watanganyika na Wazanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lissu anasema kwa kumfanya Rais wa Zanzibar kuwa mshirika sawa Kikatiba na Rais wa Jamhuri ya Muungano na pili kwa kuipa Zanzibar nafasi kubwa ya uwakilishi katika mchakato mzima wa Katiba Mpya. Sasa kama asiwe yeye mshirika wa muungano awe nani? Hakuna muungano wa CHADEMA na CCM, hakuna muungano wa CCM na *CUF*, kuna Muungano wa Watanganyika na Wazanzibar. Lakini vilevile anasema kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba upendeleo wa Zanzibar unapendekezwa katika Muswada huu kuhusiana na uwakilishi katika Bunge la Katiba na vyombo vingine vya maamuzi juu ya mchakato wa Katiba Mpya sio wa haki na haukulaliki. Nani haukulaliki? Sasa kama haukulaliki ni yeye na mimi nawaambia kwamba Wazanzibar mliopewa Viti Maalum na CHADEMA, CHADEMA haina maslahi na Wazanzibar na ndiyo maana CHADEMA haina Diwani Zanzibar, haina Mbunge Zanzibar wa kuchaguliwa. Chama cha Kitaifa na kinachojidai kama ni chama dume kinakaa hapa kinawatukana Wazanzibar, mimi nina wasiwasi na usajili wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Msajili wa Vyama vya Siasa naomba akichunguze Chama cha CHADEMA. Kweli ni chama kinachozingatia masharti ya vyama vya siasa.

Katika mchango wa Mheshimiwa Lissu anasema kwa maana ya uwakilishi katika Bunge la Katiba *CUF* ndiyo itakuwa chama cha pili kwa nguvu za kisiasa ndani ya Bunge hilo licha ya kuwa na Wabunge wawili wa kuchaguliwa kwa upande wa Tanzania Bara na licha ya kupata kura chache sana katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Si *CUF*, ni Zanzibar iliyo na haki sawa na Tanganyika katika hili. Sasa Mheshimiwa Lissu akisema kwamba ni *CUF* ndicho chama cha pili cha upinzani, mimi simuelewi. Wanaojulikana kama ni Kambi Rasmi ya Upinzani, sisi ni wapinzani lakini Kambi Rasmi ni wao na ndiyo maana kumbe sisi kama tungeungana na watu hawa tukaunda Kambi moja wangetupelekesha vibaya sana. Ni watu waovu ambaa hawana maslahi ya nchi na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudia kusema kwamba vifungu vya Muswada 5, 6, 7, 8, 9, 10, 13, 16, 20 mpaka 32 vibaki kama vilivyo. Kusiwe na sababu ya kufuata marekebisho ya kifungu cha sita. Ukrejesha kifungu cha sita kama Bunge hili halijawaka moto basi nakuhakikishieni Zanzibar kutawaka moto kwa sababu Wazanzibar hawatakulali kabisa kabisa! Hatuzingatii CCM, hatuzingatii *CUF* hapa tunazingatia Uzanzibar basi. Kwa hiyo, kwa kulinda Muungano wetu, kwa kulinda heshima ya nchi zetu basi Muswada ubaki kama ulivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN M. WASIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kutumia haki yangu ya kutoa maoni kuhusu Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme chimbuko la Muswada huu ilikuwa ni maoni ya wananchi kupitia vyama, kupitia taasisi zisizo za Kiserikali, kupitia madhehebu mbalimbli ya dini ambao walisema kwa kiasi kikubwa kwamba nchi yetu inahitaji Katiba Mpya. Hili jambo si jipya, jambo hili limezungumzwa miaka mingi ya nyuma na kwa hiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Rais wa watu wote, si Rais wa CCM akaamua sauti za wananchi zisimamiwe na Katiba mpya ipatikane kuelekea miaka 50 ya Uhuru wa nchi yetu. Kwa hiyo, hii itakayokuwa Katiba haiwezi kuwa Katiba ya chama fulani. Itakuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya watu wote. Kwa hiyo, tunapojadili suala hili tuweke maslahi ya watu wote na si maslahi ya chama fulani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuwe wa kweli kama Watanzania. Wakati tunafanya uchaguzi wa mwaka 2010 kulikuwa na vyama viliviyokuwa vinagombea mamlaka ya kuongoza Tanzania. Wenzetu wa CHADEMA walisema wao wakishinda itawachukua siku 100 kuweka Katiba mpya. Sisi tunasema tunawapatia Katiba Watanzania kwa miaka yote mitano. Leo tunaleta Muswada wanasema haraka ya nini? Mimi nauliza zile siku 100 wangepata wapi mawazo haya? Maana tuisahau tulichosema, tena tunakuwa wasahafuli sana, ni siku 100 sina uhakika kama ile Katiba mpya ilikuwa mfukoni, ilikuwa imekwishaandikwa, ingetoka wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nasema tutazame jambo hili kwa umakini katika kuzingatia maslahi ya nchi yetu zaidi kuliko kuzingatia maslahi ya chama fulani. Kauli ya Rais ilisema tukubali tuanze mchakato wa kuleta Katiba mpya na kazi tunayofanya hapa ni mwanzo wa mchakato wa kutafuta Katiba mpya. Sasa yapo mambo ya upotoshaji ambayo yamesemwa na mimi nataka niyaseme.

Moja wanasema Bunge sasa linajadili Katiba mpya tena wanaosema hivyo ni wasomi na ni watu wanaoheshimika katika jamii lakini kwa kweli Bunge hili huwa halitumii neno uongo lakini kwa kweli wanasema mambo yasiyokuwa ya kweli. Bunge hili hata kwa mujibu wa Katiba iliyopo haina mamlaka ya kuandika Katiba mpya kwa sababu Bunge hili ni zao la Katiba. Rais wa Jamhuri ya Muungano ni zao la Katiba na Mahakama ni zao la Katiba. Vyombo vyote vitatu haviwezi kuandika upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Wanaoweza kuandika Katiba mpya ni wananchi wa Tanzania au kwa kuwakilishwa na Bunge Maalum au wao wenyewe moja kwa moja ndio wenye mamlaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu anayesema kwamba Bunge hili sasa linajadili Katiba mpya anafanya kazi ya kusema mambo yasiyokuwa ya kweli na mambo yasiyokuwa ya kweli yana matatizo. Jambo lingine liliopotoshwa ni la kusema eti tupo hapa tunajadili Muswada kinyume cha Kanuni za Bunge lenyewe. Hili nalo si la kweli lakini hili sitaki kulisema sana kwa sababu hata Tundu Lissu naye huku akisema kwamba Kanuni hairuhusu lakini alijadili. (*Makof*)

Sasa Muswada ukisomwa mara ya kwanza wewe unajadili nini. Muswada ukisomwa mara ya kwanza ni kuwekwa mezani halafu Wabunge tunakwenda nao tunatafuta maoni ya wananchi na hivyo ndivyo tulitakiwa kufanya mwezi wa nne kwenda kupata maoni, Muswada unasema hivi wananchi wenyewe wanasema nini? Kama hatukufanya basi tukubali tu kwamba hatukufanya. Lakini sio kwamba nafasi ya kuuliza wananchi haikuwepo, si kweli. Halafu magazeti yote yalandika Muswada huu ili maoni yaje kwa njia mbalimbali, kwa maandishi na kwa mdomo. Kwa hiyo, kwamba Watanzania hawakupewa fursa ya kutoa maoni, nalo si jambo la kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimewasiliza wenzangu hapa wakimnukuu sana Baba wa Taifa na siku hizi tunamnukuu sana. Sasa na mimi nataka nimnukuu mahali ambapo alisema lakini hapakuandikwa. Wakati wa uhai wake alisema hivi; "ukikuta mtu mzima anadanganya watu wazima wenzake, anaweza kuwa na tatizo moja kati ya matatizo mawili. Au akili yake ndio imeharibika au anawadharau wale anaowadanganya." Sasa wale wanaodanganywa watachagua ni tatizo gani kati ya mawili wanayo. Je, akili imeharibika au anadharau Watanzania. Uchaguzi ni wao tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa niingie katika Muswada na maudhui yake, Sehemu ya Pili ya Muswada huu ili kuthibitisha tunachosema. Inasema madhumuni ya Muswada huu ni nini? Inasema madhumuni ya Sheria hii itakuwa ni kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayokusanya na kuratibu maoni ya wananchi. Ndiyo msingi hasa wa hii. Kuweka masharti kuhusu hadidu za rejea, kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa mpana katika kutoa na kuwakilisha maoni, kuainisha majukumu ya mamlaka ya Tume, kujenga muafaka wa Kitaifa katika masuala yenye maslahi kwa Taifa wakati wa mchakato kuhusu Katiba. Hayo ndiyo madhumuni katika madhumuni mengi. Sasa kama hayo ndiyo madhumuni uandishi wa Katiba uko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inazungumza juu ya kuunda Tume. Hapo ndipo kuna maneno yanaongelewa na nimepata fursa baada ya kupumzisha akili yangu na kuondoa jazba nilisoma nakala ya Tundu Lissu neno kwa neno, maana nilitaka kujua hivi huyu bwana anafikiri nini. Maana si Kambi ya Upinzani, Kambi ya Upinzani imegawanyika katika jambo hili, wenzetu wa *CUF* ndiyo hawataki. Kwa hiyo, inawezekana haya ni mambo ya CHADEMA au ni ya huyu bwana peke yake, maana hata hilo nalo linawezekana. Maana ukisoma vilevile hii karatasi yake inachanganya sana mambo. Katika sehemu moja kuhusu jambo hili la kuunda Tume anasema Tume hii ingeundwa na vyama vya siasa, kwamba vyama vya siasa vikutane ndiyo viunde Tume.

Ukienda mwisho unapozungumza juu ya Bunge la Katiba anasema Bunge hili halifai kwa sababu limeundwa kwa misingi ya vyama. Kwa hiyo, tufanye uchaguzi ambao utaleta wagombea usiokuwa na chama huyo huyo mmoja. Upande mmoja anataka vyama viunde Tume, upande mwingine hataki watu wa vyama waingie. Kwa hiyo, kuna katatizo hapa ambako ni vizuri kukachechi vizuri maana haya mambo ni ya kuishi. Wakati mwingine unaweza ukaugua bila kujua kama unaumwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachosema ni kwamba Tume itaundwa na Rais na huyu Rais tunampa Mamlaka haya ye ye anasema ni Urais wa Kifamle. Mimi nauliza ufalme upi maana hata CHADEMA waligombea urais ule kwa Katiba hiyo hiyo. Sasa walikuwa wanagombea urais au ufalme? Lakini tumemwekea masharti Rais juu ya namna ya kupata hao wajumbe, hatukumwambia ni *open*, amewekewa masharti hakuna muda wa kutosha lakini yapo masharti ambayo amewekewa. Hadidu za Rejea sasa zimehamishiwa kwenye Muswada kuonyesha kwamba mjadala ulifanyika na haya yametokea na ni mawazo ya wadau ambao tumehehishimu mawazo yao. Kwa hiyo, kusema wadau hawa hawakushiriki si kweli vilevile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiendelea kufika na mwisho ambako ni kuundwa kwa Bunge la Taifa, jamaa huyu katika maandishi yake anamnukuu Profesa Shivji, anasema Profesa Shivji alisema hesabu ya Wabunge hawa ukiunganisha Mabunge na wale watu 116, CCM itakuwa na Wabunge wengi zaidi katika Baraza la kuunda Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si suala la CCM, ni suala la uwakilishi. Mimi ni Mbunge wa Bunda, hakuna Mbunge wa CHADEMA kule mwingine, ni mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawakilisha wote wale, wawe wa CHADEMA, wawe *TLP*, ndiyo walionichagua, kwa hiyo, mimi nawasemea wote. Ukishachaguliwa huwi tena wa chama chako peke yako. Na Rais naye tunampa mamlaka haya kwa sababu naye ni Rais wa wote, siyo wa chama chake. Haya ndiyo masuala ya msingi. Lakini elimu haina mwisho, kwa hiyo tutaendelea kusoma na kusoma na kujelimisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwisho nataka niseme, Watanzania wenzangu, tujelimitshe, tuelewe ukweli wa jambo hili. Hatutungi Katiba hapa, tunaandaa mazingira ambayo wananchi ndio watakaotunga Katiba. Tume hii itakwenda kwa wananchi, kila Kijiji, kila Mtaa itapata maoni. Maoni yale yakiandikwa vizuri, yatawasilishwa kwenye Bunge la Katiba ambalo wawakilishi wa wananchi watakuwepo. Lakini hata baada ya Bunge la Katiba kukubali, bado kabla hajjava sheria, tutaanzisha mjadala ambao utakwenda kwenye kura ya maoni ili mwananchi asome,

aelewe, aseme mimi nakubali hii Katiba au naikataa. Demokrasia inayozidi hapo itakuwa ipi ambayo kila mwananchi anapewa haki ya kusema, anakubali au anakataa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaminya demokrasia kwa msingi upi wakati tunasema wananchi ndio watakoosema Katiba hii nzuri au mbaya. Anasema Tundu Lissu kwamba humu tumesema ikiwa haitakubalika Katiba ile, Katiba iliyopo iendelee, anasema haiwezekani. Sasa kama haiwezekani ile iliyopo kuendelea, tutakuwa na nchi ya Katiba ipi? Yaani ghasia na maandamano ndiyo yatakuwa Katiba? Lazima iwepo Katiba ili nchi iendelee. Kama tunarudia, tunarudia, lakini Katiba ipo na amani ipo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kuwaambia Watanzania, nchi hii ni yetu wote. Ni sawa na kuishi kwenye nchi moja, ukiona mtu anasema anataka kuchoma nyumba ambayo mnaishi mle wote, lazima kutahayari na kumwambia unachoma na wewe umo, acha! Unamwambia acha kuchoma! Akizidi sana tunampeleka Mirembe ili kuwa na hakika kama hali yake ni nzuri. Maana hatuwezi kumruhusu achome nyumba wote tumo! Eee, kama ni ugonjwa, tutamsaidia tu kumtibu, ni mwenzetu. Lakini hatuwezi kumruhusu akachoma nyumba ambayo wote tumo. (*Makof!*)

Kwa hiyo, hao wanaosema sasa tunakwenda kuandamana, sisi Wabunge wengine tunakwenda kwa wananchi kuwaambia mjiandae kutoa maoni juu ya Katiba Mpya. Yule anayeandamana, ataandamana kwao huko, lakini baadaye naye tutamwambia na hata kwenu huko nako uandamane kwa amani, maana unataka kuchoma nyumba ambayo wote tumo, na hii hatuwezi kukuruhusu. Kwa hiyo, tunataka mjadala, tunataka amani katika nchi yetu, tunataka utaratibu ambao utatupa Katiba Mpya bila mfarakano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja! (*Makof!*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mzee wetu Wasira kwa mchango wako. Nafikiri wamekusikia. (*Makof!*)

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wa SMT na Waziri wa Katiba na Sheria wa SMZ kwa kazi hii nzuri waliyoifanya hadi leo imetufikia kwa madaha tunaizungumza. Basi nawapa hongera. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sina budi kuwaambia Wazanzibari wote ambao ni Watanzania kwamba Muswada huu msiuogope, hauna matatizo. Na sisi wenzeni tupo tunaona kila kinachotendeka hapa, msiwe na wasiwasi, ngojeni Tume iundwe. Tume ikishaundwa, mtatoa maoni yenu. Zile kero zenu mlizonazo hapa ndipo mahali pa kuzitoa. Sasa mtakaorudi nyuma, mkiwa hamjaenda mtakuwa bado hamjajitendea haki ili kuchangia Katiba yetu. Lakini tunachokizungumza sasa hivi hapa Bungeni siyo Katiba, tunatayarisha Tume itakayosimamia mchakato wote wa Katiba jinsi itakavyokuwa. Sasa hizo kelele mtakazoisikia ndugu zangu huko nje, lazima mfahamu, kama hamjaelewa, sisi tukirudi, tutawaelimisheni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakwenda moja kwa moja kwenye Muswada. Jina la Muswada ni refu lakini limejitosholeza kulingana na maudhui ya Muswada huo. Kwa hiyo, halina tatizo linaweza kuendelea kuimarisha Muswada wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamekuwa na wasiwasi katika hadidu za rejea. Wasiingiwe na wasiwasi kwa sababu zimejikita kuanzia kifungu cha 8, kifungu cha 9 ambacho ni misingi mikuu ya kazi hiyo na kifungu cha 16 ambacho kinasema utendaji kazi wa Tume hiyo. Sasa vitu vyote hivyo kama kweli utausoma Muswada, vitu hivyo vinajieleza kwa ufasaha na vinafahamika na vinaelewaka, ambacho ni kero ndogo tu hapa, ni kwa nini havikuandaliwa kabisa kwa urefu vikaingizwa katika jedwali. Lakini na hiyo siyo kazi ngumu wakati kitu kipo na nina uhakika mtakiweka kutokana na marekebisho yetu haya tunayoyatoa sasa hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaingia kifungu namba 18; Uwasilishaji wa Ripoti ya Tume. Ripoti ya Tume baada ya kuwa imeshamaliza kupita kwa wananchi wa Tanzania nzima, Bara na Visiwani, wakiwa wameshahapeka kero zao, maelezo yao, furaha yao, kila ambacho wanaona kikiingia kwenye Katiba hii kitafanya kazi, watatengeneza rasimu ya Katiba. Rasimu ya Katiba ikishatengenezwa itabidi iwasilishwe kwa Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi tu hapo nilikuwa naushauri ambaao Muswada unasema Mheshimiwa Waziri atauwasilisha, si mbaya. Lakini nataka ashirikiane na Mwenyekiti wa Tume kwa sababu yeye ndiye aliyetembea kwa wananchi, aliyeona kero za wananchi na atajua wakati anaulizwa, atajua kwa vitendo, kwa sura za wananchi alivyozunga, kwa vitendo vya wananchi alivyozunga. Kwa sababu Waziri hakutembea, atakuwa kama kapata taarifa kwenye ile rasimu kama ni mtu wa Serikali, lakini bado hajajua kilitendeka nini kwa wananchi. Sasa mimi naomba washirikiane kwa pamoja wapeleke rasimu hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningekwenda tena kwenye kifungu cha 30 pamoja na 32; kura za maoni. Haki ya kupiga kura ya maoni ya Muswada huo ambaao utakwenda kwa wananchi baadaye kutoka rasimu, tunasubiri sasa wananchi watoe baraka zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumesema kwamba kitakachotumika pale ni daftari la wapiga kura la Bara na daftari la wapiga kura kwa upande wa Zanzibar. Lakini ukiangalia Muswada kwa upande wa Zanzibar hawakusema daftari la kudumu la wapiga kura, wamesema daftari la wakaazi la wapiga kura. Sasa inabidi waangalie pale warekebishe kwamba yote, huku daftari la kudumu la wapiga kura na huku Zanzibar daftari la kudumu la wapiga kura. Hali hiyo itakuwa siyo mbaya, inakubalika kwa sababu kura nydingi tumeshapigana, tumepata Wabunge, tumepata Wawakilishi, na tumepata Madiwani, halina tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika kifungu namba 32: Kifungu hiki kinasema baada ya Zanzibar kumaliza kura za maoni, itabidi wazilete Tanzania Bara kwa ajili ya kutangazwa rasmi. Sasa mimi nimehisi hapa wakati kule Zanzibar ndiyo wamesimamia mchakato wote, basi na wao wangepewa baraka kwa kushirikiana NEC na ZEC kutoa baraka katika matangazo, wakawa pamoja, yakatoka matangazo kwa pamoja, wakashirikiana ili kuleta uwiano kwa pande zote mbili kwamba kitu hiki ni sahihi na kilitendeka hivi kwa utaratibu wa maelekezo tuliyopewa ndani ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naingia kwenye mchakato wa Bunge Maalum wakati lipo kwenye Bunge lake. Pale kidogo kuna kitu kinanipa wasiwas. Tunaingia Wabunge wa Bara, tunaingia Wabunge wa Visiwani, tutafanya kazi kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo. Lakini ukiambiwa kuna Mwanasheria, kuna Mawaziri ambaao wanataka waingie; kwa sababu mimi najua Mwanasheria ni Mbunge na Waziri ni Mbunge; na Bunge ile wote mnaoingia ni sawa sawa, hamna Waziri, hamna Mwanasheria, mle mnatakiwa muingie Wabunge na wale 116 walioteuliwa pamoja na Mwenyekiti wetu na Makamu wetu na Katibu na Naibu Katibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningependekeza hawa Wanasheria na Waziri wasilingie kwa vyeo vyao kama watalaaam, waingie kama Wabunge ambaao watapiga kura katika Bunge Maalum au Bunge la Katiba au wakitaka kuingia kama watalaaam, ina maana wao watakuwa hawana kura? Kama wataingia kama watalaaam, basi watakuwa hawana kura. Lakini wakiingia kwa mujibu wa nafasi zao kama Wabunge, kama Wawakilishi, basi inakuwa kitu hicho hakina tatizo, wataweza kupiga kura bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa haya yangu niliyoeleza ni mepesi na muda najua umekwisha na najua nimeleweka. Nimeeleweka na Watanzania, nimeeleweka na Wazanzibari na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Muswada hauna matatizo, tunakwenda kwenye Tume. Bado mchakato wa kutoa maoni ya Katiba. Watanzania msidanganywe. (*Makofii*)

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ili nami leo niweze kujadili Muswada ambaao uko mbele yetu. Ni fursa muhimu kwangu kwa sababu Muswada huu ni muhimu sana na umekuja katika wakati muafaka, wakati ambaao Watanzania wote tunayo hamu kubwa ya kuona nchi yetu inaingia

katika mabadiliko makubwa ya Kikatiba yatakayotuwesha kuziba mianya mbalimbali inayopelekea Taifa hili kupata hasara kubwa katika masuala mbalimbali, masuala ambayo yanarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa sababu ya kuwa na dhamira ya dhati katika kuleta Muswada huu kwa wakati. Ni dhamira yake ya kisiasa kuona kwamba nchi yetu sasa tunasonga mbele na katu hatutamani kurudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Kamati ya Sheria na Katiba na wadau na wananchi mbalimbali ambao wamejitokeza kutoa maoni na mawazo yao kuitia majukwaa mbalimbali, mengine majukwaa rasmi, mengine majukwaa yasiyo rasmi, kuitia vyombo vya habari, kwa sababu kwa kufanya hivyo imetupa mwanya na fursa ya kufahamu mawazo ya Watanzania wenzetu, na sisi kama wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tumeona ni vizuri tuwapongeze kwa sababu mawazo na mchango wao tunaviheshimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba Tanzania ni nchi huru na uhuru huo unatuwezewesha sisi kupanga, kujadili na kuamua mambo yetu pasipo kuingiliwa na mtu yeoyote yule. Ninasema hivi kwa sababu ninapata hofu kubwa sana kwamba ipo sasa dhana kwamba wapo baadhi ya watu, zipo hata nchi rafiki ambazo kwa wakati mwingine hawana nia njema, wanajaribu kuingilia mchakato huu wa Watanzania kupata Katiba yao, nadhani jambo hili siyo jema. Tutaendelea kushirikiana na rafiki zetu popote duniani lakini wale wenye nia njema ya kuona kwamba Taifa hili linakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayazungumza haya kwa sababu zipo dalili kwamba kuna baadhi ya watu, Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo kwa kiwango kikubwa kuitia mijadala yao, unaona kabisa hapa lipo tatizo la kimsingi. Lakini Watanzania tunasau, tunaacha uzalendo kwa Taifa letu kwa sababu ya misaada inayopenyezwa katika taasisi hizo ili kuchochaea, ili kuleta mawazo hasi na wananchi wasipate fursa ya kupata Katiba mpya tunayoizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge humu ndani, tunajadili Muswada huu na tunafanya kazi hii na tunalipwa kuitia kodi za wananchi wetu. Kwa hiyo, haya tunayoyazungumza ni kwa sababu tupo kazini pia. Lakini wapo wenzetu ambao wanapaza sauti, lakini wanategemea hisani na malipo kutoka kwa wafadhili ambao wanaonekana hawana nia njema. Na mimi nitumie fursa hii kuiomba Serikali kwamba ipo haja ya kufanya uchunguzi wa kina na wale wote wanaobainika kwamba wanatumiwa aidha, kwa kisingizio cha misaada kutaka kuwapotosha Watanzania, wachukuliwe hatua. Mashirika na taasisi hizo zinafahamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa Kiswahili unaosema anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua wimbo. Hawa wenzetu hili zumari wanadolipiga na kuchaguliwa wimbo na mpiga zumari ni kwa faida na manufaa ya nani? (*MakofiKicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya Watanzania wenzangu kushirikiana, kushikamana na kuhakikisha kwamba mchakato huu unafika mahali pazuri na Watanzania tupate Katiba Mpya itakayokidhi haja na matakwa yetu na si kwa ushawishi wa mtu mwingine yeoyote au Taifa lingine lolote kwa sababu nchi hii ni huru na tutajiamulia na kupanga mambo yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Muswada wenyewe. Maudhui ya Muswada, Ibara ile ya 4 yamejieleza vizuri na Mzee Wasira ameyasema vizuri, sina haja ya kuyarudia. Kwa hiyo, ninaamini kabisa maudhui yale yatatoa fursa hata kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Mchinga waliopo Kiwawa, Mputwa, kupata fursa ya kupata maoni ya namna ambavyo wanataka Katiba hiyo iwe. Kwa hiyo, ninawatoa hofu wapiga kura wa Jimbo la Mchinga kwamba mawazo na maoni yao yatazingatiwa kwa sababu fursa hiyo itapatikana kuitia kura ya maoni itakayoendeshwa hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 6(1) zinapotajwa sifa na vigezo vya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume. Zimetajwa sifa na vigezo vingi. Lakini kifungu kile cha 6(3)(e) kinasema: "Rais kuteua kwa kigezo anachoona yeze kinafaa."

Mimi nadhani kwa kuwa tumejikita pia kuangalia na kuondoa baadhi ya mambo ambayo yanapeleke watu wengine kuamini kwamba Rais ana mamlaka makubwa, sioni haja ya kifungu hiki kuendelea kuwepo kwa sababu kama sifa za msingi zimetajwa. Mheshimiwa Rais atafuata sifa hizo kuteua Wajumbe wa Tume hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo hiyo ya 6(4); "mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe endapo: (a) akiwa ni Mbunge, Mwakilishi, Diwani au Kiongozi wa Chama cha Siasa, mtumishi katika vyombo vya usalama, mtumishi ambaye amewahi kuhukumiwa au ana kesi Mahakmani." (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono kifungu hiki. Ninaunga mkono kifungu hiki kwa sababu sisi Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wawakilishi tutapata fursa ya kujadili mchakato huu vizuri kupitia Bunge la Katiba ambalo linatajwa kwenye Muswada huu, na kwa kufanya hivi pia tunaondoa dhana kwamba sisi wanasiwa tunataka kuhodhi mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kufanya hivi pia tunaondoa dhana kwamba sisi wanasiwa tunataka kuhodhi mchakato huu, na ipo dhana kwamba endapo tutajihusisha moja kwa moja maana yake tutakuwa hatutoi uhuru kwa watu wengine kuweza kushiriki. Kwa hivyo Tume hiyo nadhani isiwashirikishe wanasiwa hao kwa sababu tunayo sehemu ambapo tunaweza kujadili taarifa au ripoti itakayoletwa na Tume. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu ukisoma ripoti ya Tundu Lissu, Kiongozi na Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria na ninaomba kunukuu ukurasa wa kumi anasema; "Ni matusi kwa watu waliochaguliwa na wananchi kuwa Wabunge, Wawakilishi au Madiwani au viongozi wa Vyama vya Siasa viliviyopendekeza watu hao, kuwekwa pamoja na wahalifu na kutamka kuwa hawana sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya mabadiliko ya Katiba," yeze anasema ni matusi. Maneno haya ni makali sana, nadhani busara hapa haikutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia taarifa hiyo inaendelea inasema na ninaomba pia kunukuu: "inaelekea lengo kuu la pendekezo hili yaani kuwaondoa Wabunge, Madiwani kwenye hiyo Tume ni kuhakikisha kwamba Vyama vya Upinzani hasa CHADEMA, chenye ushawishi mkubwa ndani na nje ya Bunge havipati fursa ya kuamua muundo na maudhui ya Katiba mpya, pili lengo kuu vilevile ni kuhakikisha kuwa Rais na chama chake cha CCM wanadhibiti mchakato wa Katiba mpya katika hatua muhimu ya uundwaji wake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya siyo sahihi hata kidogo, lakini pia hawa wanaosema mamlaka ya Rais ipunguzwe wanayahamishia mamlaka haya kwa Wabunge, kwa hivyo ninadhani jambo hili siyo sahihi hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika kifungu hicho kwa kusema kwamba upo msemo wa Kiswahili unaosema anayedai heshima kwa nguvu ananunua dharau kwa bei rahisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeleo niliyoyasema yanaonesha kabisa wenzetu hawa wanadai heshima kwa nguvu kwa kudhani kuwa wana ushawishi mkubwa ndani na nje ya Bunge, jambo ambalo mimi siliamini kwa sababu sisi Wabunge ndani ya Bunge hili tumepewa ridhaa na wananchi na ndani ya Bunge hili tupo Wabunge zaidi ya 300, Chama cha CCM kina Wabunge zaidi ya 200 wao wanaodhani wana ushawishi mkubwa ndani na nje ya Bunge hili kwa kuwa na Wabunge 48 wanatoa wapi hiyo jeuri? Jambo hili siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie Kifungu cha 20 Mheshimiwa Fakharia pia amekisema kifungu hiki vizuri sana, kwamba Wajumbe wanaotajwa wengine kwa nyadhifa zao kama Waziri wa Sheria na Mwanasheria, wao pia ni Wajumbe kwa sababu ni Wabunge, kwa hivyo sioni haja ya kuwatamka Wajumbe wenye nyadhifa mbalimbali kwa sababu kama ni Waziri ni Mbunge

ataingia kwenye kipengele cha Ubunge kwa nini turudie tena, kwa hiyo nadhani kifungu hiki cha 20 ama kifutwe au tupewe ufanuzi ni kwa nini kinaendelea kuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kifungu cha 20(2) kinaainisha wale Wajumbe 116 kwamba watashirikishwa watu kutoka taasisi mbalimbali, Mashirika ya Dini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali lakini nilikuwa ninaomba tuongeze wadau muhimu kwa mfano *Tanganyika Law Society*, Chama cha Majaji Wastaafu, Chama cha Mawakili hawa ni watu wenye uzoefu mkubwa na nadhani wakitamkwa katika kipengele cha 20(2) kwamba ni miongoni mwa makundi muhimu ya kuyashirikisha linaweza kutusaidia kupata uzoefu wao na kutuwezesha kwenda vizuri katika mchakato huu wa kupata Katiba mpya itakayotusaidia sisi Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 19 ukisoma kuanzia Ibara ya 19(1)(2) kuhusu makosa na adhabu, kifungu hiki kinasema kwamba yeoyote yule ambaye atakwaza utendaji wa Tume au Sekretariati au Mjumbe atakabiliwa na adhabu kali ambayo ni faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungu kisichozidi miezi 12, nadhani adhabu hii ni kali sana, faini shilingi milioni tano nadhani kipengele hiki kiangaliwe tena ili kiweze kurekeblishwa. (*Makof*)

Kifungu cha 30 kinaonesha haki za watu watakaoshiriki kupiga kura na tuna refer zaidi kwenye daftari la kudumu la wapiga kura. Lakini madaftari haya yamechakaa na wakati mwingine orodha kubwa ya wananchi weny sifa za kuwa wapiga kura hawamo. Kwa hiyo, ninatoa wito kwamba aidha, madaftari yale yaboreshwe ili kuwaruhusu Watanzania weny sifa ya kuwa wapiga kura kuingia katika daftari hilo na waweze kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kupiga kura za maoni, na lile daftari la wakazi kule Zanzibar pia liboreshwe ili wale amba wana sifa za kuwa wapiga kura waingie daftarini na waweze kupata haki yao ya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti nimalizie kwa kusema kuna watu wanajiita Jukwaa la Katiba, sifahamu wanatokea wapi, lakini kwa kuwa ni Watanzania na wametoa mawazo yao na mawazo yao ninayo haya ninadhani nitamkabidhi Katibu wa Bunge ili mawazo yao yaweze kujumuishwa, yale yanayoonekana yanafaa na kwa kiwango kikubwa maoni yao nimeona yamepitiva na Serikali imeyazingatia, sasa wanaposema, maana waliwahi kutoa tamko wanasema ninanukuu Jukwaa la Katiba: "Tanzania tupo mbioni kuunda na kutangaza jopo la watalaam wa masuala ya Katiba ambalo litakuwa na kazi ya kulishauri Taifa kuhusu mchakato huu, kuanzia sasa mpaka tutakapopata Katiba mpya. Hivi hili Jukwaa la Katiba linapata wapi mamlaka ya mambo haya, Serikali haipo? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya yote waliwahi kusema kupitia vyombo vya habari kwamba eti Wabunge sisi ni wachache na wao wako wengi tukipitisha Muswada huu wao watahakikisha...

(*Hapa kengele illia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtanda ni kengele yako kumbe ya pili.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtanda hujatuambia kama umeunga mkono hii hoja ama la! Kwa kumbukumbu nzuri za *Hansard*.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa manufaa ya Watanzania ninaunga mkono hoja hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, nilisema baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mtanda tutamsikiliza Mheshimiwa Chenge na baada ya Mheshimiwa Chenge tutamsikiliza Mheshimiwa Injinji Stella Manyanya, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na baada ya hapo Mheshimiwa Ali Juma Haji kama muda utaturuhusu. (*Makof*)

MHE. ANDREW J. CHENG: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi napenda nikushukuru kwa kunitambua. Na niseme moja

kwa moja kwamba naunga mkono Muswada huu, ni Muswada muhimu sana ni Muswada wa kihistoria kwa nchi yetu. Na kama walivyo sema Waheshimiwa Wabunge walotangulia Muswada huu siyo wa kutunga Katiba, Muswada huu unajenga barabara, unajenga miundombinu ambamo wananchi wa Tanzania watapita ili kuelekea katika kuitafuta Katiba wanayoitaka ya nchi yao. Kwa hiyo huo upotoshaji ambao umekuwa uklendelea kwa kipindi ni vizuri tukauweka sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Nikiangalia tangu tulipoanza mwezi wa nne, tukubali Serikali imefanya kazi kubwa, naipongeza sana, imekuwa sikivu, imechukua maoni mengi sana yaliyotolewa na wananchi na wadau mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Wale wanaobezza hata nyumbani jamani, hata ukifanya mengine mazuri namna gani wapo wale ambao hawasemi hata ahsante. Mimi nasema Serikali ahsanteni sana. Tumeanza vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliogopa sana kipindi kile Muswada huu ulipoletwa kwa hati ya dharura, nilikuwa ni mionganini mwa Wabunge ambao nilisema hapana tutakuwa tunaanza vibaya na kweli Serikali illisikia hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kidogo kwenye Muswada halafu nitasema mengine. Kwenye Muswada mimi bado nasema eneo la Mabaraza ya Katiba Kifungu cha 16, Kifungu cha 17, mpaka Kifungu cha 18 naomba tukiandike vizuri. Kilivokaa sasa hivi ukisoma Kifungu cha 16(8) halafu uende kwenye kifungu cha 18 huoni huo muingilio wa Mabaraza haya kufanya kazi ya ushauri na kwenye Kamati suala hili tulilisema sana na hapa niseme nimshukuru Spika kwa kutambua uzoefu wangu na kunteua kwenda kuimarisha nguvu katika Kamati ya Katiba na Sheria. Tumefanya kazi nzuri kwa takribani wiki tatu na nusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mtuamini na matokeo yake ni *hii schedule of amendment* ambayo imekuwa ambayo ina maoni mazuri sana, Serikali imeendelea kutusikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kile kifungu cha 24(2), kimesemwa na baadhi ya wachangiaji hapa, mimi naomba tutambue kwamba Bunge Maalum nikipata muda nitaeleza kidogo. Bunge Maalum ni chombo tofauti sana, linapotunga Katiba ya nchi kipindi hicho lenyewe ndiyo linakuwa lipo juu ya Katiba. Linaweka matarajio ya wananchi kupitia Katiba ambayo inakuja. Hivyo huwezi ukaliwekea masharti, ufanye hili na usifanye hili, naseme hili tuliangalie kwa makini na ndiyo maana baadhi ya Wabunge wamelliona hilo, hivyo ni vizuri Serikali isikilize. Naomba sana tuliangalie eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kweli ripoti ya Tume ni lazima iende kwenye mamlaka ambayo imeiteua. Huwezi ukateua Tume halafu kesho asubuhi unasilika wameshatoa ripoti yao mitaani. Haiendi hivyo katika uongozi wa nchi.

Kwa hiyo, ripoti itawasilishwa kwa Rais kama Muswada unavyoshauri. Lakini mimi nilikuwa na ombi. Ingependeza tuwe na kifungu ambacho kinasema nodani ya siku tuseme saba au 14 baada ya Rais kupokea ripoti hiyo basi yeye aitoe kwa wananchi na wananchi waanze kuijengea mazingira na kuiandalia ripoti hii mazingira mazuri. Wale ambao wanadhani kwamba eti itachakachuliwa, hapo ndiyo uwazi unapotaka uone, kwamba wananchi walitoa maoni yao katika majukwaa yao katika vikao vyao, je, Tume imezingatia kiasi gani? Haya mimi nilikuwa najaribu kushauri tuone uwezekano wa kuiboresha hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika eneo hili ambalo lipo katika maeneo tunapoenda katika kura ya maoni, napenda kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano tufikirie uwezekano wa kutunga sheria ya kura ya maoni kwa upande wa Tanzania Bara kwa suala hili, kuliko kusema kwamba tutaenda kutumia Sheria ya Uchaguzi na ile Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tukifanya hivyo tutakuwa tutaenda vizuri na kile ambacho wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tayari wameshafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme jambo moja ambalo mimi linanisumbua sana, nimeliona tangu Jumapili wakati tunaanza kesho yake mjadala huu. *Public hearing* zilianzishwa mwaka 1993 kwa nia njema sana. Lakini sasa zinaanza kuonekana dalili hasa kupitia tuliyoyaona kwenye Muswada huu. Mimi ni mionganoni mwa wengi wanaothamini sana mchango wa kila mtu, maana tungekuwa na mawazo yanayofanana dunia hii ingekuwa ya hovyo sana, lakini naheshimu mawazo hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja ambalo mimi nasema Bunge lako ni lazima liendelee kukataa ni mtindo huu ambaa unaanza kujitokeza sasa kwamba kuna kikundi cha watu tena nyuso ni zile zile, maeneo ni yale yale, utawakuta wanaanza kuongea vitu ambavyo ni vya ajabu kidogo na wanataka kushinikiza kwamba yale waliyonayo vichwani mwao sasa ni lazima yaingie kwenye Muswada wa Serikali, Muswada wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge litakubali suala hili tutakuwa sasa tunaanza kuruhusu mtindo na utaratibu ambaa haukulaliki. Na lazima niseme kabisa wale wenzetu ambaa wana mawazo kama hayo wanaamini kwamba wao wamejiaminisha kwamba yale ya kwao waliyonayo ni sauti pekee ambayo lazima iaminwi na Watanzania waliozaidi ya shilingi milioni 40, mimi nawashauri na kuwasihii sana kwamba wafanye tafakari ya kina kuhusiana na msimamo wao huo potofu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha uwakilishi halali wa wananchi ni lazima kiruhusiwe kufanya kazi yake. Muswada huu ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu. Tangu mwezi wa nne nafasi imetolewa kwa watu kutoa maoni yao, wenyewe mapenzi mema na nchi yao wamefanya hivyo, yale mazuri kama nilivyosema Serikali imeyachukua, lakini pamoja na kuheshimu maoni ya wananchi na umuhimu wa Muswada huu na nafasi ya wananchi ambayo ni muhimu sana kwa safari tunayopianza ni lazima mjadala huu kwa Muswada huu ufikie mwisho. Na mimi ninawaomba Watanzania wote haya tunayoyafanya ni mazuri kwa sababu ndiyo yatatupatia nguvu ya kwenda kule tunapotaka kwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa haraka sana, kwa haya Kanuni inasemaje; Muswada umesomwa kwa mara ya kwanza na Kanuni zipo wazi kabisa hasa utaurejeshaje hapa uusome kwa mara ya kwanza, ni kichekesho tu. Ukiwasikia hawa watu unasema ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umekuwa kwenye Kamati kipindi chote tangu uliposomwa kwa mara ya kwanza na tumeshiriki kule, tumeuboresha mpaka umekuwa katika sura hii, sasa ukisema kama nilivyomsikia msomi mwenzangu anasema kitu cha namna hii, cha kupotosha wananchi mimi nasema haikubaliki hapana, hapana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinawezekana kufanya ambacho naishauri Serikali katika hatua hii wasifanye ni kupitia Kanuni ya 90 ya kuondoa Muswada ili tuondoke, Serikali iutoe kabisa Muswada tukaanze upya, itakuwa kama tunapoteza muda. Wananchi sasa hivi wana hamu ya kwenda mbele na ninaishauri Serikali twende mbele, kaza buti, twende mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 98 cha Katiba wale wanaosema kwamba tulipaswa kurekebisha Katiba kwanza, nasema kabla ya kuanza mchakato huu ni vizuri tu tukaelewana kwamba wanapotosha ukweli wa *Constitutional theory* ya kutunga Katiba.

Mamlaka ya kutunga Katiba mpya siyo mamlaka ya Bunge liliopo na ndiyo maana tunasema hivi, Katiba unaanza kusema Katiba ilizaliwa na wananchi wenyewe mamlaka na nchi yao kupitia Bunge Maalum kama inavyopendekezwa. Bunge kama *creature*, mtoto wa Katiba haliwezekani likaifuta Katiba hiyo. Linachowea kufanya ni kufanya marekebiso tu. Wanaosema kwamba tungekuja kurekebisha, haiwezekani, hiyo kazi ndiyo itaenda kufanywa na Bunge Maalum la Katiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naheshimu sana mawazo tofauti, lakini sitaki kurudia, someni ukurasa wa tano na wa sita wa mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusiana na Tume ya Vyama vya Siasa ambayo baada ya Rais, ndugu zangu Katiba ya Jamhuri ya Muungano

ipo na itaendelea kuwepo mpaka tupate Katiba Mpya. Rais wa Jamhuri ni Kiongozi Mkuu wa Nchi hii, ni Rais Mtendaji na pia Amiri Jeshi Mkuu. Lazima tutambue nafasi ile ya kwanza ya Mkuu wa Nchi ndio kielelezo chetu kama Taifa. Sasa unaposema angalieni kama wao kuna uwakilishi wa Vyama mbalimbali humu ndani ya Bunge, wameshindwa kuingiza kwenye Kambi Rasmi Vyama vingine vyta Upinzani sembuse kwenda kuka kule na kusema kwamba eti watashirikiana. Hawa wanataka kuchelewesha mchakato wa kwenda mbele. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni sana tuupitishe Muswada huu, ni kwa faida ya Taifa letu na ni kwa faida ya nchi hii. Lakini nataka kutoa tahadhari kidogo kwa hawa amba owanajaribu kuchafuachafua hali ya hewa, tuwazue na tunachowea kuwazuia ni kuhakikisha kwamba Muswada huu tunakwenda tarehe Moja, tusimamie tuhakikishe kwamba unaanza kufanya kazi, vyombo vile vinavyotakiwa vipatikane. Tutafute viongozi, naishauri Serikali itafute kwa utaratibu mzuri wajumbe amba o wakitangaza tu majina na nchi itasema ndio tunaanza vizuri kwenye safari yetu. Mwishoni kabisa tupate Katiba ambayo itakuwa ni *National Heritage* yetu, urithi wa Taifa kwa faida ya Taifa hili, kwa faida yetu sisi wenyewe, kwa faida ya watoto wetu na kwa faida ya watoto wa watoto wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema tumefanya kazi ya kutosha sana katika Muswada huu. Ukiniona nimesimama kwa kitu hiki naomba mtambue kidogo mchango wangu. Nilikuwa mkali sana ulipotoka mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ubarikiwe sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli hata mimi Mwenyekiti nitambue mchango wa Mheshimiwa Chenge. Tunakushukuru kwa mchango wako mzuri. Tunakushukuru kwa utumishi wako ndani ya Serikali yetu katika eneo hilo la sheria. Waheshimiwa Wabunge, naomba mniruhusu nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi hiki cha leo cha asubuhi ambaye ni Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*. Karibu Mheshimiwa Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia huu Muswada amba o ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu. Kwa nafasi hii ya kwanza kuchangia, naomba nimshukuru sana Rais kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi kwenye *site* kwenye hali halisi na mazingira ya Watanzania. Naamini kama mwanamke nafasi hiyo nitaitumia kikamilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mizuri na ni muhimu sana. Labda tu nirudie kusema kwamba, suala la Katiba ambayo ni Sheria Mama ni muhimu sana katika nchi yejote ile. Kwa misingi hiyo ningetamani sana kuona kwamba hakuna mtu wala kikundi cha watu kilichojojewa au kuwekwa na vyombo visivyo rasmi kuwa chenyewe ndio kinahodhi mustakabali wa Katiba au mawazo au mawazo ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nimepangiwa ile *site* ya kule Rukwa na Mkoa Mpya tarajiwa wa Katavi huwa nastuka sana ninapoona mtu anasimama na kusema Watanzania wengi hawataki hili, wakati nikiwa kule sijawahi kuwaona wakipita kuzungumzia suala hilo. Naogopa sana, huwa nasema hizo nguvu wanazipata wapi, nashindwa kuelewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi pia ni Mbunge katika Bunge la *SADC*, naomba nitoe uzoefu wangu nilioupata wakati nasimamia uchaguzi Zambia. Kule kulikuwa na mambo hayo hayo wakati wa uchaguzi. Kulikuwa na jambo zito karibu kila redio, *TV*, hasa zile *private* na Vyama vyta Upinzani, vikilalamikiwa juu ya uteuzi wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu inateuliwa na Mheshimiwa Rais, wakasema Tume hii haitaweza kutenda haki kwa sababu inateuliwa na Mheshimiwa Rais, pamoja na taratibu zote ambazo zinahusika katika kumshauri Mheshimiwa Rais. Hayo ndio ninayoyaona hapa tena.

Ndugu zangu mimi najiuliza, hivi tunapomuangalia Mheshimiwa Rais tunamfananisha na nini kiasi cha watu hadharani kwa sauti kumuita vyovyote wanavyojisikia mtu kumuita bila kujua kwamba yeje ni chombo kikuu katika nchi. Kwa nini tunaamua kutokuwa na adabu tena juu yetu sisi wenyewe kwa mambo tuliojipangia wenyewe? Kwa nini tumefikia ile hali ya kutokuaminiana

kwa kiasi hicho? Kwa nini wachache wameamua kuchukua jukumu wao ndio Taifa na ndio wanaaminika na siyo wengine? Kwa nini *NGOs* ambazo tunaamini zipo kwa ajili ya wananchi zikaamua kusimama upande mmoja zikaacha upande mwengine? Hayo mambo huwa najiuliza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Tume ile imezungumzwa vile sisi tulibahatika kuongea na yule mama Mwenyekiti wa Tume akasema look *I am a Judge, I can't abuse my position.* Mimi ni Jaji, tena mzoefu, siwezi kutumia vibaya madaraka niliyopewa na kuaminiwa, alisema mama yule. Kweli ameendesha uchaguzi vizuri mpaka mwisho na wenyewe ikawashangaza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilikuwa ni juu ya mabadiliko ya Katiba yao, kulikuwa na mambo ya kuangalia namna ya kuweza kupata wanawake wengi zaidi katika nchi kuwa wawakilishi. Lakini pia mambo mengi mazuri ambayo walijatarajia yawe kwenye Katiba, lakini kulikuwa na ubishi mkubwa uliokuwa unasema kwamba mshindi lazima ashinde kwa kura kwa asilimia 50 na kiasi cha ziada. Kwa hiyo, ile iligombewa sana badala ya kwamba kushinda kwa *simple majority*, yaani anayeshinda zaidi ndio apewe. Vyama vyta Upinzani vilikataa kabisa vikaamua hata kutokupitisha ule Muswada na wakabaki wanakwenda kwenye uchaguzi bila Muswada. Wanawake umewatia hasara kwa sababu sheria ambazo zingewasaidia zimeshindwa kupatikana. Baada ya kutangaza matokeo, mshindi ameshinda kwa *simple majority* na amepewa, Mheshimiwa Rais tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu ni kwamba, kama ingetokea hali ile imejitokeza kwa Rais aliyejikuwa madarakani pengine yangetokea maandamano. Lakini kwa sababu upande wa pili umechukua na amani ikapatikana hapo. Lakini kwa nafasi hii pia nimpongeze sana Rais ambaye alikuwa madarakani kwa kuridhia kwa moyo mzuri kwamba wenzangu wameshinda wachukue nafasi yao. Haya ndio tunayoyataka Tanzania. Tunahitaji kupata maamuzi yenyetija yanayoweza kutambulisha Watanzania kuwa ni watu wenyewe amani kama ambavyo tulijilea siku zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye hizi *NGOs*, niko kule Rukwa, kuna matatizo mengi tu yanayokabili jamii zetu ambazo naamini kabisa *NGOs* zetu ziliikuwa ndio zina mchango mkubwa katika kuangalia masuala hayo. Lakini zote zimeamua kujikita katika masuala ya *politics* au UKIMWI basi. Ukiijuliza kwa nini hujui. Wakipewa nenda kafanye tafiti, watasema unajua mtumishi huyu hafanyi vizuri, unajua hawa akinamama wanakuwa kwenye vifo. Lakini hawaendi ndani. Kwa mfano, nichukulle kitu kidogo kwa upande wa wenzetu ambaao wanatusaidia *development partners* wetu na naomba hili nilitamke bila woga kwamba, masuala mengine yanayosababisha umaskini kwenye nchi yetu siyo ya kwetu na ya kujitakia, yanatokana pia na hali ya mabadiliko huko nje ya nchi yetu kwa mfano, mafuta tulikuwa tunapata kwa bei nafuu kutoka nchi za mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi maeneo haya yamekuwa na vita vyta hapa na pale, kung'oana kwa watawala kwa hapa na pale, matokeo yake bei ya mafuta imekuwa ikiongezeka kila siku. Leo bidhaa zinapanda bei, hali hiyo je, ni ya kuilaumu Tanzania peke yake? Mbona hatujapata mchango wa *NGOs* zikinyoosha vidole huku nje jamani mnatuua, zimenyamaza, kwa nini na wanashirikiana nao mara kwa mara. Kwa nini *NGOs* haziwezi kuona jambo kwa mapana? Kwa sisi Wahandisi huwa hatumpi mtu tick kwa ajili ya jibu la mwisho, tunaanzia njia nzima umefikia vipi hilo jibu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, katika mchango wangu wa hapa na naongea katika misingi ya hali halisi ya wananchi wetu, nazidi kusisitiza kikundi cha watu kisitumike kujitaa ni Watanzania. Watanzania kama Watanzania wapewe haki yao kama wao. Vijana wetu wasitumike kwa kazi ambazo hazina manufaa kwao. Tunaangamiza Taifa, mtu anapoongea anasema, nitakwenda kuandaa maandamano na vijana watanifuata ina maana hilo ni shinikizo. Mtu anaposema kwamba yeche atahakikisha hili haliwezekani kama ni vurugu na ziwe, ina maana ni kuwanyima haki Watanzania. Je, katika Muswada wetu huu kuna kifungu kinachonilinda mimi Manyanya au mama yangu kule kijijini kuwa huru katika maamuzi ya kuchangia wakati wa Katiba itakapokuwa inatayarishwa. Vipo vifungu hivyo, maana nikiangalia kifungu cha 19 kinazungumzia adhabu kwa mtu atakayezuia Tume kutekeleza majukumu yake.

Lakini sioni mwananchi huyu wa kawaida analindwa vipi anapolazimishwa kujunga kwenye maandamano, anapolazimishwa asichangie kwa uhuru. Ninyi mnaona mijadala ambayo imekuwa ikijitokeza hivi karibuni na kwa kweli kwa heshima kubwa kabisa *TV* zetu ikiwemo ya *ITV* imekuwa na mchango mkubwa sana katika kuelimisha wananchi. Lakini sasa hivi watu wanataka kumchonganisha Mheshimiwa Mkoo wa *TV* ile na wananchi kwa sababu wanapeleka *programs* ambazo *purely* ni za uchonganishi. Hali kama hiyo nadhani lazima iangaliwe kwa uzuri, kwa nini mtu amejitao miaka yote ya maisha yake kuona kwamba Watanzania wanapata kitu cha kuwaelimisha cha thamani, leo kinatumika kwa ajili ya kuwachonganisha Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tumtetee Mheshimiwa Mzee Mengi, kwa nguvu zote, wanaopeleka hizo *programs* lazima waziangalie kwa nini wanapeleka *programs* za kutuchonganisha? Kwa hiyo, nasema kwamba, lazima kuwe na utaratibu maalum ambaa ndio utakaoratibu taarifa zinapotolewa, lakini pia hata namna ya utoaji wa taarifa tutapiga hizo kura za maoni. Lakini kabla majibu hayajajitokeza mtu ameshaanza kutangaza. Unajua kuna hili kuna hili. Tunadhibiti vipi? Wanasheria, mimi kazi yangu ni kusema yale ambayo nayaona ni tatizo. Mpeku Muswada huu ninyi mliosomea sheria mseme hivi vifungu vipo? Mimi sivioni vya kutulinda sisi wananchi wa kawaida, kwa sababu tusiwe tunagombana tu inapofikia jambo fulani la msingi, mengine tutayakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile nilimwangalia sana ndugu yangu mmojawapo aliyejewa anachangia, nisingependa kumtaja. Lakini nakumbuka katika Bunge hili siyo mara moja kumetangazwa kwa mfano wanawake jasiri Mheshimiwa Dada yangu mama Kilango alipata, Mheshimiwa Dada yangu Ananilea alipata, lakini sisi wanawake hatkuulizwa. Tungeulizwa labda tungenesema na mimi nipeleke kuwa mwanamke jasiri. Lakini tulitegemea kwamba wale wachache waliofanya ile kazi wamefanya vizuri. Sasa leo inakuaje unamuona Mbunge yuko humu ndani unamuona kama yeche siyo mwakilishi wakati Katiba ndiyo iliyomfikisha kuwa mwakilishi wa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuaje tuna-cross majukumu yetu? Nimeona niyaseme haya kwa dhati na nikiwa kama Mkoo wa Mkoa wa Rukwa lakini mwakilishi kutoka Mkoa wa Ruvuma ninasema nitawakaribisha wote watakaokuja kufanya kazi kwa nia njema katika Mkoa wangu. Lakini sitawavumilia wale watakaokusudia kuwasumbua wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana hata wahisani wetu akinamama wanakufa, nimetembelea mara ya mwisho katika hospitali zangu mpaka kufikia mwezi wa 10 hela za *basket fund* ziliikuwa hajifika. Nikataku kujua ni kwa nini, ni kwa sababu Serikali yetu imechelewesha kupeleka au ni kwa nini. Kwa hiyo, niombe rai kwa sababu mwaka 2015 wa malengo ya *Millenium* mwisho wake hauko mbali, tunahitaji kufikia malengo yetu, tunaomba hizo hela wanazosaidia ziende kwa wale wananchi zikatature matatizo yao kuliko watu wachache kupewa na wao kuzitumia hizo katika kutuchonganisha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani nao, tunawapenda na tunaamini wataendelea kutusaidia chanya kwa faida yetu sote. Kwa sababu kama ni madini haya yanayolalamikiwa hizo sera tunapotunga hatutungi sisi peke yetu, mara nydingi tunapata *consultation* kutoka kwao. Hatuna haki ya kulaumiwa peke yetu. Tunaomba nchi hii ikiwa na amani ni kwa faida ya wote ikiwa na matatizo ni shida ya wote. Tunaomba tusaidiwe Watanzania tufikie Katiba yetu ambayo itatufaa na Katiba yenye ridhaa ya wananchi kwa uelewa mpana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii naunga mkono kabisa Muswada huu ambao unalenga kuweka chombo ambacho kitakuwa na meno katika kudhibiti mwenendo mzima wa kufikia kupata Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, nakushukuru na nazidi kuunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli ilitakiwa nitambue uwepo wa Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* kama *RC* mpya mionganini mwa *Ma-RC* wapya walio teuliwa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, naomba nikupongeze na nikutakie kila la heri katika kazi zako wewe pamoja na wanawake wengine, lakini pia na wanaume mnategemewa sana kusaidia kuleta maendeleo ya nchi kwa nyadhifa zenu kama Wakuu wa Mikoa ambao mmepewa dhamana na Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za leo asubuhi, naomba nitoe tangazo liliokuja hapa mezani kwangu. Nimeombwa na Mheshimiwa George B. Simbachawene Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa *Basements* leo tarehe 16 Novemba, 2011 kuanzia saa saba mchana huu. Wajumbe wote mnaomba kuhudhuria bila kukosa na kuzingatia muda.

Baada ya tangazo hili Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru kwa kweli kwa michango yenu mahiri kabisa ya kipindi hiki cha asubuhi. Tutakoporejea kipindi cha jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ali Juma Haji, akifutiwa na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na wengine wataendelea kufuatana na orodha kadiri ilivyo.

Baada ya kutoa tangazo hilo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa hadi Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni, Bunge lilitrudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Masele Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano yetu. Naomba kuwataja ambao tutaanza nao sasa hivi. Tutaanza na Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer ajiandae. Pia Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Mshama ajiandae. Mheshimiwa Ali juma.

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo afya njema kuweza kusimama hapa na kupata nafasi hii nami kutoa mchango wangu katika mjadala huu tunaoendelea nao wa Muswada wa kuunda Kamati au kamisheni ya kuratibu na kutafuta maoni ya Katiba yetu mpya, Mwenyezi Mungu atujalie twende nao mjadala huu na tuufikishe kwa amani kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kunipa nafasi hii kuwa mtu wa kwanza kuchangia mada hii tunayokwenda nayo. Niwapongeze kwanza wananchi wa Zanzibar kwa kuwa watulivu mara baada ya kuletwa tena Muswada huu kwa mara ya pili na kusikiliza nini kinachoendelea na wao kusubiri nini kitakachoamuliwa katika Muswada huu na katika Bunge lako hili Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia Muungano, maana wenzetu hawa hasa wa Upinzani wa Chama cha CHADEMA, labda Msemaji wao wa Kambi ya Upinzani sidhani kama hajui lakini labda alikuwa anapotosha umma makusudi. Muungano ni chombo muhimu sana kilichoundwa kutohana na nchi mbili kwa maridhiano mazuri kutohana na nchi hizi mbili zilizokuwa huru kabisa yaani ya Tanganyika na Zanzibar. Sasa kuna watu wengine tunapojadili suala kama la Muungano wao huchukulia upande ule wa Muungano kwa udogo wake, watu hawa wanajiita wasomi, lakini sijui kama Mwalimu Nyerere alipoamua kukutana na marehemu Mzee Abeid Amani Karume sidhani kama hakujua kama Zanzibar ni ndogo, lakini bado alikubali pamoja na udogo wake, tuungane kwa maslahi ya wananchi wa Tanganyika na Zanzibar ndipo tukapata Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo anapotokea mtu akaidharau Zanzibar ama kwa udogo wake au kwa anavyojiona ye ye mwenyewe tu alivyo, basi kwa kweli anakuwa haitendei haki Zanzibar na Wazanzibari huwa hatuko pamoja nae yule mpaka kiyama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaeleze wananchi wa Zanzibar na Watanzania wote kwa ujumla, leo hapa tuliposimama wachangiaji wote karibu walioipa wameshaeleza wazi wazi kwamba hatujadili Muswada wa Katiba mpya. Tunajadili Muswada wa kuunda Tume ambayo itaratibu maoni ya wananchi kufikia katika hiyo Katiba mpya, nadhani hili limeshaelezwa sana, kama ni elimu imeshatoka ya kutosha. Tunaomba wananchi wetu watuelewa vya kutosha na hata kwenye vyombo vya habari wengine nimewahi kuwasikia, walikuwa ni wananchi hawajui kwamba hapa tunajadili Muswada wa kuunda Tume. Wao wanasema wanafikiri tunajadili Muswada wa Katiba mpya. Kwa hiyo, nadhani kama sasa hivi wanaliangalia Bunge hili, basi wameshapata elimu ya kutosha kwamba tunachokijadili ni Muswada wa kuunda Tume ambayo itapita Wilaya zote, Vijiji vyote, Mikoa yote kuratibu maoni ya wananchi ili kufikia katika huo Muswada wa kuunda Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Wazanzibari tulikuwa na kilio cha muda mrefu sana kuhusu labda Mungano wetu, tunaonewa, uwe vipi, hapa sasa wananchi wa Zanzibar wajiweke tayari kwa kuja kutoa maoni yao wakati itakapokuwa imeshaundwa Tume ya kuratibu, nawasihi sana wananchi wa Zanzibar kama walivyokuwa watulivu kwa sasa hivi hakuna zogozogo lililokuwa hapo mwanzo kama wakati kulivyokuwa na matatizo katika ile rasimu ya mwanzo, lakini baada ya kurekebishiwa na makubaliano yote ya Serikali hizi mbili, tunawaomba wananchi watuamini kwamba hapa kinachoendelea sasa hivi ni suala sahihi.

Serikali yetu ya Muungano wamezingatia yale yote, karibuni yote, karibu asilimia 90 au zaidi ambayo yalikuwa ni matatizo walivyoyaona wananchi wa Zanzibar katika Muswada huu tunaoendelea nao, lakini tunawahakikishia kwamba yamezingatiwa kwa asilimia kubwa sana na sasa hivi wawe tayari kusubiri Tume ambayo itakuja kuratibu maoni yao na ndipo tutasema Muungano wetu tunautaka uwe vipi, kwa sababu wao wananchi wanautaka Muungano hadi sasa, lakini walichokisema ni kwamba, labda kuna kero za Muungano au kuna matatizo fulani kwenye Muungano. Hapa sasa ndipo tunapowasihi kwamba wakae tayari, tukishaupitisha Muswada huu Rais wetu aunde Tume na ipite, wananchi wasiwe waoga, watoe maoni yao kwa uwazi kabisa na yatachukuliwa yote na sisi tutakuwa tayari kuwasimamia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nadhani wananchi wa Zanzibar wameshatuelewa na nategemea sana kwamba, watatusikia na watakuwa tayari nao kufuata haya tunayowaelekeza kama ni Viongozi wao na wawakilishi wao wa Majimbo yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana kumuona Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu anaishambulia Zanzibar karibu asilimia 75 ya hotuba yake, hiki kitu kilinishangaza sana, pamoja na kwamba ye ye ndiyo alikuwa anatoa maoni yake, lakini mashambulizi makubwa yalikuwa katika upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano. Sasa ningewaomba wananchi wa Zanzibar, hiki chama cha CHADEMA wakiangalie vizuri sana tena vizuri sana na wakione kwamba kwa mashambulizi haya yaliyoshambuliwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, basi nawaomba wananchi wa Zanzibar, Viongozi wa Zanzibar, Wabunge wenzangu hapa tukubaliane kwa pamoja tukutane na kufanya maandamano ya amani kulaani mashambulizi haya na udhalilishaji huu wa wananchi wa Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufanye maandamano makubwa kulaani mashambulizi haya na udhalilishaji huu, wananchi wa Zanzibar tusikubali kabisa kudhalilishwa na mtu mmoja kwa niaba ya chama chake cha CHADEMA. Nina wasiwasi sana na chama hiki cha CHADEMA na namuomba Msajili wa Vyama kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Kombo na nadhani Msaidizi wa Msajili hapa tunamuona toka juzi yupo, tunampa agizo hili, waunde muundo mzuri, mfumo mzuri wa kuhakiki Vyama hivi vya Siasa kila baada ya muda waonee kweli vina wanachama pande zote mbili na vina wadhamini pande zote mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nina wasiwasi kama kuna wanachama wao kule Zanzibar na wadhamini wao, asingeshambulia Zanzibar kiasi hiki kwa sababu mwanachama ni mfalme, ni mteja wao na mteja ni mfalme. Kwa hiyo, kama mwanachama ni mteja wao na mteja ni mfalme ataishambulaje Zanzibar kiasi hiki na wanachama wale washeherekee kiasi hiki?

Tunaomba msajili, aweke mfumo mzuri wa kuhakiki vyama vyote na nina imani kubwa chama hiki sijui kama kitapata kule wanachama tena. Kitakufa na kitakuwa sio cha Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza, chama hiki cha CHADEMA, hivi karibuni Zanzibar imepata msiba mkubwa sana wa ajali ya *Spice Islander*, wakatoa ubani wao kwa Makamu wa Pili wa Rais huyu hapa, lakini walivyokuja walikuwa wanaonesha imani kwamba wanawapenda wananchi wa Zanzibar, lakini angalieni mashambulizi haya na vile walivyokuja, hata hao maiti waliokufa wakazikwa huko kaburini basi kama wanamsikia Tundu Lissu aliyoshambulia, hawako radhi na mchango wao ule na nahakikisha wangekuwa kuliko Michael Jackson wangeshafufuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Makamu wa Pili wa Rais na kuwaomba wananchi wa Zanzibar tukubaliane juu ya hili tuukatae mchango wao ule wa CHADEMA, Makamu wa Pili wa Rais, tunakuomba ukaukatae mchango wa CHADEMA kwa sababu ni wanafiki kabisa. Urudishwe kwenye chama chao hatuna haja nao, wadhalilishaji wa Zanzibari, halafu wanatuletea kutuonesha michango ile, tunakuomba Makamu wa Pili wa Rais unatusikia na hili nalisema na wenzangu, kofi hizi zinaashiria kwamba, Wabunge wenzangu wameniunga mkono. (*Makofî*)

Kwa hivyo, tunachotaka tuje tukusikie Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais unaurejesha mchango wa chama cha CHADEMA, hatuna haja nao kwa sababu hata hao maiti hawaukulali tena. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si msemaji sana, lakini haya mambo kwa kweli yanaudhi sana, sana kwa sababu sidhani jamani kuna chama hasa cha CHADEMA, sidhani, uhakiki huu ukishafanywa nasisitiza tena, kwa hiyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja, asilimia mia moja, wananchi wa Zanzibar watulie. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Kwanza ujumbe wako Mheshimiwa umefika kwa Msajili na mamlaka ulizoiomba. Sasa napenda kumwita Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Assumpter ajiandae, Mheshimiwa Peter Serukamba nae ajiandae.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada ulio mbele yetu, lakini nitangulie kusema naunga mkono Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu sana, nasema ni tofauti na Miswada mingine kwa sababu Muswada huu na Katiba tunayozungumzia ni roho ya Taifa letu. Kwa hiyo, Wabunge wenzangu wamechangia kwa nguvu sana na wamesema mengi wakitumia Kanuni ya Bunge ya kutorudia yaliyosemwa, nadhani wengine mngekosa la kusema kwa sababu mengi yamesemwa, lakini niseme tu machache; Tume hii inayoundwa na Rais ni Tume ya kuratibu namna ya kupata mjadala au mawazo ya Watanzania wote na nasema kwamba Rais anapaswa na ana haki ya kuunda hii Tume, kwa sababu hatujui Rais mwininge aliyeko Tanzania ambaye anaweza kuunda hiki chombo, hakuna mtu mwininge na Mamlaka ambayo amepewa Rais, amepewa na Katiba hii na hii Katiba ndiyo wametumia Marais wote waliomtangulia huyu aliyepo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna sababu ya kuhoji sasa madaraka ya Rais, kama tunataka kupunguza madaraka ya Rais, basi wananchi wapunguze kwenye Katiba hii ambayo inazungumzwa sasa, Katiba ijayo lakini sio kupunguza kwenye Katiba hii. Hatuwezi tukabidilisha chochote kwenye Katiba hii mpaka tubadilishe wakati wa kuunda Katiba mpya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano hapa Bungeni hatujadili Katiba mpya, tunajadili Muswada huu na ningependa kusema kwamba katika Ibara ya (5), Rais amepewa madaraka, ndiyo mwenye madaraka pamoja na Rais wa Zanzibar ya kuunda hii Tume na nadhani hiyo Tume

itakayoundwa, itafuata utaratibu wote utakaopewa au hadidu za rejea watakazopewa na Rais, kwa hiyo mtu akisema kwamba hatutaki Rais atoe utaratibu wa kufuatwa, sijui sasa tutampa nani utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia Ibara ya (7), Muundo wa Tume. Tume itakuwa na Mwenyekiti, itakuwa na Makamu Mwenyekiti, itakuwa na Makamishna wasiopungua au wasiozidi 30. Sasa hapa ndiyo naona hawa tu ni wachache, ukilinganisha na jiografia ya nchi yetu, naona hawa watu ni wachache kwa sababu imeandikwa wasiozidi, inawezekana wakawa 15 au inawezekana wakawa 20, kwa hiyo hapa kwenye hiki kifungu itazamwe upya ili wapatikane watu ambao wanaweza wakafanya jambo hili kwa ufanisi na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyininge ambayo ningependa kuzungumzia, chombo hiki tunachokiunda, hatuzungumzii Katiba ya chama chochote, Katiba hii inayotafutwa sio Katiba ya Chama cha Mapinduzi, wala ya *TLP*, wala ya CHADEMA, ni Katiba ya Taifa, kama ilivyo Katiba hii ya sasa tunayoitumia. Inawezekana 2015 akakabidhiwa Rais anayetoka chama chochote, kwa hiyo inawezekana Rais akatoka *TLP*, *CUF* au CHADEMA au CCM kama ilivyokabidhiwa katika miaka yote iliyopita. Kwa hiyo, tushojoj sana kwamba hii Katiba ni ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo inayounda na naomba chombo hiki kikiundwa kiwe ni chombo hiki tu, ndiyo kinafanya kazi kusiwe na watu wengine pemberi ambao wanazunguka, hakuna cha wanaharakati, hakuna cha nani, ni chombo hiki kimoja tu ndiyo kifanye kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuzungumzia ibara ya (9), kazi ya Tume, kuna mambo yaliyotajwa ambayo ni muhimu na ya kuzingatiwa, kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hilo ni jambo muhimu la kuzingatia. Kuwepo na Serikali, Bunge, Mahakama, hapo ndiyo nataka kuzungumzia kidogo, Serikali tunajua kwamba itakuwa moja itakayoongozwa na chama chochote kile. Bunge litakuwa ni Bunge kama hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika Mahakama. Tunafahamu kwamba nchi yetu Mahakama ni moja. Tukianza kuanzisha Mahakama nyininge za dini, kila dhehebu watataka Mahakama yao. Hata sisi jamii ya Kimasai tulikuwa na utaratibu wetu, tunaweza kusema hata hiyo ni Mahakama kwa sababu tumejitungia sheria. Tulikuwa na Sheria zamani. Kwa hiyo naomba kusiwe na Mahakama nyininge itakayoundwa tofauti na Mahakama tuliyonayo. Ikiundwa Mahakama nyininge yoyote kuwekwa kwenye Katiba ni vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ibara ya 16. Ibara ya 16 nayo inazungumzia kazi ya Tume. Wanapokwenda Wilayani kule, kuitisha vikao kuna DC, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Mtendaji wa Kijiji, hapo ndiyo wasiiasi wangu, sijui kama wananchi wataitishwa vizuri kwa sababu mara nydingi tarehe zinapotoshwa, wananchi wanakosa tarehe sahihi za mukutano, wananchi hawapati taarifa mapema. Hilo ndiyo nataka lifahamike haraka sana, kila kijiji wajue ratiba kwamba sisi tunatembelewa na Tume lini ili waende wakatoe maoni. Wamasai wenzangu hawajawahi hata siku moja kushiriki katika uundaji wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mambo mengi ambayo ni ya unyanyasaji ambayo yapo katika nchi hii. Sisi tunataka kuweka kwenye Katiba ijlilikane. Sisi hatuko pemberi mwa Tanzania na sisi ni Watanzania tunataka tushiriki kabisa kwenye muundo wa Katiba. Kwa hiyo, tunataka kabisa hata kama ni kwenda mpaka Gilai, mpaka kule Lake Natron, mpaka Wosiwas. Ni lazima hiyo Tume iende, wananchi watoe maoni yao. Msizungushe mijini tu, halafu tunaambiwa kwamba, tayari Tume imekwishaundwa. Tunataka tushiriki kikamilifu katika Katiba hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wasukuma wametawanyika Tanzania nzima, lakini kule waliko Katiba hii iwafuate ili nao watoe maoni. Kwa vile wenzangu wamesema mengi, naomba tu niseme kwamba, kwa kweli Katiba hii siyo ya kisiasa, hatuko hapa katika jukwaa la siasa. Naomba Wabunge wenzangu pamoja na wananchi kwa suala la Katiba siasa tuiweke pemberi kwa sababu Katiba siyo ya chama chochote. Vyama vingine wanaweza wakaja wakaongoza, wakaongoza nchi wakitumia Katiba hii tunayounda. Kwa hiyo, nawaomba tuache siasa, wakati wa siasa upo, lakini kwa sasa tuunde Katiba ambayo itaweza kuongoza nchi yetu bila kuwa na vurugu. Tuwe na amani kama tulivyokuwa na amani miaka mingine iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninayo heshima kubwa kusimama mbele za Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu na mbele zako mwenyewe kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Muswada mkubwa uliopo mbele yetu.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi mkubwa wa ujasiri wa kuona ni wakati mzuri sasa tunapotimiza miaka 50, twende na kitu kipyä katika miaka 51 na 52 kuendelea. Jambo lingine ambalo napenda kuipongeza Kamati pamoja na Waziri mhusika kwa kazi kubwa waliyoifanya usiku na mchana kuhakikisha Muswada huu unaletwa mbele yetu na tunaujadili kwa usalama. Labda nianze tu unipatie nafasi na ukubali ninukuu mtu anapokuwa anaongea habari ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Uksoma katika Katiba hii ukurasa wa 213, utakuta maelezo ya Tanzania Bara maana yake nini? Maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani liliikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda maana ya Tanzania Zanzibar, ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani liliikuwa eneo la Jamhuri ya watu wa Zanzibar na ambalo kabla ya Sheria ambayo ni hii Katiba nilyoshika, kutungwa iliiwt Tanzania Visiwani. Sasa labda niongelee pia kwa nini watu wanaendelea kuongelea kitu kinachoitwa Zanzibar na kinachoitwa Bara. Mimi nadhani ni bora hata wote wawili tuelewe kwamba sasa hivi Tanzania Bara hakuna jambo la Tanganyika tena. Kuna Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Sasa hii habari ya kukaa tunakereketwa, tunakereketwa, tunakereketwa tunaongea Zanzibar, Tanzania, aaah! Wote tunaitwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo, nadhani kwa Watanzania wote limeeleweka. Wote kila mmoja aliacha jina lake, tukaungana, tukatengeneza jina moja.

Labda niongee tena, mtu anapothubutu kumwongelea Rais, maana ya Rais ni nini? Naomba unikubalie ninukuu tena, katika ukurasa wa 214 katika ile ibara ya 151, kifungu cha pili, kinasema: "Kanuni zifuatazo zitatumika kwa madhumuni ya ufanuzi wa masharti ya Katiba yaani kila yanapotajwa madaraka ya Rais ifahamike kuwa madaraka yanayohusika ni pamoja na mamlaka ya kutekeleza shughuli na kazi mbalimbali na vile vile wajibu wa kutekeleza shughuli na kazi mbalimbali kama Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia mamlaka mengine kama hayo au wajibu mwngine kama huo ikiwa imeelezwa katika Katiba hii au katika sheria nydingine yoyote kwamba mamlaka hayo mengine ni ya Rais au kwamba wajibu huo mwngine ni wa Rais. (*Makofi*)

Hebu nieleze maana yake nini? Unapokuwa unaongea kwamba Rais amepewa nguvu nydingi. Hebu nieleze kwanza maana ya Rais. Rais ni Mkuu wa Nchi, Rais ni Mkuu wa Majeshi, / mean Amiri Jeshi Mkuu, Rais ni namba moja. Rais ni Mtawala Mkuu wa nchi, nikienda kwenye Kiingereza ni (*VIP*) very very very important person, ni mtu muhimu sana katika Taifa hili. Kwa hiyo kazi zingine zilizotajwa hapa na shughuli zingine ni kama vile kuteua Tume, kuitisha Bunge la Katiba na kupokea mapendezo ya Katiba. Hiyo ndijo kazi nydingine anayoweza kuifanya Rais. Pia kuchagua mfumo wa kuiende Katiba nayo anaweza akachagua. Tumeona nchi zingine zinaamua tu, Rais anasema aah! Hakuna haja ya kuitisha, tutaita Bunge hili hili, tutapanga na litatunga Katiba. Kwa hiyo, naomba tuelewe kuwa Rais huyu njaa ikija ni Rais, nchi ikiingia katika mtafaruku, mtu wa kwanza kuulizwa ni Rais, kama tukikosa mafuta ni Rais. Sembuse kuunda Tume ya maoni ya Katiba ndijo ioneokane ni jambo kubwa? Nani namba moja katika nchi hii? Nani wa kumwendea, ni nani atakayeulizwa dunia nzima masuala ya Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala nyeti kama hili naomba tu nichangie kwamba Tume peke yake itakayokuwa imechaguliwa na Rais ndijo Tume peke yake itakayokusanya maoni ya Watanzania wote. Hayo mambo ya harakati, hivi wanaharakati, wamechaguliwa na nani? Tanzania nzima tumeamua wote kwa akili zetu, tukaenda kwenye vi-box tukaweka tiki kwa Kikwete, tukasema huyu ndije kiongozi wetu. Lakini inapofika kuteua Tume eti siyo tumempa madaraka mengi. Ni Watanzania wote wameamua kumpa madaraka mengi, kama unamwonea husuda pole, ataendelea kuwa Rais mpaka 2015 na tutaendelea kumtii kwa namna yoyote, maana ni wajibu aliopewa na Katiba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, walikuwa wanatingisha kiberiti, kiberiti kimejaa na CCM inaendelea kutawala. Hawa watu ambao wanajiita wanaharakati siku zote wako *negative* na Serikali, kwa nini hata siku moja wasiseme jamani tumekuja kumpongeza Rais ambaye yeye baada ya kuchukua siku mia moja kutengeneza Katiba ameamua zaidi ya miaka mitatu. Kwa nini isiwe hivyo? Wakati kuna watu walituambia wakiingia madarakani watachukua siku mia moja tu na watu walikuwa wanashangilia. Nini tatizo leo Mheshimiwa Kikwete akikaa na kutupatia Tume ya kutengeneza na siyo kutengeneza tu pia na kutafuta maoni ya wananchi, namna gani tuendelee kutengeneza Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza vizuri, lakini naomba niongelee katika Chama cha CHADEMA walionelea suala linalohusu utawala wa kifalme. Naomba nieleze kwamba utawala wa kifalme uko kwenye chama cha CHADEMA, kwa nini? Ukiangalia mfadhilli wao amekuja na mtoto wake, kuna mdogo wake, kuna mtoto wa nani. Ukienda kwa Tundu Lissu kaja na dada yake. Ukienda kwa Mwenyekiti wa chama ana ndugu watatu. Nani ameleta ufalme zaidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Slaa kuna mke wake. Nani ana utawala wa kifalme. Ndesamburo amekuja na mtoto wake na mkwe wake, samahani Mheshimiwa Ndesamburo. Hivi hebu tuseme na naomba nieleze ukweli, Chama cha Mapinduzi kilitengeneza utaratibu wa kupata Viti Maalum na watu wako humu wamechaguliwa na wanawake kuwakilisha mawazo yetu. Wao ukiangalia tena siyo kifalme tu, na ni tuseme Kaskazini tu, nawashangaa watu wanaojiita CHADEMA Tanzania. Hivi kweli wewe ni CHADEMA unaangalia tu. Wenzako wapo Bungeni wewe huulizi watu hao wamepatikanaje? Waliweka mkutano Dar es Salaam, mkutano ukafanyika watu wakapatikana, baada ya kupatikana wakasema ni batili. Wakaenda kuitana kwa sababu ndugu hawakuwemo. Wakaenda kuitana, wakachaguana, tunawaona Bungeni, nani wana ufalme, CCM au CHADEMA? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusiogope kuambizana ukweli. Huu ndiyo ukweli *period*, hakuna haja ya kubabaisha Watanzania. Mjiulize Watanzania huko. Mimi namshukuru Mungu kule kwetu tuliporudia kufanya uchaguzi, wengine wameona aah, CHADEMA basi. Tumefanya kwenye vitongoji ambavo vilishajiita, sasa wamesema mmh, sasa kwa tabia hii ya ufalme hiki chama hakifai. Kwa hiyo, nataka kusema wanatuchokoza CCM, lakini CCM tuna utaratibu na tumesema kwamba, tutunge kanuni, sasa watu kunyanyuka kuondoka kwenye mkutano inaleta picha gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndio tunaweka utaratibu na kwa bahati nzuri CHADEMA wasitudanganye, mawazo yao wameyakusanya, wakayatengenezea karatasi moja wakatuletea. Kwa hiyo, hapa kinachofanyika mawazo yao ndiyo tunayajibu. Maana hata hapa ninajibu utawala wa kifalme ni kutoka kwenye karatasi yao. Nawashauri sasa kama wanataka tukae kwa salama wathubutu kufanya hivyo wanavyosema kwamba eti wanatupa *time* yaani kuanzia leo tukifanya hivyo, tutafanya maandamano. Hivi hatuwezi kutunga Sheria ya kuzuia maandamano ambayo hayana tija? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tu kwa kumalizia, naomba tu niwaeleze Watanzania na Wanajimbo langu la Nkenge kwamba Kamati ya kukusanya Maoni itakapokuja, wajikusanye waseme wanachotaka na kitaletwa hapa na tutakijadili, kinachofaa kitawekwa, maana kuna watu wanadhani kila nitakachosema, hivi tupo milioni 40, kila mtu akisema hicho kitabu tutakibeba. Kwa hiyo, tutayapunguza yale maneno tutyaweka pamoja tutatengeneza kitu kimoja kinachowezekana, naona unataka kuniambia, basi nimemaliza na naomba kwamba niunge mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mchungaji kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi ajiandae na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu muhimu, ingawaje nakuja kuchangia wakati waliobobea kwenye

mambo haya wameshachangia, kwa hiyo napata taabu kama hutaweza kueleza vizuri lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema Bunge hili la Kumi linaingia kwenye historia maalum ya nchi yetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu Mungu ametupa nafasi kuwa sehemu ya kuandika historia ya nchi hii kwamba leo tunapitishaa Muswada ambao tunakwenda kuleta Katiba Mpya kwa maana ya mwanzo mpya wa nchi yetu ambayo tutakuwa wenyewe tumefikiri vizuri tulikotoka, tulipo sasa na tunakokwenda kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unapoona mtu anapata tabu na kujadili Muswada huu inasumbua kidogo. Rafiki zetu wa CHADEMA safari hii wameamua kuwa *style*, nadhani ni *style* tu. Wao waliamua, nadhani wana kazi nyngi, wakaamua kukusanya maoni yao, wakampatia mtu mmoja akayasoma maoni yao na wakaamua kwenda kuendelea na kazi zao. Kwa hiyo, nadhani tuwaheshimu kwa hilo. Lakini nimewasikitia tu hawakupata nafasi, labda wale wangepata nafasi kuongea yale waliyoyasahau, lakini wao wameamua kumwachia mtu mmoja alete maoni yake. Naambiwa wako *busy* wanajaza fomu za mali. Kwa hiyo, ni vizuri waendelee na hiyo kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuchangia, tunapounda Sheria hii yuko Mwanafalsafa mmoja alisema lazima tubakie kama Taifa. Tunapounda Muswada huu jambo la kwanza libaki ndani ya vichwa vyetu, lazima tubakie kama Taifa la Tanzania kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilivyoingia Bungeni na hii ni mara ya pili nilipewa Katiba hii niliapa kuiheshimu Katiba. Kuilinda na kuihifadhi. Wengine wote ambao ni Wabunge pia waliapa kuilinda na kuihifadhi Katiba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi leo kuunda au kutunga sheria inayokinzana na Katiba hii. Hatutaeleweka na nimewaambia hata wale wenzangu kwamba, nia yetu tunatunga Muswada lakini kinachotuongozia kwenye kutunga Muswada ni Katiba hii ambayo tuliapa kuilinda na kuihifadhi na ndio inatupa madaraka kwa kweli ya kutunga sheria. Wako wanaosema Tume isingeundwa na Rais. Ukisoma ibara ya Katiba ya 33 na 34 inampa nguvu Rais kufanya hiki alichofanya. Lakini niende mbali, Rais huyu amekuwa muungwana sana kwa Watanzania. Angweza akaamua akaunda Tume bila hata kuja kuleta Muswada hapa ndani na tusingemfanya lolote kwa sababu ana mamlaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1991 Rais Mwinyi, aliunda Tume ya Nyalali, hakuleta Bungeni, kwenda kuangalia kama kweli Tanzania tuingie kwenye Vyama Vingi au tusingie kwenye Vyama Vingi. Tume ya Nyalali, 80% ya Watanzania ikasema hatutaki Vyama Vingi. Lakini kwa *good will* ya kiongozi aliyejukwepo na chama kilichokuwa kinaongozoa, tukasema kwa mazingira ya sasa, twende kwenye Vyama Vingi na kwa sababu hiyo leo ndio maana tuna Vyama Vingi. Lakini baadaye alikuja Rais Mkapa, aliunda Tume ya Kissanga, ikamshauri, yapo aliyyoyafanya akaendelea mbele. Hata huyu angeamua kuunda Tume, ikafanya kazi anayoitaka na wala tusingemfanya lolote. Lakini ye ye ameamua kwa utashi wake mwenyewe kwamba, jambo hili ni jambo la kihistoria, ni vizuri niwahusishe watu wote na kila Mtanzania awe sehemu ya kuandika Katiba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukiuangalia Muswada huu wanaajaribu kuupotosha, Muswada huu hauna mambo mengi, Muswada huu unasema namna ya kupata Tume. Ambapo Tume kazi yake ni kuratibu maoni ya Watanzania, ikimaliza inapeleka ripoti kwa Rais na Rais ripoti hiyo tutakachofanya, tutaifanya iwe ya wazi. Akitoka hapo ni kuunda Bunge la Katiba, tukitoka hapo tunakwenda kwenye kupiga kura za maoni. Ndio kazi ya Muswada huu! Kanuni za Bunge, tumekuja hapa ndani tukasomewa mara ya kwanza. Leo tunabishana kwenye *first reading* na *second reading!* Hii ni nini! Ukisoma Kanuni za Bunge, ni kwamba tumezasoma mara ya kwanza. Lakini tukaambiwa kwa Muswada huu ni vizuri tukawahusishe watu wengi zaidi watoe maoni yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa waliokaa humu Bungeni miaka mingi, ukienda kwenye historia, toka mwaka 1977 hakuna Muswada ambao umechambuliwa, umepata maoni kuliko Muswada huu. Kila msomi, kila mwanaharakati, kila mwananchi, walio wengi waliotaka kutoa

maoni kwenye Muswada huu nafasi hiyo waliipata. Kwa kweli, niipongeze Kamati ya Bunge, ilifanya kazi kubwa sana kuhakikisha inachukua kila maoni ya kila aliyetaka kuleta maoni. Lakini jamani tukubaliane, leo tunasema tupeleke kila kijji wakatoe maoni! Waulize, wangapi wamesoma hata hii Katiba? Kwamba, sasa Muswada huu, Watanzania milioni 40 watasoma, sio kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema, nataka nitoe mifano michache, mwaka 2001 Rais Yoweri Museveni, aliunda Tume kwa ajili ya Katiba, hatukusikia kelele. Ghana, mwaka 2010 Profesa Atta Mills, ameunda Tume, ndio Rais wa nchi! Zambia, mwaka 2003 waliunda Tume! Kenya, waliunda Tume tena ya watu 6. Lakini leo inakuwa ni nongwa kwa Tanzania kuunda Tume! Hili ni la hatari sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Muswada huu nina mambo machache. La kwanza, ni *Section 24(2)*, ambayo tunawawekea masharti namna ya kupiga kura kwenye Bunge hili la Katiba. Ndugu zangu na Watanzania Bunge hili la Katiba, tunaliinua kuwa juu ya kitu kingine chochote; ni vizuri tungewaachia wao waamue namna watakavyopiga kura. Kwa hiyo, ningesema tubadilishe pale isiwe *two third*, waamue wao namna watakavyofikia uamuzi wa mambo watakayoyaamua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la Ibara ya 5 na Ibara ya 20. Ningombwa sana, Wanasheria Wakuu, kwa maana ya Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Tanzania Visiwani tuwaache, wataendelea kufanya kazi yao kuishauri Serikali kila siku, wasilingie kuwa sehemu ya huu Muswada. Lakini pia, nataka kuongeza pale, *Section 18* kwamba, baada ya Rais kupata maoni, ningombwa baada ya muda mfupi maoni haya yawekwe wazi ili tuondoe hii biashara kwamba maoni haya yamechakachuliwa, ripoti ile iwe wazi. Ningombwa tuongeza pale *Section* ya 18 ili tuweze kupata, ile ya kufanya maoni kuwa wazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningombwa, tuwashauri Waheshimiwa Wabunge, tulitafakari sana. Ukiangalia nchi zote walizokwenda kwenye kutunga Katiba Mpya, walichagua njia mbili za kupita; aidha walikwenda Bunge la Katiba wakamaliza wakaunda Katiba, ama walikwenda kwenye *Referendum*. Naomba kama Tanzania, tulitafakari upya! Sio vizuri kwa welfare ya nchi yetu kwenda njia zote mbili. Twende tuamue njia ambayo itakuwa ni nzuri, ambayo itashirikisha wananchi wengi, lakini tusifanye vitu vyote viwili. Naiona hatari kubwa zaidi na msisahau, tulikuwa na *Bomas One* ya Kenya, wakaenda kwenye Bunge la Katiba, walipokwenda kwenye *Referendum* ikakataliwa! Wamekwenda wakapata mpaka machafuko yale! Ndio maana wakaamua mara ya pili sasa, kuunda Tume ya watu sita, ndio ikaenda kutafuta maoni, yakaletwa kubarikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona ni vizuri tulitafakari upya kama Bunge, tunapotengeneza Muswada huu leo, tuamue tunakwenda na njia ipi ambayo itawashirikisha Watanzania wengi zaidi. Nashauri, kama inawezekana, twende kwenye *referendum* tuache Bunge la Katiba, ili tuwe na hakika na tunachokitafuta. Kwa sababu, hapa ndugu zangu, tunajenga Taifa. Tunachofanya leo, tunaleta Muswada wa kuja kujenga Taifa ambalo ni lazima libakie kuwa Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huo ndio umekuwa wasiwasi wangu, naomba sana tulitafakari upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu, hoja muhimu ya Muswada wa kutafuta utaratibu wa namna ya kuunda Tume itakayotafuta maoni kwa ajili ya kupata Katiba Mpya. Naomba nianze kwa kuungana na wachangiaji wenzangu, kumshukuru sana Mungu kuweza kunipa fursa ya kuweza kusimama na kutoa mchango wangu mfupi ambao nitautoa kama ifuatavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubali kabisa kwa

utashi wake kuturuhusu sisi Watanzania tuingie katika mchakato wa utaratibu wa kupata Katiba Mpya, ifikapo mwaka 2015. Nasema namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu kama yeye asingeweza kuruhusu tuanzishe mchakato, tusingeweza kufanya hivyo. Nampongeza sana na kwa kweli tunaomba Mwenyezi Mungu, amjalie kwa kila jambo na ampe afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeziki, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Celina Kombani na timu yake yote. Naomba pia nimpongeze Mwenyeziki wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pindi Chana, kwa kazi nzuri sana waliyofanya ya kuchambua maoni ya wananchi, maoni ya wadau, maoni ya Kamati ya Sheria na Katiba na leo tunapata Muswada mzuri kabisa ambao kwa kweli nauona ni Muswada wenyetia kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyeziki, baada ya utangulizi huo na kwa kuwa, wachangiaji wenzangu tangu juzi wamekuwa wakiwaelimisha Watanzania, juu ya upotoshwaji ambao umekuwa ukifanywa na baadhi ya vyama vingine vya wenzetu, ningependa kujielekeza tena huko kwa sababu, najua Watanzania ni waelewa sana hivyo wameshaelewa mchele ni upi na pumba ni zippi. Rai yangu kwao ni kwamba, waendelee kutuunga mkono, watuombee dua na hasa kwa wanawake, vijana na wazee, ili Muswada huu tuweze kuipitisha kama tuliyopanga na mchakato wa Katiba upatikane na ifikapo mwaka 2014 tupate Katiba Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeziki, nasema naunga mkono hoja hii kwa sababu, Muswada huu umezingatia maoni ya wananchi, umezingatia maoni ya Kamati na umezingatia maoni ya wadau mbalimbali. Naomba sasa nzungumzie vipengele vichache ambavyo nimeviona vinahitaji kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyeziki, naomba nzungumzie kile kipengele cha uundaji wa Tume. Hapa ningependa nitoe ushauri kwamba, badala ya kusomeka kwamba, Rais baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, pia atawashirikisha Wanasheria wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria wa Serikali ya Zanzibar naomba hawa tuwaondoe, badala yake Rais peke yake na Rais wa Mapinduzi Zanzibar, wanatosha kabisa kuunda Tume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeziki, kipengele kingine ambacho naomba kifanyiwe marekebisho, ni ule utaratibu wa muundo wa kupata Tume yenyewe. Pale kinapozungumzia uteuzi wa Mwenyeziki, kile Kifungu cha (2), kinasema kwamba, uteuzi wa Mwenyeziki na Makamu Mwenyeziki, utafanyika kwa msingi iwapo Mwenyeziki atatoka upande wa Zanzibar na mwingine atatoka upande wa Jamhuri. Napenda nishauri kabisa kwamba, kipengele hiki kiwe wazi kabisa na kieleze kwamba, uteuzi wa Mwenyeziki na Makamu Mwenyeziki wa Kamati ya Tume, utafanyiwa na Rais Mwenyeewe baada ya kushauri na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyeziki, sehemu nyininge ambayo nimeona niitilie mkazo, ni lile eneo la uundaji wa Tume; ambayo inawataja Wanasheria pia watahusika. Hapa pia nashauri Wanasheria waondolewe.

Mheshimiwa Mwenyeziki, lakini kuna kile kifungu katika ukurasa wa 30, kinazungumzia namna ambavyo Tume itakuwa, kwamba itazingatia umri, itazingatia jinsia na itazingatia uwakilishi. Nashauri ingewekwa wazi kabisa, kiongezeke kifungu ambacho kinaonesha ni wanawake wangapi watakuwa katika Tume hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeziki, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni ukurasa wa 31, kuhusu Muundo wa Tume. Hapa nilikuwa nashauri pia, uteuzi ufanywe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika ukurasa wa 35, ningependa nishauri pale, Tume yaweza; hapa imeonekana kwamba, Tume inaweza ikamuagiza Mkuu wa Wilaya, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji, wakaitisha mikutano kwa ajili ya kuongea na wananchi. Naomba niungane na Mheshimiwa Lekule Laizer, kwamba hapa tungeongeza Madiwani na tungeongeza Wenyevitii wa Serikali za Vijiji na ikiwezekana Wenyevitii wa Vitongoji kwa sababu, hawa ndio wenyetia. Nashauri hivyo kwa sababu, tukiwaachia Watendaji wetu wa Vijiji na tukiwaachia Watendaji wetu wa Kata, ambao kwa kweli kimsingi hawana watu, ipo hatari Tume ikakuta tunapokea maoni kwa watu wachache, kutohana na hali halisi ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nichangie katika ukurasa wa 37. Kuna mahali Ibara ile ya 19(1) inasema: "Mtu ye yeyote hataruhusiwa kukwamisha shughuli za Tume". Nashauri, lionezwe neno Taasisi, yaani Taasisi yoyote, kwa sababu, katika kipindi hiki kinachoendelea, tumeshuhudia baadhi ya Asasi na Taasisi, zimekuwa zikipotosha hata zoezi hili linaloendelea. Tukiiacha hivi hivi, tukasema mtu peke yake bila kutaja na Taasisi, ipo hatari kabisa ya watu wanaojiita Wanaharakati, kuingilia shughuli za Tume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 37, napenda pia kushauri kwamba, Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar, hapa pia nilikuwa nashauri Wanasheria watoke katika kile kifungu cha 20, abakie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, wanafaa kabisa kumaliza hii kazi bila kuwaingiza Wanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuzungumizia ule ukurasa wa 30, kuna kifungu kinachozungumzia kwamba, kutakuwepo kile kifungu cha (2), kwa madhumuni ya kuwaelimisha na kuwashamasisha Watanzania kuhusu kupiga kura ya maoni. Hapa tumetajwa sisi Vyama vya Siasa, Vyama vya Hiyari na Vyama vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda niweke angalizo. Ni lazima Muswada au Sheria tutakayoitunga ileze wazi kabisa kwamba, huu uhamasishaji pasiwepo na upotoshaji. Hapa nilipenda kabisa nishauri na nafikiria suala la kukusanya maoni tuiacie Tume peke yake. Sisi wanasiwa na wanaharakati tukae pembedi, maana tukichanganya mambo ipo hatari ya kufanya mambo yasiende kama tulivyopanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushauri haya machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache kuhusu mchakato tunaoendelea nao wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wenzangu wameongea mengi sana. Naomba nijikite moja kwa moja kwenye maeneo makuu matano. Jambo la kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Vile vile napenda kuwapongeza wananchi wote na wadau mbalimbali walitumia nafasi yao kutoa maoni yao, baada ya Muswada wetu kuusoma kwa mara ya kwanza na kupata fursa kuchangia ili tuwe na uelewa wa pamoja na kuongeza maeneo ambayo yatatusaidia kuelekea kupata Katiba Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuchukua fursa hii kupongeza Ofisi ya Spika, kuwa karibu na sisi Wabunge, pale ambapo tulikwama tulivyokuwa tumekubaliana kwa mara ya kwanza, kwenda kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu mchakato mzima wa Katiba. Pale ambapo tulikwama tulifika kwenye Ofisi yake, tukapata ushauri, tukaweza kuwafikia wananchi wetu kwa urahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu napenda nichangie kwenye Sehemu ile ya Tano ya Muswada wetu ambayo inasema, Kuundwa kwa Bunge la Katiba. Tunaona kwamba, hapa Wanasheria watashirkishwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar; lakini vilevile napenda kupendekeza kwamba, Wanasheria waondolewe kwenye sehemu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia jukumu kubwa litakalofanywa na Bunge la Katiba kwanza, Wajumbe wa hili Bunge la Katiba haihitaji sana masuala ya sheria. Tunaona wajumbe watatoka kwenye Asasi za Kidini, Vyama Vya Siasa, makundi ya watu wenye mahitaji, taasisi za elimu, na kadhalika. Kwa hiyo, nasema kwamba, kwanza hawa wanasheria moja kwa moja ni wajumbe kwa nafasi zao kwa sababu, Mwanasheria wa Jamhuri ya Muungano ni Mbunge na Mwanasheria kutoka Zanzibar ni Mjumbe kwenye Baraza la Wawakilishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile napendekeza watoke hapa kwa sababu moja; haihitaji *application* ya sheria kupata wajumbe hawa. Lakini vilevile tusimfunge Mheshimiwa Rais kwamba, sasa hawa ndio wawe washsuri wake, tumuache Mheshimiwa Rais kwa mamlaka yake aliyopewa, kwa sababu tunajua Rais ni Taasisi, kama atahitaji ushauri kutoka kwa viongozi wa dini, maaskofu, katika utaratibu wa kuunda Tume, tumwachie ataamua mwenyewe. Lakini tusimfunge kwamba, lazima apate ushauri kutoka kwa Wanasheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu Mamlaka ya Bunge la Katiba. Napenda kuchangia sehemu hii kwa sababu moja tu, tumeona kwamba mamlaka ya Bunge la Katiba, kutakuwa na masharti ya Muswada wa Katiba. Haya masharti ya Muswada wa Katiba yataletwa kwenye Bunge la Katiba na Mheshimiwa Waziri na pale tunaambiwa kwamba, Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Wajumbe kutoka Tanzania Visiwani lazima idadi yao kwa kila upande itimie theluthi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi kwanza niseme sio Mwanasheria, lakini naijuliza maswali, hapa tunaongelea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ambayo inatuunganisha sehemu zote mbili! Sasa huu utaratibu uliowekwa hapa, tumefika hapa kama Wajumbe kwenye Bunge la Katiba, lakini tunalazimishwa kwamba huku ni lazima itoke theluthi mbili na kule ni lazima itoke theluthi mbili, kwa misingi gani wakati sisi sote ni wamoja? Kama tunakutana kama Bunge la Katiba, tuwe wamoja, isiwe tena lazima tuhakikishe theluthi mbili itoke kila sehemu, hapa tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani, inaweza ikatokea upande mmoja isitimie theluthi mbili, je, hapo ndiyo itakuwa mwisho wa mchakato wa kupata Katiba au kutatokea nini? Tutakuwa tunawanyima wananchi fursa na tutakuwa tunarudisha mchakato wetu wa kuelekeea kupata Katiba Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa naijuliza binafsi katika muundo huu wa Sekretarieti, hapa tumeambiwa kabisa kwamba Katibu wa Sekretarieti atateuliwa na Rais, mimi sina tatizo lakini sifa zilizowekwa pale kwa Katibu wa Sekretarieti ndiyo zinatupa mashaka, awe na taaluma ya sheria, awe amefanya kazi miaka kumi, awe na mwenendo na tabia nzuri, tabia nzuri ni ipi? Sisi tumezoea kwenye masuala ya *public* tunasema kwamba huyu mtu asiwe amehukumiwa kwenye makosa ya jinai tosha, lakini hapa tunaambiwa awe na tabia nzuri. Sisi hapa tunamchonganisha Rais wetu na wananchi, huyu atakayeteuliwa ndiyo mwenye tabia nzuri kushinda Wanasheria wote? Anaweza kutuambia tabia nzuri ni zipi? Kwa mimi nasema Wanasheria watafute lugha nyngine hapa wasiseme awe na tabia nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii Katiba ni ya Watanzania, ni ya wananchi wote, Utumishi wa Umma unaingiaje hapa, hatuendi kutunga *Public Service Act*. Kwa hiyo, kama kigezo ni Uanasheria, tutafute Wanasheria ambao ni *competent*, wawe *listed*, waende wakafanye *interview*, kuwe na *fairness* ili hata atakayepatikana tujue kwamba huyu ndiyo ameshinda anakuwa Katibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaangalia muundo wa Sekretarieti, tunaambiwa ukubwa wa sekretarieti itategemea jinsi itakavyopendekewa na Bunge na Katiba. Sasa mimi nikaijuliza na hapa wanasema tena lazima wote wawe Watumishi wa Umma. Sasa mimi nikasema Utumishi wa Umma hapo kuna nini, wanaofanya kazi kwenye taasisi nyngine ambao tumewahamasisha wenyewe wasitegemee ajira za Utumishi wa Umma hawana fursa? Kwa hiyo, mimi nasema kama Sekretarieti watakuwa watu 20 kuwe na *fairness*, kumi watoke kwenye *Public Service*, kumi watoke kwenye taasisi nyngine, hii kwanza itakuwa inaleta uwazi, hakuna haja ya kuweka migogoro kwenye sehemu ambayo haina haja. Kwa hiyo, nimeona hili niliseme na lichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kuongea ni mchakato wa kupata Katiba Mpya, kwangu mimi naona umekuwa mrefu sana, Tanzania ni wanachama kwenye Jumuiya za Madola, tumeona nchi nyngi mfano Kenya, Uganda, Ghana na nchi zingine wanapitia kwenye michakato hii ya Katiba Mpya lakini sisi tunaanza kwanza Kamati, Bunge la Katiba, Bunge la Katiba litoe mapendekezo yaafikiwe na theluthi mbili kwa kila upande, tukitoka hapo wote tukubaliane

theluthi mbili ipatikane, twende tutembee tena kwa wananchi, tutaelimisha wananchi lini Mwenyekiti? Sisi wote ni mashahidi pamoja na kwamba Katiba ni msingi unaotuongoza lakini hatuna utaratibu wa kusoma Katiba zetu. Siamini wananchi wangu wa kule Morogoro Vijiji, Ulanga, Malinyi wanajua Katiba hii, tunatumia muda mwangi kwenye michakato ya huku ndani sisi wenyewe kwa wananchi tutaenda saa ngapi? Kwa hiyo, mimi napenda tufuate utaratibu mwagine, tusitumie *system* zote mbili, Bunge la Katiba, tumalize hapo twende kwenye *referendum*, kura za maoni, tunawachelewesha wananchi, wananchi wana kiu na Katiba yao, wananchi wanapata shida huko, wanawake wanakandamizwa, vijana wanataka kujua fursa zao za kumiliki mali, tunawachelewesha sisi tunajifungia huku ndani tunatafuta theluthi mbili kila upande. Naomba kama inawezekana tuchague utaratibu mmoja tuutumie kama wenzetu Kenya na nchi zingine Ghana walivyotumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kulichangia ni kuhusu mamlaka, kuna maneno mengi sana huko mtaani kwamba Rais ana mamlaka makubwa, Rais amefanya hivi, mpaka watu wamesahau kwamba Rais ni taasisi, Rais siyo Jakaya Kikwete, Rais siyo Mkapa, Rais siyo Mwinyi, Rais siyo Nyerere, Rais ni mtu yeoyote atakayechaguliwa kwa kura za kutosha, wamegombea wengi ameshinda yeeye.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa.

(Hapa Mhe. Sara M. Ally aliendelea kuongea huku microphone yake ikiwa imezimwa na Mwenyekiti)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa naomba kumwita Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Kigola na Mheshimiwa Sulemani Jafo wajiandae. *(Makofî)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya sijui ni maruhani ya wapi?

WABUNGE FULANI: CHADEMA!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Lakini naomba kusema yashindwe na yalegee katika jina la Yesu. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kushiriki katika mjadala huu muhimu sana katika Taifa letu la Tanzania. Mimi naweza kusema kwamba namshukuru Mungu kwa sababu nafasi hizi ni nafasi adimu sana na kwa kweli unapokosa kutumia nafasi adimu kama hii ya kuweka historia ya nchi yako kwenye suala nyeti kama la Katiba, sidhani kama unaweza ukaipata tena. *(Makofî)*

WABUNGE FULANI: Haipo!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Miaka hamsini ya uhuru, tunaipongeza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mimi kwa kipongeza sana Kamati ya Katiba na Sheria. Najisikia faraja sana kwa sababu Kamati hii inaongozwa na akinamama wawili na Waziri anayesimamia Muswada huu ni mwanamke. Mimi nafikiri niseme kwa uadilifu wa wanawake, kazi hii kwa kweli imefanyika kwa umakini mkubwa, nawapongeza sana. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, mchakato huu tunaoendelea nao wa kuisaidia nchi yetu kutimiza hii miaka hamsini ya uhuru lakini tukiingia na harakati za kuwa na Katiba Mpya, mimi nadhani ni zoezi la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Sisi ni tofauti na mataifa mengine, ziko nchi ambazo labda wamekuwa wakizitolea mfano, zenyewe zimekuwa na harakati za kuandika Katiba Mpya bila kuwa na Katiba nyingine. Sasa huwezi ukafanisha michango ya wale ambaa hawana Katiba, ukatulinganisha na sisi Watanzania ambaa kwa miaka hamsini tumekuwa na Katiba yetu hii. *(Makofî)*

(Hapa alionyesha Katiba)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Sasa haya mambo mawili ni mambo tofauti kabisa. Sasa sisi tunaongozwa kwanza wakati tukiingia katika mchakato huu wa kuandika Katiba Mpya lakini bado tunaongozwa na Katiba iliyoko hapa mbele yetu na tena ndiyo Katiba ambayo imetupa dhamana hata sisi Wabunge kuwa ndani ya Bunge hili kuwawakilisha wananchi ingawa sisemi kwamba Katiba yetu hii tunayoenda kwenye mchakato; na tutakapotoa mawazo Watanzania wote watakuwa huru kutoa maoni yao nini wanakitaka kiwe katika Katiba yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza ya Katiba ambayo tunayo sasa kabla sijaingia katika sheria yenye, naomba niyasema haya. Sehemu ya Kwanza ya Katiba hii inamtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa mtu ambaye kwa namna yoyote ile hajisikii raha ama uhuru kuona sehemu ya Katiba tuliyonayo sasa ambayo tunaiheshimu inamtaja Rais hilo siyo shauri yetu, ni shauri la Katiba ambayo tunaiheshimu siku zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Sehemu ya Tatu ya Katiba hii inalitaja Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwemo Wabunge na wawakilishi kutoka Zanzibar na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini Sehemu hii ya Tatu inasema kwa mfano Ibara ya 62(1) kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge yaani bado hapo tena unaona kwamba Rais pia ni sehemu ya Bunge hili. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Sawasawa!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Kwa hiyo, hata kama kuna mawazo ambayo Rais anayaleta humu ndani, ni sehemu jamani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Sehemu ya Tatu inaendelea, katika Ibara hiyo ya 62 inasema, iwapo jambo lolote lahitaji kuamuliwa na kutekelezwa na sehemu zote mbili za Bunge yaani Rais na Wabunge kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii ama masharti ya sheria nyininge yoyote basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo ila mpaka limeamuliwa au limetekelezwa na Wabunge na vilevile na Rais, kwa mujibu wa madaraka yao kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoleta jambo, ndiyo maana nilianza kwa kuwaambia ndugu zangu sisi ni nchi tofauti kwa sababu bado tunayo hii Katiba na ndiyo tunafikiria sasa mchakato wa kuandika Katiba Mpya. Katiba hii inatuambia madaraka mengine ya Bunge hili ni kutunga sheria, jamani Katiba hii Mpya kuiandika ni *process*.

MBUNGE FULANI: Sawasawa!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Ni mchakato, sasa mchakato ukaanzie wapi, porini?

MBUNGE FULANI: Nadhani!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Hauwezi kuanzia porini ama mahali pengine ni lazima tuwe na mahali pa kuanzia mchakato na mahali pa kuanzia mchakato kwa mujibu wa Katiba ambayo tunayo mpaka sasa ni ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa mchakato wenyewe ili uanze ndiyo tumesema kwamba unaanza na Muswada ambao tuko nao leo ndani ya Bunge hili, hiyo ndiyo sehemu ya kwanza sasa ya mchakato. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania muelewe kwamba kuandika Katiba Mpya, ni mchakato na uzuri ni kwamba sisi tunaanza Katiba Mpya wakati tayari tunayo Katiba yetu miaka yote hii hamsini ya uhuru tunayo Katiba yetu. Kwa maana hiyo, ni lazima sasa tuanze mchakato wa kuandika Katiba Mpya na mchakato Watanzania wenzangu wa kuandika Katiba Mpya ndiyo unaanza sasa kwa kutunga sheria hii na sheria hii tunayoitunga leo siyo ndiyo Katiba mpya hii sasa ndiyo sehemu ya kwanza ya mchakato wa kutunga Katiba Mpya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwalimu na ninaweza sana kufundisha. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Sawasawa!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Nadhani leo nichukue nafasi yangu ya Ualimu nifundishe kwanza. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Fundisha!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitakuambia.

MBUNGE FULANI: Mmmh!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Kwenye mchakato wa sheria hii ambayo sasa sisi kwa mujibu wa Katiba kama Wabunge ambao tuna mamlaka ya kutunga sheria, sheria hii tunayoianzia mchakato huko baadaye tutakuwa hatuna ubavu nayo baada ya Bunge la Katiba kuundwa sisi sasa mchakato wetu utakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kusema nini? Ukiangalia maana ya Muswada huu pale tunapoanza katika sehemu ile ya mwanzo kabisa ya taarifa na utanguzi, sheria hii tunasema imeandikwa tena vizuri tu. Tunatunga sheria kwa ajili ya kuunda Tume, Watanzania tunatunga sheria kwa ajili ya kuunda Tume ya mabadiliko ya Katiba, kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba. Tumeona kabisa kwamba maana ndefu ya Muswada huu inajieleza vizuri na bado inaendelea kuainisha na kuchambua maoni ya wananchi. Sasa jamani hayo maoni ya wananchi yataanza kuainishwa vipi kama hii sheria ya jinsi ya kuainishwa itakuwa haijapita? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado inaendelea kuainisha masharti kuhusu mabaraza ya kuhalalisha masharti yalimo kwenye Rasimu ya Katiba, yaani huo mchakato baadaye utatengeneza mpaka rasimu, sasa rasimu ile itatengenezwaje tuisipomaliza mchakato huu wa leo? Kwa hiyo, lazima tumalize mchakato huu wa leo ndiyo hata haya mabaraza sasa na rasimu ya Katiba itaweza kupatikana. Lakini naendelea, mimi hapa ndiyo naona kuna ugomvi, mengine yote wala siyo ugomvi, watu hawaelewii kama kitu hiki kipo. Lakini tunaendelea kuweka masharti juu ya utayarisha na uwasilishaji wa ripoti kuhusu maoni ya wananchi, ina maana maoni ya wananchi yatachukuliwa, Watanzania maoni mtatoa, sasa mtu anayesema kwamba maoni yenu hayajatolewa wakati sheria hii tunayoitunga leo ndiyo itapokea maoni yenu, sasa mimi siwezi kuelewa tunazungumza nini. Hapa leo ndiyo sehemu yenye matatizo lakini tunasema hivi ni kuweka utaratibu wa kuunda Bunge la Katiba, Watanzania leo hapa sisi hatujakaa kama Bunge la Katiba bado halijaundwa. Sheria hii ndiyo itakayounda Bunge la Katiba, tunapoikubali sheria hii na kuijipitisha ndiyo itatusaidia kuunda Bunge la Katiba. Mwisho, uendeshaji wa kura za maoni na kuweka masharti yanayohusiana na mambo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu niwalize Watanzania, kuna ugomvi katika haya? Mnatuona kweli tunafanya kitu ambacho hakieleweki? (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Hakuna!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Tumefanya kitu kinachoeleweka kwa manufaa na mustakabali wa nchi yetu. Kwa hiyo, naomba niseme ndugu zangu Watanzania ukishaangalia sasa sehemu hiyo ndiyo utakuta sasa Muswada huu umeeleza mambo mengi, tafsiri ya maneno katika huo Muswada, umeeleza madhumuni ya Muswada wenywewe na Waheshimiwa Wabunge hapa wamewaelezeni kwa undani kabisa wala sitaki kurudia. Ukiendelea Muswada huu unaeleza uundwaji wa Tume utakaoenda kuunda utaratibu mzima wa kukusanya hayo maoni, ipo humu ndugu zangu na tunapopitisha Muswada huu ndiyo sasa tutayapata hayo yote. Imeeleza namna ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri mzuri tu, Mbunge yejote mwenye busara na ilikuwa atoe ushauri wake sasa humu ndani kusudi tupate kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Watanzania wote mnaotusikiliza, naomba niseme hatua hii ama itatuunganisha Watanzania na kudumisha amani na umoja wa Taifa letu ama hatua hii tusipoangalia toka mwanzo ndiyo itavuruga amani na umoja wa nchi yetu. Kwa hiyo, niwaombe tuone umuhimu wa Muswada huu na Muswada huu nirudie kusema siyo Katiba ndiyo mchakato na ndiyo tunaanza kazi na tunamwomba Mwenyezi Mungu atusaidie sana kazi hii ya kutunga Katiba Mpya iwe na tija kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi, nimesikiliza maoni ya Kamati, nimepitia haya majedwali ya mabadiliko ya Serikali hakika kazi kubwa imefanyika wala sitaki kurudia, tutakapofikia hatua ya mwisho ya Muswada huu Watanzania watapata picha kwa kiasi gani Serikali imezingatia masuala mengi, ushauri wa kila namna kutoka katika makundi mbalimbali toka Muswada huu Uliposomwa Mara ya Kwanza na kukabidhiwa kwenye Kamati yetu. Kwa hiyo, nawaomba tuwe watulivu, nawaomba tusingie katika kujadili kitu ambacho hakipo, sheria yetu hii ndiyo itakayotuongoza na nimesema maneno hayo ili tuweze kuelewa nini tunachokianza, huu ni mchakato na sasa ndiyo tunaanza mchakato mzima, wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho, nitapita tena kijiji kwa kijiji wote nyie nitawaandaa mtoe maoni yenu na nina uhakika Serikali itafanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuitakia kila la kheri Serikali yangu imefanye zoezi hili kwa umakini mkubwa na Mwenyezi Mungu kwa kweli atusimamie, nchi nyingi zimepoteza amani katika mchakato wa kutunga Katiba. Sisi hayo Mungu ayaepushe katika Taifa letu na nchi yetu. Ndugu zangu sasa hivi tunapitia sheria ya kuanzisha mchakato na siyo Katiba, hatuzungumzi humu Katiba na Katiba wananchi watapata nafasi ya kutoa mapendekeo wanayotaka yazingatiwe kwenye Katiba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mhagama kwa mchango wako mzuri. Namwita sasa Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Muhammad Sanya wajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mawazo ambayo ninayo kichwani. Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani kwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Kamati yake kwa jinsi walivyofanya kazi nzuri sana ya kutuongoza katika mjadala huu. Mjadala huu ni wa muhimu sana kwa Watanzania wote na ninashukuru sana kwamba Watanzania wa sasa hivi siyo Watanzania wa mwaka jana bali ni Watanzania wanaolewa vizuri...

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Kuna watu wanaoongelea masuala ya Muungano, wengine wanasema Muungano eti Hayati Mwalimu Julius Nyerere alichukua mchanga akachanganya ndiyo tukapata Muungano, mimi nakubaliana na hilo lakini pamoja na hilo, nadhani Muungano umekwenda mbele zaidi, kuna watu wengine hawaelewii. Sasa napenda nieleze umekwenda mbele zaidi kivipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano huu siyo wa kuungana kwa mchanga tu, sasa hivi watu wameungana mpaka familia, yaani familia ya Zanzibar na familia ya Tanzania Bara tupo pamoja. Kuna watoto wengine tunavyoongea hapa wazazi wao wako Zanzibar lakini wanaishi Dar es Salaam, watoto wengine wazazi wapo Dar es Salaam lakini wanaishi Zanzibar. Huo ni mchanganyo wa hali ya juu sana. Sasa wewe ukisimama hapa unasema Muungano una wasiwasi basi wewe ndio una wasiwasi kwani Muungano hauna wasiwasi hata siku moja. Nakuhakikisha hata ukisema kwamba unataka Muungano ufe labda utakufa wewe mwenyewe lakini Muungano upo palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Watanzania tuelewe kwamba dunia ya leo ni ya hali ya juu sana. Kila siku mambo yanabadilika, siku ya leo ni tofauti na siku ya kesho. Sasa kuna watu

wengine wanafikiri wakileta vitu vya ajabuajabu hapa watu watabadilika vichwa basi waelewe kwamba wakati wote tunatumia akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mtoto anatoka darasani, hahudhurii kipindi basi hawez i kufaulu mtihani, hata akifafulu hawez i kuwa mwanafunzi mzuri kwani hawez i kutoa *advice* kwa watu yaani hawez i kushauri watu hata siku moja. Sasa sisi darasa letu la leo naona limekamilika kwani watu wote waliopo ndani ni watu wa kufaulu mtihani. Katiba itatungwa na mchakato unakwenda salama, hizi nyingine ni mbwembwe tu na kuna watu sasa hivi wanafanya utafiti, wanaangalia Tanzania kwa nini ni nchi ya amani na wanaangalia ni *formula* gani imetumika. Sasa hivi ukiangalia ulimwengu wote watu wanaishi maisha ya ajabu sana, tukitoa *reference* na siyo siri, sasa hivi tunavyoongea watu wa Siria wanapata shida sana na wenzetu wa Libya wamepata matatizo kutohana na vitu vidogovidogo tu lakini baadaye vikawa vikubwa. Lakini kwa Watanzania weny e akili na umoja, weny e familia moja, weny e kabila, hawana udini, watu wengine hawataweza kuwavuruga, mimi nawahakikishia. Sasa hivi tumeanza na hatua nzuri sana, kitu chochote unapofanya utafiti ni lazima uanze na hatua ya kwanza na hatua yetu ya kwanza kabisa sisi Watanzania weny e akili iliyotulia ni kwamba tumeanza na mchakato wa kuunda Katiba Mpya na mchakato huu tumeanza na Tume. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka ya 1974, Mwalimu Nyerere aliweza kuwahamisha wanakijji wote wanaokaa porini kwenye vichaka akasema mkae kwenye barabara na tulihama. Sasa hivi Rais Jakaya Kikwete amefikiria amesema kwa sababu ulimwengu umebadilika na Katiba ni lazima ibadilike na wananchi tumekubali, lakini sasa itabadiika kivipi? Ni lazima tuanzie mwanzo, huwezi kusema unatunga safari labda ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam ukaruka na kufika Dar es Salaam, haiwezekani kwani ni lazima kuwe na hatua za kuanza safari yako. Watanzania nataka niwaambie na sisi tumeanza safari ya kutunga Katiba lakini huwezi kuanza kutunga Katiba kama hakuna Tume, nani atakusanya maoni?

MBUNGE FULANI: Hapo sasa!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Ili kutoa maoni ni lazima watu watembelee vijiji vyote. Mimi nawaambia kwa niaba ya Wilaya Mufindi, wananchi na Watanzania wote, hatua tulioanza ni sahihi kabisa wala hakuna wasiwasi. Ndiyo maana nimesema Watanzania ni watu weny e akili na tumeanza vizuri. Rais angeweza kutunga kufuatana na Sheria inavyosema, angeweza kukaa na kuunda Tume, amepewa Mamlaka hayo na ninataka nimwambie Mheshimiwa Rais kwamba ukitaka Watanzania wakukumbuke vizuri basi itoke vizuri Katiba hakuna shida kwa sababu italenga miaka 20 ijayo na tutakukumbuka kwani umeanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna watu wanataka wAMDANGANYE kwamba kwa nini Wanasheria wanashiriki, Wanasheria ndiyo washauri wakuu na kama Wanasheria hawatamshauri vizuri kwa kufuata vifungu vya Sheria ambavyo vinatuongoza katika maisha sisi tutawauliza, wala hakuna shida kwani ndiyo *system* inayotakiwa kuwa na ndiyo maana ukienda tofauti na Sheria unakwenda kwenye Mahakama, unapigwa jela miaka kadhaa, ni Sheria! Sasa tumeanza vizuri kabisa watu wengine wanataka kupinga hata Sheria, aah! Hiyo haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Tume, tukirudi kwenye Muswada kamili, mimi naomba kwanza kabisa inabidi Katiba zitawanywe kwa wananchi ili waanze kusoma kabla maoni hayajakusanya, kwa sababu huwezi kuanza kukusanya maoni wakati wananchi hawajaelewa Katiba ya zamani. Najua Watanzania walio wengi siyo wasomaji wa Katiba, walio wengi ni wasikilizaji wa maneno kwamba Katiba inasema mambo kadhaa, sasa tunasema wasome. Naomba Katiba zipelekwe kwa Madiwani wote ili wazisome kadhalika na Watendaji wa Viji wapewe na bahati nzuri leo Waziri wa Katiba na Sheria amejibu vizuri sana wakati akijibu swal, amesema kwamba kuna Katiba zinaandaliwa na amesema kuna Katiba karibu 200,000. Sasa nasema hizo Katiba ni chache ziongezwe. Tunataka Walimu wote wa Shule za Sekondari na Shule za Msingi wapewe Katiba wasome kwa sababu wanaishi na wananchi mahali walipo wataweza kuwaelimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Watanzania, nchi yoyote ukiona ina uchumi uliokamilika vizuri basi ina Katiba nzuri na Katiba ndiyo itatusaidia kuwa na maisha mazuri. Sasa hivi

uchumi unayumba na kila mtu anasema uchumi unayumba, unayumba kwa sababu mambo yamebadilika, sasa na Katiba yetu ni ya zamani hivyo ni lazima ibadilike kulingana na hali ya hewa inavyobadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Muswada, mimi sina tatizo nao, umekaa vizuri na nimeusoma vizuri kabisa lakini labda kuna vipengele vichache ambavyo tukiviangalia, kwa mfano katika Ibara ya 13(6) bahati nzuri kimesharekebishwa, kwamba Sekretariati itakuwa na idadi ya watu lakini hawakuweka idadi wamesharekebisha, hiyo sina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye gharama za uchaguzi ambazo zimeelezwa vizuri kabisa na mjumbe aliyepita kuhusu malipo, amesema Waziri anaweza akaamua kuanza kulipa. Kwa kweli mwenzangu mmoja kasema kwamba Waziri anaweza akaamua analipa tu, akiamka asubuhi anakwenda kulipa lakini ni lazima kuwe na utaratibu wa ulipaji kwa sababu siku ya siku inaweza ikaonekana bajeti kubwa sana imetumika kupita maelezo tukaanza kuuliza maswali mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna watu wengine wanasema Muswada uanze Kusomwa Mara ya Kwanza, jamani hebu tuangalie kwani kuna vitu viwili vy a kuzingatia. Kwanza kabisa ni muda. Watanzania siyo tutasimamisha shughuli zote za kufanya kwa ajili ya kujadili Katiba siku zote, kuna mambo ya kufanya. Kwa hiyo, ni lazima tuzingatie muda na kwa hiyo ni kusonga mbele haturudi nyuma hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba Watanzania wengi sasa hivi tuna matatizo mengi ambayo inabidi tuyatatue, sasa tunaweza tukaacha kufanya shughuli zote tukasema tuna kazi ya kubadilisha Katiba. Hii ni kazi mojawapo ya maisha lakini ni lazima kazi nyingine zifanyike kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naweza nikaliangalia katika Muswada, ni Tume ambayo itakwenda kuundwa baada ya muda mfupi na masuala ya ripoti. Kuna mjumbe mmoja ameshaeleza tayari lazima ripoti itolewe kwa watu ili waweze kujua imeandikwa nini na ili wawe na imani nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla sina mengi zaidi kwa sababu kila nikisoma Muswada naona hauna matatizo, kwa sababu hata vipengele vidogo ameweza kuelezea yaani wame-*define* vizuri kabisa lakini tujitahidi kusoma na katika usomaji mimi nina wasiwasi wa usomaji kwani unaweza ukasoma lakini usielewe. Tukae katika vikundi tusome na kujadili Muswada kwani kuna watu hawauelewi. Huu Muswada hauna shida wala matatizo lakini inawezekana wenyewe tuna matatizo, hatuelewi vizuri, tumesema kwamba huu ni mchakato wa kwanza, tuanze, yaani hii ni *stage* ya kwanza. Sasa nashangaa kuna watu wengi sana wanatumia hata vyombo vy habari wanatoa tafsiri tofauti, Watanzania sasa hivi wanajua Katiba imeanza kujadiliwa lakini Katiba haijaanza kujadiliwa. Halafu nilisikia kuna mtu mmoja akasema kama Wabunge hatutapitisha watakwenda kwa Rais kupinga, wanapiga Katiba iko wapi?

(Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, naamini hata ile laana iliyosemwa jana haitatufikia sote na pia Mheshimiwa Waziri amesikia kwa kuongezwa kopi za Katiba kwa wananchi wote. Naomba sasa kumwita Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Sanya na Mheshimiwa Mushashu wajiandae.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa jioni ya leo japo na mimi kuzungumza machache katika mchakato huu muhimu. Lakini kubwa zaidi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha leo na mimi kuwa katika hadhara hii nikifanya mjadala katika jambo hili muhimu la Katiba yetu ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala zima la mchakato wa kuanza kuweka miundombinu sawasawa ili mradi Watanzania waweze kutoa maoni yao katika Katiba wanayoihitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kabilo letu tuna misemo miwili, bahati nzuri ikachukuliwa katika lugha ya Kiswahili. Msemo wa kwanza unasema "*Kaseteka kaja*" na wa pili unasema "*Kagundumuka kawasala inzala*". *Kaseteke kaja* maana yake amefanya subira akafanya jambo la muhimu. Msemo huo unawagusa moja kwa moja Wabunge wa CCM, wa CUF na wa TLP waliokuwa humu ndani waliofanya subira kwa ajili ya mustakabali wa nchi yao ya Tanzania. Lakini msemo wa pili unasema *Kagundumuka kawasala inzala*, kwamba Kasusa kalala na njaa na wenzetu wakasema ukisusa wenzio nini?

WABUNGE FULANI: Wala!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Wala! Mimi ninapenda kuwaambia Watanzania kwa ujumla kwamba waliobaki ndani ya Bunge hili ndiyo wenyewe kutaka maslahi ya wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Wanasheria wameshasema lakini kama kasema Chenge, Jafo utasema nini? Kama kasema Wasira, Jafo utasema nini? Lakini angalau na sisi tuweze kuweka baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania waelewe kwamba Wabunge waliokuwepo ndani ya ukumbi wa Bunge ambao wote wamekubali mjadala huu uendelee, ni Wabunge waliochaguliwa na wananchi wa Tanzania na Wabunge hawa ni zaidi ya 85% waliokuwepo ndani, nini maana yake? Maana yake ni kwamba Taifa la Tanzania na wananchi wa Tanzania wanakubali kutengeneza Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana mtu anasema kwamba watu wengi hawakubaliani, hao watu wengi ni akina nani? Mimi ni Mbunge wa Kisarawe, wananchi wangu sasa hivi wanataka mchakato uanze ili waende wakatoe maoni yao kwani wana kero nyngi na hivyo kutaka Katiba mpya itengenezwe. Ni nani huyo anayesema kwamba wananchi wa Tanzania hawataki mjadala huu? Nani anasema? Hivi iweje leo hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wananchi wanaishi katika Jimbo la Ubungo au Kinondoni ndiyo waseme kwamba ni wananchi wa Tanzania, hivi kweli itakuwa inaingia akilini? Huu ni upotoshaji wa mawazo ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania kwanza wasipotoshwe katika sentensi hiyo, Watanzania wana akili na uwezo wa kuamua mambo yao ili yaendane sawasawa. Bahati mbaya nakumbuka siku ya Jumapili wengine walisema sana katika vyombo vya habari, wakasema hatutakubali kwa lolote, tutakubali kufa na nini? Ndugu zangu tuangalie falsafa hii pana kwelikweli mtu mpaka anasema sikubali hata kufa tufe. Mtu mzima anaweza kujaji maneno haya katika vyombo vya habari, kuna kila sababu lazima tuijulize maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Malkia mmoja anaitwa Balkis alikuwa akiishi nchi ya Ujerumani wakati ule ikiitwa nchi ya Saba. Wakati anataka kwenda kupambana na Mfalme Suleiman, alipoulima jopo lake la washauri wakasema twende tukapambane na Suleiman, bahati nzuri mwanamama yule akawa na hekima kwelikweli akasema hakika vita vinapotoka watu wanapoteza ufalme, watu wanapoteza mali zao. Hii ni falsafa pana imetolewa na mwanamama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu hao wanaozungumza kwamba tupo tayari kupambana, ina maana kwamba hawatii amri za Watanzania walio wengi ambao ni pamoja na sisi Wabunge ambao tumekuja kuwawakilisha wananchi wetu, ina maana wananchi wetu wote wameonekana hawana maana dhidi ya hao wachache. Naomba Watanzania muelewe jambo hili kwamba tupo katika maslahi ya Watanzania ambao sasa hivi wana kero nyngi, wanataka hii Tume iundwe ili waende wakaporomoshe kero zao kwamba Tanzania inahitaji nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya, napata mashaka mengine, mashaka ninayopata ni kwamba watu watatoa maoni na maoni hayo wanataka yaingie katika Katiba, wengine wakiona maoni ya wananchi hao wataandamana tena watasema tuandamane kwani maoni haya ya wananchi hatuyataki. Mimi nilianza kupata shaka hiyo mapema, watataka kuwahamasisha watu kusema kwamba maoni ya wananchi katika Katiba yamechakachuliwa. Ndugu zangu tusifanye hayo lakini tuijangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania ambao sasa hivi wana shida sana, watu wengine wanaozungumza haya ukimuangalia yeye mwenyewe ameelimika, baba yake ni mfanyakazi, mtoto wake pia ameelimika, amemaliza Chuo Kikuu yaani wamepata fursa zote za maendeleo. Kuna watu wengine ambao ndiyo wana kero halisi wanataka mchakato huu uanze mara moja, wakatoe kero zao, watu wanasema kwamba hakuna mchakato kuendelea. Nasema kama Watanzania tusikubali jambo hili liingie katika Taifa letu. Tujifunze kutoka kwa Mataifa mengine, tuangalie hali ilivyokuwa Libya, mwananchi wa Libya hata kama alikuwa mfanyabiashara maana yake siyo Mlibya yule tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba ikitokea vurugu yoyote katika nchi kwa mfano Dar es Salaam, ndugu zangu Wachaga mmejaa na mna maduka mengi sana. Biashara yako itaharibika na wewe utakuwa maskini hata kama ulikuwa na elimu, unafanya kazi katika *NGO* hiyo *NGO* maana yake itakuwa haifanyi kazi, maana yake utakuwa huna kazi. Lakini watatokea Wasela wanajita Wasela wa mitaani ambao wamechakachuka na akili zao zimekuwa mbaya, hao ndiyo wataanza kushika hatamu za miji mikuu yote kwa sababu hawana elimu, wataona wamenyanyasika na wataona sasa huu ni muda wetu, hatuna elimu wala hatuna fedha maana yake fursa yetu ni kuingia mitaani na kufanya vurugu, Tanzania itabadijika kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania wenzangu kuona kwamba linalofanya hapa ni kwa ajili ya mustakabali wa Tanzania na Watanzania wote wameamua katika jambo hili. Mimi napenda kuishukuru sana Serikali kwa sababu imeona kwamba sasa hivi nchi imebadilika. Mheshimiwa Rais siku ya mwaka mpya tulipoingia kipindi kile alitangaza rasmi kwamba sasa mchakato wa Katiba Mpya Tanzania tunaingia katika miaka 50 ya uhuru tuweze kujipima katika kuanza mchakato mpya ili tupate Katiba ya Tanzania. Hili ni jambo la faraja kubwa sana na ninapenda kumshukuru Waziri mwenye dhamana kwa kulihangaikia suala hili lakini pia napenda kuishukuru vilevile Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu zangu muelewe kwamba Muswada huu ulivuosomwa Mara ya Kwanza, wananchi walitoa kero na hamasa zao kwamba nini kifanyike katika *amendment* ya Muswada huu. Kuna watu wengine nakumbuka mpaka walifikia hatua ya kuchana Muswada ili kuonyesha hisia zao. Angalieni katika *schedule of amendment* hisia zao zimepokelewa, zimeingizwa katika Muswada uliokuja hapa. Mwanzo *Terms of Reference* hazikuwepo lakini sasa hivi zipo katika Ibara ya 9 na 16, je, tunataka nini? Uki muona mtu mwingine ana wasiwasi basi huyo ana *agenda* ya siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaomba vijana wenzangu tusije tukaongopeana kwani wengine mama zao wanafanya kazi katika *NGOs*, baba zao wanafanya kazi sehemu mbalimbali lakini sisi ambao tunasema kwamba umevaa suruali tatu lakini nguo za ndani zinaonekana ndiyo tutakaopata shida katika Taifa hili. Tusikubali hata siku moja mawazo ya watu wachache eti ndiyo yatengeneze mustakabali wa nchi hili, tusikubali hata siku moja. Naomba Tanzania yenye heshima iendelee kubaki yenye heshima kuhakikisha kwamba tunaingia mahali ambapo Tume inaundwa na maoni ya wananchi yanachukuliwa na naomba kutahadharisha sana kwani kuna wengine watakuja kutudanganya tusitoe maoni yetu, naomba tujipange ili kuhakikisha kwamba tunatoa maoni yetu kwa ajili ya mustakabali wa Katiba yetu tunayoihitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20 inazungumzia jinsi gani mchakato utafanyika, jinsi gani Wabunge wa Katiba watakavyopatikana. Naomba nishauri kwamba katika kipengele kile vijana watajwe kama nao ni miongoni mwa watakaoshiriki moja kwa moja siyo makundi maalum. Katika Taasisi za Elimu ya Juu, ikiwezekana watajwe kabisa miongoni mwa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu waweze kushiriki. Naomba na walemvu watajwe kabisa. Walemvu siyo watu

wenye mahitaji maalum, naomba watajwe kwamba, kundi la walemavu ni mionganoni mwa washiriki. Maana yake ni nini! Ni kwamba, Katiba hiyo tunayoihitaji tunaenda kulenga iwe Katiba shirkishi kwa ajili ya mustakabali wa Tanzania yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapo mwanzo kwamba, mimi sikuja hapa, Mzee Chenge katufungulia kifungu mpaka kifungu, Wassira amemaliza kazi, Mama Jenista Mhagama, ametoa semina hapa ya darasa kwa Tanzania. Mimi nataka kusema, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Muhammad Sanya, Mheshimiwa Mushashu, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Eugene Mwaiposa na Mheshimiwa Sereweji pia wajialande.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo kuhusu mustakabali wa Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ilikuwa unipe nusu saa kwa sababu kuna watu wanabeza maslahi ya nchi kwa kuibezza nchi iliyomo katika Muungano wa nchi mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa Kiswahili unasema, 'Mwenda pezi na omo hurudi ngamani'. Wenzetu hawa watarudi, wala wasitutie wasiwasi. Desturi ya Mama anavyoandaa chakula kwa mwana na mwana akawa analia kwa njaa, Mama huwa hashughuliki na kilio chake, hashughulika na namna ya kuandaa chakula cha kumnyamazisha mwana kwa kumpa chakula. Kwa hivyo, sisi tutawanyamazisha kwa kuwatengenezea hiki chakula tunachokitengeneza kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa akili na mantiki ya kawaida, mtu mzima aliye muungwana anapofanya uungwana, basi uungwana humrejea mwenyewe na kuonekana kwamba, yeye ndiye muungwana. Unapokuwa una kiongozi wa nchi, kiongozi anayetawala madaraka aliopewa na wananchi, ni vibaya sana na una mdhulumu hata kidini kwa kumkashifu na kumvunja heshima yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano, niliwhi kusema na nitasema tena, na nitaendelea kusema, Kikwete mtamkumbuka atakapoondoka madarakani. Hata kama amekaa na washauri wake kushauriana nao, lakini alikuja na tamko la kwamba, Tanzania ipate Katiba Mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu hawaelewi nini maana ya Muungano. Katiba tuliyonayo inasema kwamba, Jamhuri ya Muungano inatokana na Katiba yenye na Muungano ni wa nchi mbili kwa hiari zetu. Kilichokosekana ni watu kukosa taaluma ya kuelewa na ni makosa yetu kwa upande mmoja viongozi kutowaelimisha kwamba, sisi sasa hivi tunachotengeneza ni mustakabali, mwenendo mzuri wa kuelekea huko ambako wananchi wanakutaka kwa kutengeneza Katiba. Hii ni *incubation period*, tuna yai sasa hivi linahitaji *heat* ili liweze kutotoa huyo kuku. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nastaaajabu sana na ni mambo ya ajabu Muswada uliletwa hapa tukaurudisha kwamba haukidhi haja na *public hearing* ikafanyika Dodoma, Dar es Salaam na ikawa isipelekwe Zanzibar. Mimi ndiye niliyesimama hapa kumwombwa Mheshimiwa Spika kwamba, sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano, nako ipelekwe. Akakubali na ikapekekwa Zanzibar na ikafanyika Bwawani na katika Skuli ya Haileselasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ukaanza mchakato, mwanzo mpya wa kujenga himaya ya kutambua kwamba, Katiba hii haiwezi kukamilika isipokuwa viongozi wa nchi mbili washirikishwe kikamilifu kutengeneza rasimu ya Muswada ambao tunaujadili leo. Akatoka Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Waziri wa Katiba na Sheria na Makatibu wao. Zanzibar nako wakatoa viongozi kama hao; Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Katiba na Sheria na Katibu wa Wizara, wakakaa wakajadili wakatengeneza kitu kizuri wakatuletea sisi humu ili kuelekea huko kwenye mchakato wa kutafuta hiyo Katiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa dhambi iko wapi? Tuelewe kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano hajafaa, ile tuliyokula nayo kiapo ipo na ndiyo hiyo inayotufanya tukabaki ndani humu tukijadili huo Muswada kwa kutengeneza Katiba nyingine. Kama ingekuwa haipo tusingekuwepo humu ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Katiba iliyopo ambayo sisi tunataka tuifanyie marekebisho kwa pande zote mbili za Muungano ikapelekwa kwa viongozi wetu na Mheshimiwa Spika tusimlaumu, kwenye Kamati ile akaongeza baadhi ya Wajumbe amba ni Wabunge kwenda kusaidia ili kipatikane kitu ambacho kitatufaa kwa maslahi ya nchi yetu. Walikwenda na haikumalizia hapo tu, Kanuni zetu zinaturuhusu Mbunge ye yeyote anaweza akahuduria katika Kamati yoyote inayokaa katika Bunge hili. Nani alizuiliwa asiende? Nenda kasikilize, toa maoni yako utakachokosa ni kupiga kura tu. Baadhi ya Wabunge wamehuduria na ni Wanasheria maarufu na waliobobe. Mheshimiwa Chenge yule pale alikuwepo, hakatai na ameiridhia hii na yeye amechangia hapa. Sasa kitu gani kinatubabaisha sisi? Mambo gani yanatufanya sisi tuogope kutengeneza kitu ambacho kina maslahi na nchi yetu? Kama wewe utakuja kusema; haya, tunataka Sukuma *land* yetu, *okay* nendeni mka sema kwenye kura ya maoni huko. Wazanzibari tunataka nchi yetu, tutazungumza wakati ukifika. Ukerewe tunataka visiwa vyetu tuungane na Uganda, haya! Eeeh, si ndiyo maoni halafu yataratibiwa, halafu itapatikana rasimu! Lakini hapa siyo mahali pake, hapa tunatengeneza tu mwelekeo '*the way forward*', '*road map*' ili tufikie huko tunakotaka. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa isije nikaliwa sana na muda, nasema kwamba, kama hizi hadidu za rejea, unapokwenda ukurasa wa 31 unakuta kitu kinasema hivi; bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kushughulikia jambo lolote kama itakavyoona inafaa katika kutekeleza majukumu yake. Ndiyo hapa mka sema ooh, mamlaka yote anayo Rais. Mamlaka yameingia kwenye Tume huku na wanawenza wakafanya mabadiliko kwa namna wanavyoona inafaa bila hata kushauriana na Rais. Sasa mnataka nini zaidi! Kitu muhimu cha kuzingatia na hicho tulikubaliana kwa pande zote mbili kwamba, wakati utakapofika *two thirds majority* ipatikane kwa pande mbili za Muungano yaani Zanzibar na upande wa pili wa Muungano yaani Tanzania Bara au Tanganyika kwa jina lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuja kwenye Muswada huu, ukurasa wa 30 hapa kuna Uundaji wa Tume. Nachositiza hapa ni kwamba, kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3), muundo wa Tume utazingatia msingi wa kuwepo kwa uwakilishi ulio sawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano, yaani ile *two thirds majority* na hii *two thirds majority* hajji tu kwa Katiba Mpya, hata hii Katiba tuliyonayo kama tutataka kubadilisha ama kwa kuongeza au kupunguza kitu lazima tukutane pande mbili na kila mmoja aipigie kura katika ile ile *formula ya two thirds majority*. Isipokuwa nachotaka kusitisiza hapa ni kwamba, huyu Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, Tume wenywewe wapewe nafasi wawachague. Ama Mwenyekiti akitoka Zanzibar, Makamu Mwenyekiti atatoka upande wa pili and *vise versa*. Hivyo hivyo kwa Ibara ya 7(1) kwamba, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, vilevile wateuliwe na walewale wajumbe katika ishirini (20) na thelathini (30).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalisisitiza ni hali ya kifedha katika ukurasa wa 33, kwamba, ni Waziri gani afafanuliwe na ijulikane ni namna gani watakavyolipwa kulingana na sheria na kanuni za nchi. Kwa sababu hii sheria inasema gharama za shughuli za Tume wakati wa mchakato wa mapitio ya Katiba zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Lakini nani atalipa, Waziri wa Fedha? Waziri wa Katiba na Sheria? Ifafanuliwe ili tujue nani mlipaji na kwa sheria gani ili pasije pakawa na msongamano wa kwamba, fedha hazipo, fedha hazijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nasema sisi kama Wabunge *as a team work*; CCM, CUF, CHADEMA na wengineo, tuwashauri wenzetu hawa, mimi siamini kwamba, wote wanapinga, kuna watu wanaunga mkono hili lakini wametoka tu kwa sababu ya mambo ya kisiasa, tuunge mkono kwa hili kwa sababu tunajenga mustakabali wa nchi kwa kutafuta Katiba Mpya. Sasa hii Katiba ikishapatikana itakuwa na pande zote za Muungano. (*Makof*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Nakushukuru kwa mchango wako.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema nipewe nusu saa, ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Hujatamka kama unaunga mkono Muswada!

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Naunga mpaka dakika ya mwisho na nitasimamia wala sitakwenda mahali mpaka nihakikishe Katiba inapatikana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana kwa hilo. (*Makofî*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bernadetha Mushashu, ana dharura, amekwenda hospitali.

MWENYEKITI: Naomba kumwita Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine, mwelekeo wangu utakuwa tofauti kidogo na walitangulia, si katika maudhui lakini katika mwelekeo wa yanayotukabili mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachowajibika ni kuweka hoja zetu mbele katika jambo linalotukabili ili wale wenzetu ambao tayari wameambiwa hoja za upande wa upinzani waweze kupata dhahiri hoja za upande mwininge. Mpaka dakika hii, tunangojewa kwa kiasi kikubwa sisi tunasema nini katika hoja zilizowekwa na wenzetu. Katika hili sasa ni jukumu letu kusema tunasema nini katika hoja zile ambazo ziliwakilishwa na upande mwininge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kwa harakaharaka kusema yale ambayo nafikiri yalikuwa ya msingi, yaliyosemwa na upande mwininge, halafu la pili nitagusia yale ambayo nafikiri tunahitaji kuyaboresha katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa upinzani, hoja yao kuu ya kwanza walisema Muswada huu Usomwe kwa Mara ya Kwanza kwa sababu Muswada uliopita kwa maagizo ya Bunge liliopita kuititia Spika haukupata nafasi stahili. Naomba unipe...

MWENYEKITI: Mheshimiwa upande wa upinzani au upande wa CHADEMA?

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe ruksa niweze kunukuu harakaharaka. Katika hilo walisema Serikali ilagizwa muda zaidi utelewe, Muswada uchapishwe upya na kwa lugha zote pamoja na Kiswahili na utangazwe katika vyombo vya habari vinavyosomeka kwa wingi. Vilevile utangulizi wa Muswada huu uwekwe vizuri zaidi ili wananchi waelewe madhumuni ya Muswada. Katika hili la kwanza wakahitimisha kwamba, hakuna hata moja ya maagizo haya ya Bunge ambalo limetekelizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili si sawa. Tumepata majibu kutoka wasilisho la Waziri wa Katiba, ameeleza kwa kirefu namna gani Serikali ilivyofanya mpaka hapa tulipofikia kwa kuititia mchakato wa Kamati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tunalo jibu na hivyo si sahihi kusema kwamba, hili halijafanyika. Hili limeishanyika na tena kwa urefu na kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili walisema kwamba, Muswada huu ni mpya una tofauti kubwa na za kimsingi na Muswada wa zamani na akatoa na mifano kwamba, upya huu unastahili kuletwa kama *First Reading*. Nasema hoja hii si sahihi kwa sababu mbili kubwa; Muswada kuwa mpya maana yake ni kubadilisha mambo makuu matatu. Jambo la kwanza kubadilisha maudhui ya Muswada, halafu la pili kubadilisha *structure* na jambo la tatu kubadilisha madhumuni. Vyote hivi bado vipo, kilichobadilishwa ni uboreshaji wa Muswada kulingana na mahitaji ya mchakato, lakini Muswada wenye haujabadilishwa kwa sababu hivyo vitu vitatu havikuguswa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbakiwa na madhumuni yaleyale, maudhui yaleyale na *structure* ileile, lakini kilichobadilishwa ni maboresho. Kwa hiyo, Muswada haukubadilishwa na katika sababu hiyo hatuhitaji kuichukua kama ni hoja ya kuanza upya kwa sababu haikidhi vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, walihoji sababu nydingine ni kwamba, Muswada unazungumzia uwakilishi ulio sawa na umeletwa kinyemela, kwamba, kipengele cha *fifty percent (50%)* kimebadilishwa na kimeletwa cha kificho ambacho kinazungumza *ratio*. Lakini hili nalo siyo sawa kwa sababu hakuna badiliko, ukibadilisha kutoka *fifty percent* ukaleta *ratio* hujabadilisha kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, walisema Muswada unampa Rais, majukumu makubwa bila ufanuzi wa hadimu za rejea, yaani *terms of reference*. Hili nalo si kweli kwa sababu Waziri husika wa Katiba ameisha *move a schedule of amendments* na ameweka *sections 9* na *16* zisomeke kama *terms of reference*. Kwa hiyo, hii nayo si sababu ya kuukataa Muswada kwa sababu tayari limeshatekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wamehoji kwa kitu kinachosema Urais wa Kifalme hauruhusu kupatikana Katiba ya Kidemokrasia na kwamba katika mchakato huu mamlaka kubwa sana imewekwa mkononi mwa Rais na kwa hakika hali hiyo haki haitatendeka. Napenda niliseme hili kwa kirefu kidogo, kwa sababu hili ndilo liliopelekwa hewani ambalo linagonga vichwa vya watu. Kuna mwelekeo wa aina tatu duniani katika kutunga Katiba. La kwanza, ikiwa nchi ilikuwa katika vita basi mwelekeo huwa wa pande zote kuzikutanisha na kuwa na wawakilishi wanaowakilisha makundi hayo, nchi hii haijawa katika vita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ikiwa nchi imekuwa katika makundi mbalimbali ambayo ni hasimu kwa maana ya *highly competitive political environment*, kwa hiyo makundi hayo hutengenezewa utaratibu wa kuyawakilisha kwa sababu yanaweza yakaharibu mwenendo wa usalama wa nchi, sisi nchi yetu haina jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo sisi tunautumia sasa ni kwamba tuko katika hali ya tatu ambayo ni hali ya kawaida na hali hii ya kawaida ni *one side of a political party* ikiwa ina-command *high political popularity* na hiki kigezo chake ni huko tulikofanya *General Election* kwamba kama Rais aliyeupo alipata zaidi ya asilimia 60 ya ushindi maana yake *popularity* yake ni kubwa na ana *mandate* ya kuweza kupewa mamlaka ya kusimamia *system process*. Sasa kwa vigezo hivi Rais ambaye ndio Rais wa nchi hii na aliyepatikana katika hali hii hawezu kuitwa ni *dictator* kwa sababu ana *mandate* ya *political popularity*.

(*Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufinyu wa muda, naomba niishie hapo na kwa sababu kengele imeshagongwa. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na Mheshimiwa Sereweji na Mheshimiwa Mussa Zungu wajiandae.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Kutunga Katiba Mpya ambayo iko mbele yetu. Lakini baada ya shukrani hizo pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kusimama hapa na kupata nafasi hii. Kama wenzangu walivyotangulia, nimshukuru sana Rais pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kufanikiwa kuleta sheria hii kwa wakati muafaka. Niipongeze sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Baada ya kujielekeza na kumaliza kutoa shukrani hizo, niombe tu njielekeze moja kwa moja katika Muswada wenyeewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa Muswada huu au Sheria hii, ninayo maoni machache kama ifuatavyo. Katika kipengele au katika masharti ya utangulizi, katika kile kipengele cha 3 ambacho kinazungumzia tafsiri ya maneno, pale mwisho kuna 'maoni ya wananchi', maana yake ni mawazo, maoni, fikra, taarifa, mapendekezo na kadhalika. Nilikuwa natoa maoni kwamba kwa sababu neno "maoni" ndilo linaloelezewa basi litoke katika maelezo yale yanayoendelea pale. Kwa hiyo ibaki tu kwamba maana yake ni mawazo, fikra, taarifa au mapendekezo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee pia kwenye Sehemu ya Pili ya madhumuni. Katika eneo hili la Ibara ya 4, napenda nijikite zaidi katika kile kipengele cha "e" kwamba Sheria hii ina madhumuni ya kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa mapana katika kutoa na kuwasilisha maoni yao kuhusu Katiba. Nimependa kujikita katika jambo hili kwa sababu ndilo haswa ambalo linaleta utata. Ninazungumza hasa nikitaka kuwaeleza wananchi wa Tanzania kwamba watakapoona mchakato wa kukusanya maoni umekaribia wahakikishe kwamba wamerukia fursa hii ili waweze kutoa maoni yao na maoni yao yaweze kuwa yamewekwa katika Katiba ya Nchi. Nimezungumzia hili kwa sababu, nina uzoefu mkubwa kwa Watanzania katika kuzembea baadhi ya mambo ambayo ni muhimu. Uzoefu wangu wa kwanza ni wakati tulipoambiwa kwamba tukasajili laini zetu za simu. Tulipewa muda wa kutosha, lakini siku zile za mwisho ilionekana kwamba asilimia kubwa ya wananchi walikuwa hawajajisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uzoefu mwingine wa kujandikisha katika Daftari la Wapiga Kura, tulipewa muda wa kutosha lakini mwishoni kabisa umma mkubwa ulijitokeza na kudai kwamba walikuwa hawajajandikisha. Kwa hiyo, kwa kuangalia tu uzoefu wa hayo mambo mawili uknipa wasiwasi kwamba Watanzania wanaweza wakachelewa kurukia fursa hii ya kwenda kutoa maoni yao katika sehemu ambazo zitatangazwa kwamba wanatakiwa wafike kwenda kutoa maoni yao. Kwa hiyo, naomba sana wananchi wa Tanzania na Jimbo la Ukonga hususan wahakikishe kwamba wanakwenda kutoa maoni yao tena siku zile za mwanzo bila kungojea muda wa mwisho. Lakini niombe Serikali kwamba ihakikishe hili linafanyika, kwamba wanatoa utaratibu mzuri kwa kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi hasa vijijini wamefikiwa kwa ajili ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee tena katika Muswada huu kwenye ile Sehemu ya Tatu kuhusu uundwaji wa Tume. Katika ile Ibara ya 5 pale inaonekana kwamba Rais atashauriana na Rais wa Zanzibar lakini pamoja na Wanasheria Wakuu. Nilikuwa naona kwamba kwa maoni yangu kwa sababu kazi ya kumshauri Rais ni kazi ya Mwanasheria Mkuu basi ibakie kazi kama kazi na isionekane katika Muswada huu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee katika kipengele cha 3 pale katika kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, Rais atazingatia masuala yafuatayo. Katika kile kipengele cha (a) amesema kwamba atatumia uzoefu katika kufanya mapitio ya Katiba na sifa za Kitaaluma za Wajumbe kwenye mambo ya Kikatiba, Sheria, Utawala, Uchumi, Fedha na kadhalika. Hapa nataka nishauri kwamba hebu iwekwe wazi kwa sababu watu wengi ambao wana taaluma hizi ni watu aidha wameajiriwa na Serikali au wanafanya kazi katika Taasisi mbalimbali. Ingewekwa tu wazi kwamba je, hawa watu wakibahatika kuingia katika hizi Tume je, wataachia nafasi zao zile za kwanza ili waweze kutumika kikamilifu katika nafasi hiyo mpya watakayoipata? Naomba hapo tupate ufanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukisogea chini hapo kuna ile Ibara ya 4 pale inazungumzia kwamba bila ya kujali kifungu kidogo cha 3, mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa katika Tume kama hatakuwa na vipengele hivi ambavyo vimeainishwa hapa. Mimi nilikuwa na wazo hapo kwa

sababu mpaka sasa hivi ipo mijadala inayoendelea na kwa sababu wako watu ambao tayari wamekwishakuonyesha mawazo yao kuhusu Katiba basi watu hao hata kama wana zile sifa ambazo Rais anafikiria kwamba zinafaa wawekwe pia katika kipengele hiki. Kwa hiyo, wakose sifa moja kwa moja ili isaidie kutoku-*influence* watu au wananchi wakati wakiwa kwenye mchakato wa kukusanya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika Ibara ya 7, kipengele cha 2 pale kuna uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu. Hapa inaonyesha tu ni namna gani watateuliwa, lakini ni nani atawateua watu hawa wawili katika sheria hii nzima ya Muswada hakuna mahali ambapo pamonyesha kwamba ni nani anawateua isipokuwa tu Katibu ndiye anaonekana kwamba yeye atateuliwa na Rais. Lakini pia katika Wajumbe wa Tume, nilikuwa naona kwamba pia hata Katibu awepo kwa sababu anaambiwa kwamba atawajibika kwa Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisogee kidogo katika Ibara ya 8 hapo, inazungumza kuhusu hadidu za rejea. Katika mstari wa mwisho unasema kwamba, kwenye ile Ibara ya 8 kipengele cha kwanza, Tume inatakiwa kukamilisha na kuwasilisha ripoti. Hapo nilikuwa naona kwamba kipo *loose* kidogo, itakamilisha lini hiyo ripoti, wangewekewa muda kabisa kwamba muda fulani hiyo ripoti itakuwa imekamilika kwa sababu hii ni *document* ya kisheria zaidi, ni vyema wakawekewa muda wa kumaliza kazi na kukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tisa, kwenye Ibara ya 9 kazi za Tume pale kwenye kipengele (d), kinasema kuandaa na kuwasilisha ripoti. Nilikuwa nafikiria kwamba badala ya kuacha hiyo sentensi iwe *loose* basi iweze kusomeka kuandaa na kuwasilisha ripoti kwa wakati uliopangwa, kisiachwe tu *loose* hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tena Ibara ya 18, kwenye kipengele cha kwanza kinachozungumzia uwasilishwaji wa ripoti ya Tume kinasema, baada ya Tume kukamilisha kazi yake ripoti hii itawasilishwa kwa Rais na Rais wa Zanzibar. Kipengele hiki naomba tu nacho kiwe na muda, ni lini watawasilisha lakini pia kuwepo na muda kwamba baada ya Rais kuipokea ile ripoti itachukua muda gani kushauriana na Rais wa Zanzibar mpaka aje kuitisha Bunge la Katiba, hapo pia muda usiwe *loose* sana nilikuwa nashauri tupate muda haswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo naomba niende kwenye kipengele...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mussa Zungu ajiandae na Mheshimiwa Shah muda ukiruhusu atapata nafasi.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhana Watawallah*, kwa kuturuhusu leo kuendelea na mchakato wetu huu. Lakini nimwombe tena atusaidie mchakato huo twende kwa salama na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano tuiweke kwa salama na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtu niliyefurahi au tuliofurahi ni sisi hasa Wazanzibar, lakini ni wajibu wa Watanzania Bara vilevile wafurahi. Jambo la mwanzo, kila mmoja alikuwa anauliza Muungano wa Zanzibar na Muungano wa Tanzania Bara ameuweka nani? Hata wengine wakawa wanathubutu kusema kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume. Hayo yalikuwa yanaseemwa katika Bunge hilihili Tukufu. Wengine walikuwa wanahoji mkataba wa Muungano huu uko vipi? Lakini baada ya nusu karne, miaka 50 ya uhuru, tunakuja na Katiba Mpya. Nashukuru zaidi kama Katiba hii itapita, hakuna hata mtu mmoja atakayemnyooshea kidole mwenzake, kwa nini basi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru tena Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete katika Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano Wazanzibar si wadau kabisa maana mdau unamwita unamsikiliza akimaliza anakwenda zake. Lakini Wazanzibar ni wenyewe kwa sababu wana nchi na hii ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Ina maana tunaiweka Katiba, Katiba hii kutakuwa na watu 116, katika watu 116, Wazanzibar wamo na wa Bara wamo. Kutakuwa na Tume ya watu 20 mpaka 30, Wazanzibar wamo na wa Bara wamo. Lakini vilevile kutakuwa na Bunge la Katiba, wawakilishi wote wanaingia halafu kuna watu 116 ambao hawa watatoka Zanzibar na Tanzania Bara. Hapa tungeomba kwamba watu 116, Rais aachwe huru kabisa bila ya kushauriwa na mtu yejote. Kwa hiyo, baada ya Katiba kupita hakuna atakayeuliza Muungano huu ameuvweka nani, itakuwa ni Muungano wa Zanzibar, Muungano wa Watanganyika hatimaye tunalipata jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa yule anayesema kwamba Zanzibar kwa nini wawe wadau, Zanzibar sio wadau ni wenyewe. Kwa sababu katika Katiba hiihii tukasema jamani tumechoka basi. Sasa lingine ninalolisema sababu ya Zanzibar kupewa Serikali yake viongozi wetu walikuwa waungwana, Zanzibar ni ndogo inaweza kumezwa wakati wowote kama jina la Zanzibar haliko lakini Bara, Zanzibar hatuwezi kuimeza. Kwa hivyo historia ya Zanzibar ibaki palepale Serikali yake iwepo. Sasa wasiojua hilo walijue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu gazeti la Nipashe la leo, linasema hivi "CHADEMA hatushiriki Katiba Mpya kuungana na NCCR kuwasho moto nje ya Bunge, CCM, CUF wawashambulia". Wanawasha moto Tanzania lakini si wao tu ningeomba mtazame juu kuna Mwandishi gani wa Habari kule? Kinachoendelea mbona wamezingia CHADEMA ya ndani hawayajui. CHADEMA wanataka Serikali waimmomonyoe lakini ninalosema usicheze ngoma ambayo hujui na wala wimbo wake huuji. Tusome alama za nyakati jinsi gani Bara la Afrika linavyomomonyoka na nani analimomonyoa. Kwa hivyo nawaambia Watanzania, CHADEMA ni mtu wa mwanzo ambaye anamomonyoa amani na utulivu. Nilivyosoma sijui sasa wanaosoma wanasemajie, sifa kuna mbili tu, sifa ya mwanzo mbaya sifa ya pili ni nzuri. Mtu anauliza ana sifa gani? Sereweji ana nini. Sereweji ana moja, mbili, tatu, ana sifa nzuri. Huyu ana sifa gani, moja, mbili, hii mbaya. Sasa sifa ya Jamhuri ya Muungano amani, utulivu, usalama na ushirikiano, kuna nchi hawaitaki kabisa historia hii, inatakiwa kuondoshwa na walioweka historia ni Watanzania na Chama cha Mapinduzi na wananchi wetu kwa pamoja. Sasa wako watu ambao wanataka watajwe kwa historia hii ya kuondosha, watajwe ni watu wa mwanzo kuondosha amani na utulivu, nao ni CHADEMA. Kama kitendawili hicho hamkijui, mimi nimeshakieleza, kwamba CHADEMA hawatutakii mema, wanataka kuondoa mahusiano yetu yaliyokuwepo. Usemi wa Kijeshi unasema hivi "ukiwa na adui ukimenga piga, ukirejesha anakupiga", kwa hivyo, ninalosema Serikali na wapenda amani tulenge na tupige tukirudisha tumemalizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna hata moja tutakalolifanya dhidi ya CHADEMA likawa zuri. Lakini nawaambia CHADEMA wasiwe na upinzani wa mke mwenza kwa sababu mke mwenza hata afanye nini kwa mwenziwe atataka liharibike na likiwa zuri hasifu. Kuna hadithi moja inasema hivi; mwanamke alifuatana na shoga yake, yule mama akaliona kaburi, baada ya kuliona kaburi akalisifu kaburi hili kila nikipita hakuna majani japo hakuna jua panakuwa na kivuli, ndege wazuri wanaimba, huyu mtu wa peponi. Shoga yake akamwambia hulijui, akajibu silijui. Hili ndo lile la mke mwenzako. La nalionna pembedi limekaa vibaya na pale lina tundu kwa chini, sijui kama nyoka hajakwenda mwadhibu. Kwa hiyo na sisi CHADEMA hata tufanye nini hawatutambui, hawatujui hata kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hamaki za CHADEMA kukosa Jimbo, kukosa Madiwani na kura nyingi za urais Zanzibar, wasiitukane Zanzibar kwa sababu hiyo. Kwa sababu Zanzibar tunajua hili baya, hili zuri na mkutano wao wa mwanzo waliofanya walihadaika sana kwa sababu walikwenda watu wengi sana na baada ya kuondoa wakaambwa wembe ni ule ule, hatumjui CHADEMA. Hili ndilo liliofanya CHADEMA ikasirike. Kwenye Bajeti kaitukana Zanzibar, leo kaitukana Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuwaambia Watanzania wote, leo hatupitishi Katiba. Tunapitisha muundo ambao utaratibu mchakato wa kuwatafuta watu watakaofanya kazi pamoja na twende vipi mpaka kuipata Katiba yetu. Muundo wenyewe ndiyo huo niliosema

Wazanzibar watakuwemo, hatimaye moja kwa moja tunakwenda vijjini kupata maoni ya wananchi. Sasa hapo Katiba iko wapi? Kwa hiyo, tafadhalini Watanzania, msije mkajuta, ghasia zina watu wa namna mbili. Watu wa mwanzo watakuwa wanalenga lile walilokataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahma Rahim*. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa mazungumzo ya jana na leo, nina uhakika wananchi wameshaelewa nia njema ya Serikali, nia njema ya Rais kutaka kuuleta Muswada huu ukiwa kama ndio barabara na watumiaji wa barabara hiyo ni wananchi, sio vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitasoma ukurasa wa 27 wa Muswada huu unavyosema. Sheria hii ni kwa ajili ya kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba, kuanisha na kuchambua maoni ya wananchi, si maoni ya vyama, maoni ya wananchi, si maoni ya wanaharakati, maoni ya wananchi wenye nchi ambaeo wapo juu ya Bunge na wapo juu ya Katiba, wananchi. Ndiyo Muswada huu unavyosema. Sasa kama kuna watu wanataka kupotosha Muswada huu kwa maslahi yao tu, si jambo jema kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea kusema kuanisha masharti kuhusu Mabaraza ya kuhalalisha masharti yaliyomo kwenye Rasimu ya Katiba, kuweka masharti juu ya utayarishaji wa uwasilishaji wa ripoti ya wananchi lakini hapa inajengwa hoja ni kwamba Muswada huu kujadiliwa na watu wa CCM au una lengo au maana kwa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Muswada, Ibara ya 20 inaeleza kabisa kuundwa kwa Bunge la Katiba, tatizo liko hapa. Lipo vipi? 20(1) inasema: "*Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar na kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ataunda Bunge la Katiba.*" Hapa hawataki kusema wajumbe ni nani, wenzetu hawataki kusema. Sisi tutawosome na wananchi msikilize Wajumbe watakaouna Baraza hili, iweje Baraza hili lenye heshima liunde Katiba Mpya halafu wanasema Rais akipata ripoti attachakachua? Haya ni mambo ambayo si ya busara kabisa. Tunaomba wenzetu warudi na warekebishe kauli yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo inasema hivi, bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) Bunge la Katiba litakuwa na wajumbe wa aina zifuatazo, wananchi sikilizeni, kwanza, Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, tatizo lipo hapa. Kwa nini Wabunge wote ambaeo asilimia kubwa ni CCM? Ndiyo walioridhiwa na wananchi. Hakuna Mbunge wa CCM aliyekuja hapa kwa kuchaguliwa na mke wake, amechaguliwa na wananchi. Kama CCM imepata 259, ninyi mmeputa 48 wenye wivu wajinyonge. Pili, Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar. Tatu, Mawaziri wenye dhamana ya mambo ya Katiba wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nne, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Tano, Wajumbe 116 ambaeo watateuliwa kutoka Asasi Zisizokuwa za Kiserikali na wao wataingia kwenye Bunge la Katiba, watateuliwa Asasi za Kidini na wao wataingia kwenye Bunge la Katiba, Vyama vya Siasa vilivyo na usajili wa kudumu na wao wataingia kwenye Bunge hilo, Taasisi za Elimu ya Juu na makundi yenye mahitaji maalum katika jamii. Wote hawa ndiyo watakaingizwa kwenye kundi hilo la Bunge la Katiba. Sasa tatizo liko wapi? Hivi watu wote hawa wanaokula kiapo, watapitishwa kwa ajili ya kuitisha Katiba hii na wenye Mamlaka ya kuikubali Katiba hii, ni wananchi watakubali, kweli Rais achakachue ripoti yao? Si watasema hawa, Vyama vya Siasa si vitaingia humu ndani na kusema jamani hili silo tulilopeleka kwa Rais? Hofu iko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa fursa kwa wananchi wa nchi yetu, hii ndiyo fursa muhimu na nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake, uadilifu wake na upenzi wake kwa nchi yake. Hii ndiyo fursa sasa hivi ya wafanyakazi kudai maslahi yao katika utaratibu wa Katiba Mpya, hii ndiyo fursa kwa Serikali yetu na wananchi wake kuweka kwenye Katiba Mpya masuala ya madini na rasilimali za nchi yetu, hiki ni kipindi cha kina mama kudai haki zao ndani ya Katiba hii

mpya kwa kupewa nafasi ya kutoa mawazo yao, ni namna gani nchi hii iwajali akina mama na watoto walemvu na makundi yasiyokuwa na nafasi. Nafasi hii tusiache, wenzetu kuna watu wanagombana, leo sisi tunaingia tunaandaa Muswada wa kuruhusu sasa Sheria watu wapite wachukue maoni ya watu lakini kuna baadhi ya watu na michango yao ambayo ingekuwa mizuri kuusaida Muswada huu wametupilia mbali. Wamekosa nafasi ya kuwasilisha maoni muhimu ambayo hata sisi na Serikali ingeweza kuyachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu. Juzi tumepitisha Sheria ya Ununuzi, Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Upinzani, asilimia 98 ya marekebisho ya Sheria ile yamekubaliwa na Serikali. Serikali imetambua ule mchango. Tunajenga nchi, hatujengi vyama, tusitafute kuwa *object of pit* kwa watu kuwadanganya, watu wananyanyaswa. Haya majukwaa ya Katiba yanapotosha watu katika nchi yetu. *Leadership is ability, leadership is about responsibility.* Uongozi si uwezo, uongozi ni kuwajibika kwa watu, kuwajibika kwa wale ambao wanakutegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika suala la Zanzibar, limezungumzwa tena mimi nimeshuhudua na inawezekana kwenye rekodi za mtandao ndani ya Bunge inaweza ikaonekana, asilimia kubwa ya Wabunge wa CHADEMA hawakufurahishwa na maneno ya Tundu Lissu alivyozungumzia suala la Zanzibar. Tuko nao na tumewaona. Inawezekana haya ni maneno yake yeye mwenyewe. Lakini si maneno, kwa *ability* na usomi aliokuwa nao yeye lazima aelewé kwenye suala la Katiba, Zanzibar haitaingia kwenye mjadala huu kama ni sehemu ya Tanzania bali itangia kama sehemu ya nchi huru, *as sovereign state.* Kutokuona kwao au kutokuelewa kwao si upofu wa macho yao bali ni upofu wa miyo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa kwenye Bunge la Katiba, wingi wa Wabunge kutoka Chama cha Mapinduzi, hawatatoa Katiba kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi, kamwe hatutafanya hivyo. Tutakaa na kuweka maslahi ya Taifa letu. Tayari tumeshaanza kufanya maboresho, tunaposema Rais ana madaraka mengi, tulitakiwa tuseme hapa, hatusemi kwenye majukwaa, tunakuja kusema hapa na Chama cha Mapinduzi kina Wabunge wengi kitasema. Tumeshasema hapa, Rais sasa hivi hateui Waziri Mkuu, anampendekeza Waziri Mkuu anateuliwa na Bunge. Hii ndiyo fursa, sasa fursa imeachwa, matokeo yake watu wanapita mitaani wanachanganya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania muelewe Bunge la Katiba ambalo ripoti yake itampelekea Rais litafanya kazi kwa maslahi ya Watanzania, litafanya kazi kwa maslahi ya wanyonge wa Tanzania, litafanya kazi kwa niaba ya Watanzania si kwa niaba ya vyama vyetu. Inaelekea labda kuna watu wameona wao watakuwa wachache mule ndani. Tusiende kwa masuala ya *partisan*, twende kwenye masuala ya Utaifa. Tukipata michango kutoka CHADEMA, tukipata michango kutoka CUF, michango kutoka TLP na vyama vingine, tunaunganisha, tunajenga kitu kimoja cha Utaifa na kitu kimoja kinakuwa ndiyo dira na mwongozo wa Taifa letu na Rais wetu ndiye anayetuongoza. Huwezi leo ukasema wananchi wakikataa mpango wa Katiba Mpya tusiendelee na Katiba ya zamani. Tumo humu kwa sababu ya Katiba ya zamani na uhalali wa Katiba ya zamani ndiyo imefanya Wapinzani waingie humu ndani. Leo tumelisahau hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine. Nilitaka kidogo Mheshimiwa Waziri, Ibara ya 18 inasema: "Baada ya Tume kumaliza kazi yake itawasilisha ripoti kwa Rais na Rais wa Zanzibar." Sawa hilo sina tatizo nalo, lakini baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar na baada ya kukamilisha majadiliano kuhusu masuala ya kisera na taratibu za kiutendaji, Rais atamwagiza Rais kuwasilisha Muswada wa Katiba katika Bunge la Katiba. Hapa kuwe na muda, uwekwe muda baada ya Rais kupokea ripoti basi uwekwe muda wa kisheria wa yeye kulianzisha na kuliamrisha Bunge la Katiba lianzie kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niingie kwenye Ibara ya 1(2), inasema: "Sheria hii itaitwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011, Sheria hii itaanza kutumika tarehe 1 Desemba." Mimi sioni sababu kwa nini tunaandika tarehe moja Desemba? Hapa iandikwe: Sheria hii itaanza kutumika baada ya Rais kuanguka na kutia mkono wake. Hatuna ulazima wa kuweka tarehe, Rais anaweza akapata majukumu mengine, anaweza akasafiri, akachelewa kusaini hii Sheria ikashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niwakumbushe wananchi kuwa tunaandaa *Roadmap*. *Vehicle* ya *roadmap* hii ni wananchi, si vyama. Wananchi ndiyo watakaoamua hatma ya nchi yao. Juzi tumeona viongozi wa wafanyakazi wanajidanganya na wanajipotosha. Hiki ndiyo kipindi cha kutoa maoni, mali zetu zinalindwa vipi ndani ya Katiba yetu. Kama tunasema Rais ana madaraka mengi, tunamuainishia ndani ya Katiba madaraka yake, anaweza kuteua Waziri, akateua Mkuu wa Majeshi, akateua Jaji Mkuu lakini Bunge ndiyo litakalokuja kuidhinisha. Haya maneno hayawezi kujumuishwa kama yatazungumzwa mitaani. Ni lazima wote kwa pamoja tukae tuweze kusema madaraka ya Rais na kikomo chake kitafika wapi. Tumeona nchi nyngi kama Marekani, wanateua, Rais ana-*nominate* lakini Bunge ndiyo linapitisha na hapa tunawenza tukafanya hivyo hakuna ubaya wowote. Lakini hatuwezi kufanya kama hatuonge na *spirit* ya Utaifa, hatuwezi tukapata maoni kuhusu maslahi ya wafanyakazi kwa sababu na wao watagoma kutoa maoni ya maslahi yao, hatutawenza kufanya kama wananchi watashawishika kugoma hata kutokusaidia maslahi ya akinamama, maslahi ya walemovu, maslahi ya watoto yatima na maslahi ya rasilimali ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niyasema hayo na juzi kama mmeona tarehe 14, Tume iliyoteuliwa na Rais imeapishwa, tena wenzetu kule wameapishwa na *Attorney General*, wameshaanza kazi, jirani tu hapa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na naomba wananchi wa Tanzania tuwe wamoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako, nakushukuru sana.

Kwa vile muda umeshatutupa mkono sana, kabla ya kuahirisha shughuli zetu hapa, naomba nitoe matangazo kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, Ndugu John Joel, anaomba niwatangazie kwamba kesho tarehe 17/11/2011, hakutakuwepo na kipindi cha maslahi kwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 38 (5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, hivyo nawaomba msiende kujorodhesha majina yenu.

Pili, mjadala wa Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba utaendelea kesho hadi saa saba mchana Bunge litakapositishwa hadi tarehe 18/11/2011 saa tatu asubuhi.

Tatu, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, itakutana kesho mchana pamoja na Waziri ili kuititia kwa pamoja mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Waheshimiwa Wabunge ambao watapenda kushiriki katika Kikao hicho mnaruhusiwa kufanya hivyo.

Nne, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba utahitimishwa tarehe 18 siku ya Ijumaa asubuhi kabla ya saa saba na kutokana na mabadiliko hayo, tunesambaza kwenu ratiba ya marekebisho ya Mkutano huu wa Tano kama ambavyo mmeshagawiwa na inavyoonyesha.

Baada ya tangazo hili, naomba niwatangazie wale ambao kesho mara baada ya maslahi wataanza kuchangia, ni Mheshimiwa Shah, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Bernadetha Mushashu na wengine watatangazwa kadri tutakavyokuwa tunaendelea.

Nawashakuru sana kwa ushirikiano wenu ambao mmeuonyesha na kwa michango yenu kwa ajili ya Taifa letu. Naahirisha shughuli hizi za Bunge hadi kesho, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 17 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi)